Ufafanuzi Wa Agano Jipya

1 Wathesalonike - 2 Timotheo

Na Dorothy Almond

mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa Agano Jipya

African Pastors Fellowship

1 Wathesalonike - 2 Timotheo

Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org

Nyaraka kwa Wathesalonike

YALIYOMO

UTANGULIZI

(a) Mji wa Thesalonike: Jiografia na Historia yake:

(b) Uhusiano wa Paulo na Wathesalonike:

(c) Tarehe ya kuandikwa: Waraka wa kwanza:
Waraka wa pili:

(d) Ujumbe uliohubiriwa:

(e) Sababu za kuandikwa: Waraka wa kwanza:
Waraka wa pili:

UFAFANUZI

WARAKA WA KWANZA:

1:1 Salaam:
1:2-4 Maombi ya shukrani:

1:5 - 2:16 MAKUMBUSHO JINSI KANISA LILIVYOZALIWA THESALONIKE
1:6 - 2:12 Usafi wa nia ya wahubiri na kujitoa kwao
2:13 Walileta Neno la Mungu.
2:14 - 16. Mateso

2:17 - 3:13 .MAKUMBUSHO JINSI KANISA LILIVYOSIMAMISHWA
2:17 - 3:5 Paulo amejaribu kuwafikia, akashindwa, kwa hiyo alimtuma Timotheo
3:6 - 10 Ripoti ya Timotheo
3:11-13 Maombi ya Paulo

4:1-12 KUWASIHI KUISHI MAISHA YA KIKRISTO
4:1-8 Waishi maisha safi
4:9-10 Wapendane
4:11-12 Waishi kwa utaratibu na adabu

4:13-5:11 MATATIZO KUHUSU KURUDI KWA YESU
Itakuwaje kwa waliokufa kabla hajarudi Bwana
5:1-3 Wakati wa Kuja
5:4-11 Kuwa watoto wa mchana

5:12-22 KUWASIHI MAMBO MBALIMBALI

5:23-28. MWISHO

WARAKA WA PILI:

1:1-2 Salaam

1:3-12 KUWATIA MOYO KATIKA MATESO NA DHIKI
- 1:3-5 Shukrani na sifa
- 1:6-10 Hukumu ya Mungu
- 1:11-12 Maombi ya Paulo kwa ajili yao

2:1-17 KUWATIA NURU KWA NJIA YA MAFUNDISHO
- 2:1-2 Siku ya Bwana haijaja bado
- 2:3-12 Ukengeufu mkuu utatokea
- 2:13-15 Shukrani na kuwatia moyo
- 2:16-17 Maombi kwa ajili yao

3:1-15 KUWAWEZESHA KUISHI MAISHA YA KIKRISTO
- 3:1-2 Paulo alitaka wamwombee
- 3:3-5 Uaminifu wa Mungu
- 3:6-9 Neno la Mungu na kufuata kielelezo cha Paulo
- 3:10-15. Maonyo kwa wasioenenda kwa utaratibu na wasioshika maagizo

3:16-18 MWISHO

UTANGULIZI

Nyaraka hizi za Wathesalonike ni za mapema sana na kati ya maandishi ya kwanza kabisa ya Kikristo.

Tunapozisoma tujaribu kujiweka mahali pa wenzetu wa kwanza walipozipokea na kuzifurahia na kuzifaidi.

Zinatupa picha kuhusu maisha na huduma ya wale waliowaletea Injili, jinsi walivyojitoa kabisa ili Kanisa lizaliwe pale. Pia zinatoa picha ya maisha ya wale walioupokea ujumbe na kutufahamisha ni mambo gani waliyofundishwa kuwa msingi wa imani, na ni yapi yaliyo muhimu ya kuamini na kuishi kwayo, na kutuonyesha walitakiwa kuachana na nini katika maisha yaliyotangulia, na kupambana na nini katika maisha ya kila siku, na matumaini yao ya mbele kuwa nini.

Barua hizo ziliandikwa kwa watu walioishi kweli ambao walikabiliwa na matatizo na magumu ya ulimwengu ulio kinyume cha imani ya Kikristo.

Tukumbuke kwamba wakristo katika ulimwengu wote walikuwa wachaohe, ni watu wapya, maana ni kama miaka ishirini tu tangu Kristo kuishi duniani. Kwa sababu sisi nasi tunaishi katika ulimwengu usioipenda imani ya Kikristo barua hizo zitatutia moyo wa kuendelea kumfuata Kristo kama zilivyowasaidia wenzetu wa zamani.

MJI WA THESALONIKE:

Jiografia na Historia yake: Mji wa Thesalonike upo mpaka leo. Kwa muda mwingi umeitwa Salonika na siku hizi katika vitabu vya utalii huitwa Thesaloniki. Ni mji mkubwa, unavyo viwanda vya kazi na uchumi unasitawi. Kwa upande wa idadi ya wakazi ni wa pili kwa Athene, jiji kuu la Uyunani wenye wakazi kama laki tatu.

Zamani ulikuwepo mji ulioitwa Therme kutokana na chemchemi za maji zilizokuwepo. Mwaka wa KK315 Mtawala Cassander aliujenga Thesalonike na kuuita hivyo kufuatana na jina la dada wa upande mmoja wa Iskanda Mkuu. Warumi wakaushinda mwaka KK168 na kuuweka kuwa mji mkuu wa jimbo la Makedonia mwaka KK164. Barabara kuu kutoka Rumi hadi mipaka ya mashariki ya Dola ilipitia pale na bandari yake ilitumiwa sana. Picha tunayopata ni ya mji wa maendeleo, kwa mfano Paulo alitaja kwamba wanawake wenye cheo waliguswa na Injili. Wakazi yapata laki mbili waliishi pale, wengi wao Wayunani, pamoja na Warumi, na Wayahudi.

Miji mingi iliyotajwa katika Agano Jipya imetoweka, lakini Thesalonike umedumu mpaka leo

UHUSIANO WA PAULO NA WATHESALONIKE:

Katika Matendo 17:1-15 mwandishi Luka ametuambia jinsi Paulo na wenzake walivyofika Thesalonike kwa mara ya kwanza na kuanzisha Kanisa pale. Paulo alikuwa akiuitika wito alioupata kwa njia ya maono ya usiku wakati alipokuwa Troa, taz. Mdo.16:9. Jambo hilo lilitokea katika safari ya pili ya kuhubiri Injili iliyofanyika kama BK49-50. Yeye pamoja na wenzake Sila na Timotheo, na Luka aliyejiunga nao wakavuka Bahari kutokaTroa na kufika Filipi. Pale walihubiri na kupata waamini, Lidia, mkuu wa gereza, na wengine. Walitendewa ujeuri na kushtakiwa kwa uongo na Paulo na Sila walifungwa gerezani. Mungu alifanya mwujiza wa kuwatoa. Wakaondoka Filipi, wakitembea kwa miguu kwa maili kama mia mmoja mpaka wakafika Thesalonike.

Njiani walipitia miji miwili ya Amfipoli na Apolonia, hatuambiwi kwamba walihubiri humo. Desturi ya Paulo ilikuwa kuhubiri katika miji mikubwa na kuwaachia waamini kufanya uinjilisti katika miji na vijiji vilivyowazunguka.

Paulo alipewa na Mungu utume kwa wamataifa - Mdo.9:15. Hata hivyo kila mara alianzia kwa Wayahudi kama wakiwepo. Katika sinagogi watu walifahamu Agano la Kale, na Torati, wakitumaini kumpata Masihi wao aliyeahidiwa. Paulo alifahamu watamsikiliza kwa makini atakapoyafafanua Maandiko yao. Katika mpango wa Mungu Injili ni kwa Wayahudi kwanza taz. Rumi 1:16. Pia Paulo kama Myahudi alikuwa na mzigo juu ya watu wake - Rumi 9:1-3 na 10:1.

Katika sinagogi Paulo alikutana na wamataifa wengine ambao walikuwa wamejiunga na Wayahudi katika ibada. Baadhi ya hao waliitwa "wamcha Mungu" na baadhi "waongofu". Hao waongofu walijiunga kikamilifu kwa njia ya tohara. Paulo alivuta wengi katika "wamcha Mungu" na kwa njia yao alipata daraja ya kukutana na wamataifa wa nje.

Pale Thesalonike walianzia katika sinagogi na kila sabato kwa majuma matatu walipewa nafasi ya kuhubiri. Hasa waliwaelezea kutoka Maandiko yao juu ya Kristo kuwa Masihi wao wa kweli. Walifanikiwa kupata waamini, Wayahudi na Wayunani na wanawake wenye cheo - Mdo.17:4. Wayahudi wasiokuwa tayari kuamini walijaa wivu nao wakatumia wahuni wa mjini kutokeza ghasia na kuwashtaki Paulo na wenzake kuwa asili ya ghasia hiyo.

Je! walikaa muda gani? majuma hayo matatu tu? Hatujui kwa hakika. Yawezekana walikaa zaidi, ila hawakukaa muda mrefu. Tunajua walikaa muda wa kutosha kupokea msaada kutoka waamini wa Filipo - Fil.4:16. Pia, Paulo alifanya kazi ya kujitegemea - 1 Thes.2:9 na 2 Thes. 3:6-15. Kama alikaa majuma matatu tu, kweli aliwafundisha mengi sana katika muda huo mfupi!

Iwapo hawakukaa muda mrefu walipoondoka Kanisa limezaliwa, lenye waamini walio hai, wenye nguvu, walio tayari kupambana na magumu na mateso, na wenye mzigo wa kumshuhudia Kristo.

Yawezekana miongoni mwao ni Aristarko, Sekundu, na Yasoni, - Mdo.20:7. waamini walikuwa mchanganyiko wa Wayahudi kwa Wayunani, wanaume kwa wanawake, waliomcha Mungu na waliotoka katika upagani.

Paulo aliposhindwa kuwafikia tena mapema alimtuma Timotheo, na Timotheo aliporudi baada ya kuwaona ndipo Paulo aliuandika waraka huo, 1 Thes.2:17-18 na 3:1-2.

TAREHE YA KUANDIKWA KWA WARAKA WA KWANZA NA WA PILI:
Kutokana na nyaraka zenyewe ni dhahiri kwamba waraka wa kwanza uliandikwa muda mfupi baada ya Paulo kuwepo na wa pili ulifuata ule wa kwanza bila kukawia.

Tunajua ya kuwa walikuwa Thesalonike kati ya BK49-50 hivi, kwa hiyo waraka wa kwanza uliandikwa kama mwishoni mwa BK50 na baada ya muda mfupi aliwaandikia tena.

Paulo alikuwa Korintho alipoziandika.

UJUMBE ULIOHUBIRIWA:
Kama ambavyo tumekwisha kusema Paulo alipofika Thesalonike alitumia sinagogi kuwa mahali pa kuanzia. Kwa sababu ya Wayahudi kuwa na msingi wa Maandiko ilikuwa rahisi kwa Paulo kuyatumia Maandiyo hayo na kuwaelezea juu ya tumaini lao kubwa la kumpata Masihi wao. Aliwathibitishia kabisa kwamba Yesu Kristo ndiye huyo Masihi wao kwa kweli aliyetumwa na Mungu. Ila kazi kubwa aliyokuwa nayo Paulo ni kuwasaidia kuelewa kwa nini ikiwa Kristo ni Masihi wao mbona alisulibiwa? Msalaba ulikuwa kikwazo kwelikweli. Paulo alionyesha kwamba neno hilo lilitabiriwa na Isaya katika unabii wake - Isa.53, na hata Pasaka na Mwana Kondoo kuchinjwa kwa ajili ya kuwakomboa kutoka utumwani mwa Misri ni mfano wa "Mwana Kondoo wa Mungu" aliyetumwa kutukomboa kutoka utumwa mwa dhambi. Wakichunguza Maandiko yao watatambua kwamba msingi wa dhabihu zao, mipango ya ibada katika hema na hekalu, taratibu za kuwa na Kuhani Mkuu n.k. hayo yote hushuhudia njia ya ukombozi kuwa kwa kumwaga damu.

Bila shaka Paulo alionyesha kwamba iwapo Kristo alikufa, siku ya tatu alifufuka kutoka kwa wafu, ishara ya kuwa Mungu amekubali kazi yake ya msalabani na kumpokea na kumwadhimisha.

Paulo alipowahubiri wamataifa wasio na Maandiko wala msingi wo wote wa tumaini la kumpata Masihi, alihubiri Yesu kuwa Mfalme atakayerudi baadaye - 1 Thes.1:7 na kukaza ya kuwa Mungu yu hai na wa kweli tofauti na sanamu zao zisizo hai 1 The.1:9.

Nyaraka zote mbili zinakaza Kurudi kwa Bwana Yesu, inaonekana kwamba Paulo alihubiri habari hiyo kwa nguvu, hata kiasi cha wengine kuacha kazi wakidhani Yesu atatokea mara, na wengine walipoona wenzao wamekufa walikuwa na wasiwasi itakuwaje kwao.

SABABU ZA KUZIANDIKA: WARAKA WA KWANZA:
WARAKA WA PILI.

Kwanza alitaka kuwahakikishia upendo wake na mzigo alio nao kwa ajili yao. Tukumbuke ya kwamba aliwaacha kwa haraka, akiondoka usiku. Alitamani sana kuwaona tena, na mara mbili alijaribu kuwafikia, akashindwa. Adui zake walitumia neno hilo na kusema hakuwa na mzigo na ya kuwa alihubiri kwa

lengo la kupata fedha, na ya kuwa alikuwa na mambo ya chini-chini. (siku zile wengi walitembea huko na huko wakifundisha filosofia mbalimbali na imani mbalimbali, wakidanganya watu, wakitafuta fedha za kuishi).

Katika nyaraka hizo Paulo anajitetea sana, ni kama anayajibu mashtaka mbalimbali. Kwa hiyo sababu mojawapo ya kuwaandikia ni kuyajibu, maana alifahamu kwamba kama watu wataanza kuwa na mashaka juu yake na nia yake ndipo watapoa kiroho. Aliwakumbusha juu ya kuishi kwake alipokuwa nao, jinsi alivyovumilia magumu mengi na mateso, uaminifu wake katika kujitegemea na usafi wa nia yake.

Sababu nyingine ilikuwa kuwajenga katika imani yao na kuwapa mafundisho zaidi juu ya Kurudi kwa Yesu. Wengine walikuwa hawakumwelewa vema, na matatizo yametokea kwa sababu wengine walidhani Kristo atarudi mara, kwa hiyo waliacha kazi na wengine walikuwa na mashaka juu ya waamini waliowahi kufa.

Katika waraka wa pili tunapata habari ya uvumi uliozuka kati yao uliosema kwamba Siku ya Bwana imekwisha kuwepo.

Sababu nyingine ni kwamba Timotheo aliyetumwa kwao amerudi na ripoti nzuri iliyomtia moyo Paulo na kumfanya apumue kwa upya. Kumbe kazi yake si bure. Waamini walikuwa wakiendelea, wamesimama imara hali wanaendelea kuteswa na kupata dhiki nyingi. Kwa barua hiyo alikusudia kuwatia moyo wa kuvumilia akiwahakikishia maombi yake.

Sababu nyingine alitaka kukaza umuhimu wa kuishi maisha safi na kuwa na mwenendo wa utaratibu wa kujali kazi na kuheshimu viongozi wao.

UFAFANUZI WA WARAKA WA KWANZA

1:1 Salaam Paulo alianza barua yake kwa kufuata kawaida ya siku zile. Alijitaja kwanza pamoja na wenzake waliokuwa pamoja naye alipofika Thesalonike. Silvano ni sawa na Sila kifupi chake. Halafu alitaja walioandikiwa. Alieleza mawili kuhusu Kanisa la pale. Kijiografia Kanisa liko Thesalonike, ni la pale pale. Kiroho ni "katika Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo". Alimweka Yesu pamoja na Mungu kwa ukaribu sana, ushuhuda wa kuonyesha kwamba wakristo walimwamini Yesu kuwa Mungu, mwenye umoja kamili na Baba.

Katika salaam aliwatakia mawili, "neema" na "amani" - mawili yatokanayo kwa Injili. "Neema" maana yake ni kupokelewa bila masharti na Mungu kwa njia ya imani. Tunda la "neema" ni "amani" amani ya moyoni kwa sababu ya upatanisho Yesu alioufanya msalabani alipokufa kwa dhambi zetu

1:2-4: Maombi ya shukrani: Sikuzote Paulo alimshukuru Mungu kwa ajili ya waamini katika makanisa mbalimbali. Kwa nini? Ni kwa sababu alijua kwa uhakika ya kuwa bila Mungu kuwa amefanya kazi mioyoni mwa watu alipowahubiri, na bila Mungu kuendelea kuwasaidia yeye asingaliweza lo lote. Kila mara alikumbuka hali za watu alipowakuta kwa mara ya kwanza na jinsi walivyobadilika ki-maisha baada ya kuamini.

Alikuwa ameishuhudia nguvu ya Injili. Katika maombi aliwakumbuka mmoja mmoja mbele za Mungu, hakumshukuru Mungu kwa jumla yao bali kwa kumtaja mmoja mmoja pamoja na hali zao. Wathesalonike walimfurahisha sana - walijulikana kwa imani yao iliyofanya kazi, na kwa upendo wao wa kuwa tayari kutaabika kwa ajili ya wengine, wakitumika kiasi cha kuchoka bila kujijali, na kwa saburi yao, wakimtumaini Kristo kabisa na kutazamia Kurudi Kwake. Matatu hayo - imani, upendo, subira ni makubwa na yamewekwa pamoja mara nyingi - taz. 1 Thes.5:8; Rumi 5:2-5; Gal.5:5-6; 1 Petro 2:21ku. Ebr. 6:10-12; Ko1.1:4ku. 1 Kor.13:13.

Kwa hiyo wakristo hao walikuwa na sifa kubwa, wakikua kiroho na kuimarika ki-imani.

k.4. Paulo alitumia lugha ya kuonyesha jinsi alivyowapenda aliwaita "ndugu", alitumia neno hilo mara 21 katika nyaraka hizo mbili. Zaidi ni "ndugu wanaopendwa na Mungu" - wote ni ndugu, Wayahudi kwa wamataifa, maskini kwa matajiri. Zamani Paulo alikuwa Farisayo mwenye kujaa kiburi na kujiona ni bora, akidharau wamataifa. Sasa kwa njia ya msalaba kiburi chake chote kimekwisha, uadui umebomolewa, yeye yu tayari kumwita yeyote amwaminiye Kristo ndugu yake, tena kwa furaha kubwa. Huo undugu wa Agano Jipya ni undugu katika Kristo, nao huzalishwa kutokana na uteule wa Mungu - wamependwa na Mungu na kuitwa naye kumpokea Kristo.

Kwa nini Kanisa lilizaliwa pale Thesalonike? Jibu lapatikana katika k.4 na k.5. Asili kabisa ni "mapenzi ya Mungu" aliyewoteua kumwamini Kristo. Paulo alisema alijua uteule wao. Kwa upande mmoja ni vigumu kufikiri kwamba mwanadamu awaye yote aweza kujua jambo kama hilo, ambalo limo madarakani mwa Mungu. Hata hivyo dalili ziko zinazoweza kumwelekeza mtu kuutambua uteule huo. Moja ni itikio la Wathesalonike Injili ilipohubiriwa kwao.

Iwapo haikuwa rahisi baadhi yao walimkubali Kristo. Tena wameendelea kumfuata katika dhiki na mateso. Hayo yote ni dalili ya kazi ya Mungu maishani mwao.

Uteule wa Mungu hutokana na upendo wake, hautegemei mambo ya nje kama hali zetu. Taz. Kumb.7:6-8; Mal1: 1-2.

k.5 Paulo amesema "Injili yetu", kwa nini aseme "yetu"? Ni kwa sababu ni wao walioileta Thesalonike, tena hao Wathesalonike wameipokea na kuishi kwayo.

Injili ni "nguvu ya Mungu" haiwi maneno tu, ni ujumbe wenye uwezo wa Mungu ndani yake, uwezo uletao wokovu - Rumi 1:16; 1 Kor.1:18. Paulo ameshuhudia nguvu yake katika safari zake. Kwa lugha ya "katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi" yawezekana miujiza ya uponyaji n.k. ilitokea kuthibitisha ukweli wa Neno lililohubiriwa.

Iwapo msingi wa kuzaliwa kwa Kanisa miongoni mwao ulikuwa katika uteule wa Mungu, hata hivyo wahubiri na tabia zao na kwa kujitoa kwao, walifungua njia kwa Mungu kutenda kazi.

1:5-2:16. MAKUMBUSHO JINSI KANISA LILIVYOZALIWA THESALONIKE

1:6-2:12. Usafi wa nia ya wahubiri na kujitoa kwao

Tumekwisha kuona ya kuwa asili kabisa ya kanisa kuzaliwa pale ni mapenzi ya Mungu. Ila tuliona ya kuwa kwa tabia zao na kwa kujitoa kwao wahubiri walifungua njia kwa Mungu kutenda kazi. Paulo hakusikia wasiwasi yo yote kuhusu jinsi alivyoishi kati yao. K.5b amesema "kama vile mnavyojua jinsi zilivyokuwa tabia zetu kwenu kwa ajili yenu". Yeye na wenzake walitoa kielelezo chema, hata aliweza kusema kwamba "mkawa wafuasi wetu na **wa Bwana".** Katika kuwaiga walikuwa wakimwiga Bwana Yesu!!! Bila shaka ni wachaohe wetu ambao twathubutu kusema hivyo!!.

Haikuwa rahisi waamini, walipatwa na dhiki na mateso. Yapo mawili ambayo daima huandamana katika maisha ya Kikristo dhiki na furaha ya Roho Mtakatifu. Katika maisha ya Bwana Yesu ilikuwa hivyo, na ni ahadi yake kwa wafuasi wake Yoh.16:33. Paulo alijua ni hivyo, naye aliwafundisha waamini wawe tayari kwa dhiki na mateso, maana ni fungu lao. Mdo.14:22.

Mtu huwa na faida gani katika mateso na dhiki kwa ajili ya imani yake? Faida anayopata ni kutambua kwamba imani ni kitu cha thamani sana. Pia anahakikishiwa ukweli wa imani yake anapoona anazikanyaga nyayo zile zile

alizozikanyaga Bwana Yesu. Hayo yampa furaha ya kweli, ya ndani, akionja msaada wa Roho Mtakatifu, na kujua hakika ya kuwa ni mtoto wa Mungu.

1:7-8: Katika k.5 Paulo amewasifu kwa tabia ya upendo, imani, na tumaini. Ila pamoja na hayo wametoa kielelezo chema kwa wengine. Ni wapya katika imani hiyo ya Kikristo, hata hivyo imani yao ilikuwa ikizungumziwa na watu wa mbali, katika majimbo ya Makedonia na Akaya. Ni kama wamepiga tarumbeta kwa sauti kuu na ya wazi, na wanaendelea kufanya hivyo. Na maisha yao yameunga mkono ushuhuda wao wa mdomo na wengi wameletwa kufikiri sana juu ya Injili.

1:9-10: Ni nini yaliyozungumziwa? Kwanza ni jinsi hao watu walivyoacha sanamu zao na miungu yao na kumgeukia Mungu aliye hai na wa kweli na kumtumikia. Jambo kubwa **waliacha** sanamu zao, hawakuridhiana na mambo ya maisha yaliyatangulia. walimgeukia Mungu kwa mioyo yao yote. waliamini nini? Waliamini kwamba Yesu Kristo alifufuliwa na Baba yake kutoka kwa wafu, naye atarudi tena kuchukua walio wake. Waliamini kabisa kabisa, walikuwa katika hali ya kumngojea.

Tena waliamini ya kuwa Kristo amewaokoa katika hatari kubwa ya kupatwa na hukumu ya Mungu. Kwa sababu ya kifo cha Yesu msalabani hawatapatwa na hukumu hiyo.

Kwa hiyo twajua ni mambo gani Paulo aliyohubiri yaliyowavuta kumwamini Kristo. Bila shaka waliwashuhudia wenzao habari hizo. Katika K.8 Paulo amesema kwamba Neno la Mungu limevuma si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo imeenea – si ajabu Paulo alifurahishwa nao.

Katika sura ya pili Paulo alijitetea sana. Kwa nini ajitetee? kwa sababu ya mashtaka mbalimbali kutoka adui zake, tukikumbuka ya kwamba wapinzani walimlazimisha kuondoka kwa haraka na bila shaka waliendelea kuwapinga waamini. Alianza kwa kusema juu ya usafi wa nia yake na ya wale waliokuwa pamoja naye. Alijua Wathesalonike walielewa kabisa jinsi walivyoishi na kujitoa, ni kama kuwakumbusha tu. Wangalikuwa na mashaka ingalikuwa vigumu waupokee ujumbe wao. Mahubiri yao yalitokeza mema katika maisha yao.

2:1: Kuja kwao hakuwa bure, maisha ya watu yaliguswa, na mabadiliko yaliyotokea yalidumu. Tena kuamini kwao hakuwaletea faida yo yote bali mateso na dhiki tu. Paulo alipawajia alikuwa na shabaha maalum na wakati

wote alihofu kufanya kazi bure. Taz. Gal.2:2; Fil.2:16; 1 Thes.3:5; 1 Kor.15 (mara 3).

Katika kujitetea aliendelea kwa kuwakumbusha jinsi alivyokuja kwao kutoka Filipi, hali ameumizwa kimwili na kuaibishwa kwa kufanyiwa kinyume cha uraia wake alipopigwa na kutiwa gerezani. Usafi wa nia yake ulionekana, kwa sababu alithubutu kuendelea na kazi yake na huduma ya kuihubiri Injili, potelea mbali atapatwa na magumu gani.

Tunafundishwa kwamba kama mtoto hazaliwi bila utungu wa mama yake, vivyo hivyo watoto wa kiroho, wa imani, hawazaliwi bila utungu wa wahubiri na watumishi wa Mungu. Makanisa hayatokei bila watu kujitoa. Paulo na wenzake hawakukata tamaa wala hawakukata shauri la kurudi makwao. Walidumu waaminifu kwa ujumbe uliosababisha vipingamizi vingi. Ujasiri na uthabiti wao haukuwa na asili ndani yao, bali waliupewa na Roho Mtakatifu - taz. k.2. "twalithubutu **katika Mungu** kuinena Injili ya Mungu kwenu kwa kuishindania sana". Injili ni "ya Mungu" kwa sababu ni mpango wake halisi kwa wokovu wa wanadamu. Hapo nyuma alisema Injili ni "yetu".

Waliishindania sana, kwa sababu ya upinzani. Tukumbuke ya kuwa baada ya majuma matatu kuhubiri sinagogini wivu wa Wayahudi ulifunga nafasi hiyo.

Twafundishwa kwamba Shetani hutumia njia mbalimbali za kuzuia Injili - mashtaka ya uongo juu ya wahubiri, kuziba nafasi, kutia mashaka juu ya nia na sababu zao, hata kutumia nguvu za kimwili na kuwashambulia; n.k

2:3: Paulo aliendelea kukaza usafi wa nia zao - siku zile wengi walitembeza elimu na mafundisho wakitembea- tembea huko na huko, hali wakitafuta mapato ya kuishi, bila kuwa na mzigo juu ya mafundisho yao.

Paulo alikataa mashtaka matatu: i. "maonyo yetu si ya ukosefu", ameuita ujumbe "maonyo" kwa sababu ulilenga maisha si jambo la kichwani tu. Ulikuwa na shabaha ya kuwaelekeza watu kwenye maisha mema na ya kweli, haukuwa ya kuwakosesha.

ii. "wala ya uchafu" ujumbe wao uliwaelekeza wasikilizaji juu ya usafi wa maisha, wakifundisha kwamba Mungu wa kweli ndiye Mungu Mtakatifu, anayetaka watu wake wawe watakatifu, kinyume cha siku zile za watu kufikiri uasherati ni jambo la kawaida tu, na hata katika dini mbalimbali ulikubaliwa.

iii. "wala ya hilo" hawakushawishi watu kinyume kwa kuahidi ahadi za uongo, bali waliwatoboa wazi ugumu wa kumfuata Kristo na kuwatayarisha kwa dhiki na mateso, ila pamoja na dhiki n.k. wataurithi ufalme wa Mungu.

2:4-5: Paulo na wenzake walithamini sana kazi yao na ujumbe wao. Ni Mungu aliyewakabidhi hiyo kazi na huo ujumbe na kuwatuma. Walihesabu wamewekewa amana, na Mungu amewapima kuona kama wamestahili kukabidhiwa. Kwa heshima waliyopewa na Mungu shabaha yao ilikuwa kumpendeza, kwa hiyo hawatajipendekeza kwa wanadamu, kwa kuupunguza uzito wa Injili wala kuulainisha ili watu wasikwazwe nayo. Maana watu hawapendi kuambiwa kwamba ni wenye dhambi wasioweza kujiokoa, ambao bila Kristo watapotea.

Pia, hawakuwa na choyo iliyofichwa chini ya maneno matumu, la. Walijitegemea kwa riziki kwa kufanya kazi mchana na usiku. Hawakutafuta vitu vya watu wala sifa zao, kitu kimoja tu, walitaka watu wampokee Kristo kama Bwana wa maisha yao.

k.7. Waliishi kati ya Wathesalonike kama "mlezi awatunzavyo watoto wake wenyewe", walikuwa wapole kwao. k.11. Pia, waliishi kati yao kama "baba" kwa kuwaonya kama baba amwonavyo mwana wake, si kwa ukali bali kwa upendo, na kwa kuwatia moyo, wawe na mwenendo mzuri. Walikaa na mmoja mmoja na kuzungumza naye na kumsaidia. Hawakujifanya kuwa mabwana juu yao, walijinyenyekeza, wala hawakufanya kwa mradi tu, kama ni kazi tu, wala kwa ubaridi wa moyo, bali walijitoa kabisa kwao kibinafsi kwa upendo na furaha.
Walikuwa na masumbufu mengi, kimwili walichoka sana kwa kuishuhudia Injili mchana halafu kufanya kazi za mikono usiku kwa riziki, kusudi wasiwalemee.

2:10: Tena, alijitetea juu ya mwenendo wao, waliishi kwa utakatifu, na kwa haki, na bila lawama. Hakuwa na wasiwasi, alisema Mungu ni shahidi, hamna mashtaka ya kweli.

Shetani anajua kwamba akiweza kufanya watu wawe na mashaka juu ya watumishi wa Mungu itakuwa rahisi kuharibu kazi zao. Ni muhimu sana kwa habari yo yote juu ya watumishi wa Mungu kuletwa nuruni ili ukweli wake uhakikishiwe, wala tusikubali neno lo lote kabla ya kulichunguza. Pia likanushwe kwa wazi kama halina ukweli.

2:13: Walileta Neno la Mungu. Maana yake ni kwamba walipohubriri na kusema na watu ilikuwa sawa na Mungu kusema nao. Na ndivyo

Wathesalonike walivyolipokea, Kufuatana na ujumbe ulioletwa na tabia zao waliouleta.

Ndiyo sababu walimgeukia Mungu aliye hai na kuziacha sanamu zao na kubadili mwenendo wao. Siri kubwa ya maendeleo yao kiroho na habari zao kuvuma mbali ni hiyo. Yatupasa na sisi nasi kulipokea Neno la Mungu kama ni Mungu Mwenyewe amenena nasi, kwa sababu ndivyo ilivyo.

2:14-16 Mateso: Dalili moja ya kuwa walikuwa wamelipokea Neno la Mungu kweli ni mateso yaliyofuata. Wamefanana na makanisa ya kwanza kabisa kati ya Wayahudi. Yesu Kristo alisulibishwa na watu wake Mwenyewe, na katika historia yao yote wamewapinga waliowaletea Neno la Mungu, hasa manabii wao. Tena licha ya kuwazuia watu wao wamewazuia na watu wa mataifa pia. Kwa Wathesalonike ni kweli, maana ni Wayahudi kwa sababu ya wivu wao waliosababisha fitina kutokea na wahubiri kuondoka. Katika sehemu hiyo Paulo alijifunua wazi moyo wake wa ndani, twaona mtu aliyetawaliwa na Injili si ya ukabila. Je! sisi nasi twatawaliwa na Injili si ya ukabila?

2:17-3:13. MAKUMBUSHO JINSI KANISA LILIVYOSIMAMISHWA:

Tunapopanda mbegu na kuotesha mimea twajua kwamba kazi haijaisha ila inaanza tu. Bila kuitunza mimea kazi zote zilizotangulia zimekuwa bure.

Ndivyo ilivyo katika kazi ya Mungu. Haitoshi kuihubiri Injili na kupata waamini. Waamini huhitaji utunzaji wa kutosha mpaka wawe wamesimama imara na kukua kiroho.

2:17 - 3:5. Paulo alijaribu kuwafikia, akashindwa, akamtuma Timotheo.

Paulo alikuwa ameondoka kwa haraka, usiku, kutokana na juhudi za wapinzani waliotaka kuwakamata. Pia, waamini wapya walipata mateso na dhiki.

Atawasaidiaje? Njia bora ni kwenda kuwaona, lakini kila alipojaribu kwenda alizuiliwa 2:18. Alihesabu ni Shetani anayeleta vizuizi. Kilichozuia hatujui, pengine aliugua, pengine njia zilifungwa, pengine hali zilizokuwepo hazikumruhusu - ni vigumu kujua ni nini, ila kwa kweli alizuiliwa. Alifahamu kabisa kwamba Shetani alikuwa nyuma ya hayo.

Kukosa kufika kuliwapa adui zake nafasi ya kumshtaki kuwa hana mzigo nao, na kama watu wataanza kufikiri hivyo, muda si muda, Kanisa litapoa. Kwa hiyo lazima wafahamu kuwa amejaribu sana kuwafikia, pia ana hamu sana ya kuwaona tena.

2:17-20: Katika vifungu hivi Paulo ametumia lugha ya ajabu kuufunua moyo wake jinsi anavyowaweza.

k.17: Neno "tumefarakana nanyi" ni sawa na kusema "tumefiwa nanyi". Kuwa mbali nao ni sawa na mtu kufiwa. Tena, lugha ya "kutamani" inaonyesha kutaka kwake, anataka sana sana kuwaona. Tena "kwa shauku" ni lugha ya kuonyesha upendo wake na moyo usio baridi.

k.19-20: Paulo aliendelea kuonyesha ukaribu wa uhusiano wake nao. Kwa Paulo na wenzake waamini ni "tumaini lao", "furaha yao", "taji ya kujionea fahari", na "utukufu wao", wakati wa Kuja kwa Bwana Yesu. Kwa nini? ni kwa sababu wao ni ushuhuda wa Utume wao, na thibitisho la wito na huduma yao, ishara na muhuri wa Injili na nguvu zake.

Zamani wafalme walipotoka vitani, hali ya kushinda maandamano ya kuwapokea kwa shangwe yalifanyika, na watu waliwatupia taji za maua na majani ya mitende. Yesu atakaporudi, Yeye aliye Mfalme wa Wafalme, tutamtupia nini, ni taji gani, ni zawadi gani itakayomfurahisha hasa? Paulo alifahamu kitu kitakachomfurahisha ni kuona hao waamini katika makanisa yaliyozaliwa. Ndiopi Paulo na wenzake watafurahi sana kwa kumpatia Bwana Yesu wafuasi wengi, walio waaminifu hadi Bwana wao arudi. Thawabu yao si cheo bali ni watu.

3:1-5: Kumtuma Timotheo:
Aliposhindwa kuwafikia aliona vema kumtuma mmoja wa timu yake aliyekuwa naye walipofika mara ya kwanza, Timotheo. Mzigo wake umeonekana katika lugha ya k.1. "tulipokuwa hatuwezi kuvumilia zaidi".

Paulo alihitaji msaada wa wenzake hasa katika miji mikubwa iliyojaa sanamu na aina aina za elimu na mafundisho na dini, mji kama Athene mahali alipokwenda alipofukuzwa Thesalonike. Hata hivyo alikuwa tayari kuachwa peke yake kwa ajili ya waamini wa Thesalonike. Neno ambalo Paulo alitumia kwa kuachwa lina nguvu, Paulo alisikia upweke kama wa mtu aliyefiwa au wa wazazi mwana wao anapoondoka nyumbani wakati wa kuoa.

Kwa hiyo twaona kwamba Paulo hakuwa mwinjilisti tu, bali alikuwa mchungaji/pasta pia. Waamini walihitaji kutunzwa na kuchungwa. Alifanana na Bwana Yesu aliyejiita Mchungaji Mwema Yoh.10:12-13.

Maelezo kuhusu k.1 na cha 5 - k.1 "**tu**lipokuwa **hatu**wezi kuvumilia zaidi tuliona vema kuachwa Athene peke **yetu"** ling. na k.5. "kwa hiyo **mimi nami ni**lipokuwa **si**wezi kuvumilia tena, **na**lituma mtu". Yawezekana lugha ya "tu" katika k.1. ni lugha ya uandikaji. Katika Mdo.17:10 Paulo na Sila waliondoka Thesalonike na kwenda Beroya.

Mdo.17:13-14 pale Beroya, shida ilipotokea Paulo aliondoka na Sila na Timotheo walibaki. Paulo aliwaagiza waliomsindikiza kuwaambia Sila na Timotheo waje kwake bila kukawia. Inaonekana Paulo aliondoka Athene peke yake na alipofika Korintho, baada ya muda mfupi hao wenzake walimjia - Mdo.18:1, 5.

Paulo alimthamini Timotheo kama mtumishi mwaminifu atakayewasaidia waamini wa Thesalonike. Lengo hasa ni kuwaimarisha na kuwafariji ili wasifadhaishwe ni dhiki zinazoendelea kuwapata. Ilimbidi Timotheo arudi mahili walipopata fitina na kupingwa. Ila mara nyingi ni Paulo aliyehesabiwa nguzo na kuwindwa, pale Beroya ni yeye aliyeondoka na wenzake walibaki.

Kuwafariji si kuwapa pole bali ni kuwatia nguvu ili wapate moyo wa kuendelea katika kupiga vita ya imani. Katika k.3 Paulo aliwakumbusha jambo moja linaloandama na imani ya kweli. Dhiki ni sehemu moja, isihesabiwe jambo geni. Paulo alitumia lugha ya "twawekewa hizo" ni fungu letu, si ajali wala bahati mbaya - Yoh.16:33, Mdo.14:22.

Wamekwisha kuonja dhiki, na Paulo hakutaka wakate tamaa dhiki zao zinapoendelea. Alijua kwamba Shetani alitaka kuwaondoa kwa nguvu katika imani yao - k.5 "asije yule mjaribu akawajaribu". Kwa kumtuma Timotheo Paulo alikusudia kumwahi Shetani ili asifaulu. Paulo na wenzake walitaabika sana katika kupanda kanisa pale, na sasa Paulo yu tayari kusikia upweke mkali wa kuachwa pale Athene ili Timotheo awafikie na kuwatia moyo, wasije wamefanya kazi bure.

3: 6-10: Ripoti ya Timotheo:
Paulo aliandika waraka huo mara baada ya Timotheo kurudi -k.6
"Timotheo alipotujia hivi sasa".

Alileta habari gani? Kweli alileta habari njema, na Paulo alisikia kupumua kwa upya, Timotheo alipowasimulia habari ya imani na upendo wao na jinsi wanavyowakumbuka vema na hamu yao ya kuwaona, dalili nzuri ya upendo wao. Kumbe, hawajakubali kujali mashtaka ya wale waliosema Paulo alifanya kazi kwa faida yake mwenyewe na ya kwamba hakuwa na mzigo.

Pia, iwapo mateso na dhiki vinaendelea hata hivyo wamesimama imara. Kwa Paulo na wenzake ni furaha kubwa sana kusikia hivyo, ni "kuishi" k.8. Pia ni faraja, kwa sababu hata wao walihitaji faraja kwa sababu ya dhiki na shida walizozipata.

Hao waamini wa Thesalonike ni kama "kipimo cha kuupima uwezo na nguvu ya Injili". Mmea mgeni wa Injili ukipandwa katika ardhi ngumu ya wamataifa, Je! utasitawi?, Je! upeop mkali utauangusha? Je! vidudu watafaulu kuupenya na kuuharibu? Kwa ripoti ya Timotheo jibu ni kwamba mmea mgeni waweza kusitawi, wao ni uthibitisho.

Sasa Paulo na wenzake watazidi kwenda kwa miji mingine na kuhubiri na kupanda makanisa.

3 9-10: Paulo aliendelea akiuliza swali? "ni shukrani gani tuwezayo kumlipa Mungu kwa ajili yenu kwa furaha ile yote tunayoifurahia". Ni wazi Paulo amefurahi sana na kuwa na shukrani nyingi kwa Mungu kwa sababu alifahamu kabisa kwamba ni Mungu aliyefanya kazi mioyoni mwa Wathesalonike, iwapo yeye na wenzake wametaabika kwa ajili yao na Timotheo amewafikia na kuwatia moyo, kwa hiyo twaona jinsi Mungu na wanadamu hukutana katika kufanya kazi yake. Paulo bado angali anataka kuwaona, na kwa juhudi alimwomba Mungu daima ili njia ipatikane. Alikuwa na mawili: i. kuona nyuso zao; ii. kutengeneza mapungufu yao. Kweli wameendelea vema, ila wakati wote wakristo huhitaji kukua kiroho na kusaidiwa ki-maisha na kujifunza zaidi imani yao.

3:11-13: Maombi ya Paulo:
Katika vifungu hivi twafunuliwa ni mambo gani aliyowaombea. Kwanza alimwomba Mungu juu ya kuwafikia. Alipoomba alimweka Yesu Kristo sawa na Mungu Baba na kwa ukaribu sana, hata badala ya kusema "watuongoze njia" amesema **"atuongoze"** hilo si kosa la Kiswahili ila ni tafsiri kamili ya Kiyunani. Amekwisha kuonyesha kwamba hali moja ya sifa kwa hao wakristo ni upendo wao 1:3, kwa hiyo aliomba upendo wao uzidi kati yao na kwa wengine. Halafu aliomba kwamba maisha yao yawe matakatifu, lisiwepo neno litakalosababisha lawama, wawe imara mpaka Bwana Yesu atakaporudi. Ni wazi kwamba Paulo alisema sana juu ya Kurudi kwa Bwana Yesu akiwaelekeza kujiweka tayari kwa wakati huo - ling. 1:10.

4:1-12: KUWASIHI KUISHI MAISHA YA KIKRISTO:

4:1-8 Waishi maisha safi:
Kila alipopanda kanisa Paulo aliwaambia juu ya mwenendo uliopaswa kwa lengo la kumpendeza Mungu. Aliwasihi na kuwaonya wayakumbuke maagizo aliyowapa wasiridhike na hali yao njema bali wazidi kusonga mbele. Mkazo mmoja kuhusu mwenendo wao ni usafi wa maisha ya kimwili. Katika maisha ya nyuma wengi wao walikuwa wamezoea uasherati na uchafu kama ni kawaida ya kuishi. Ilikuwa vigumu wauwaze uasherati kwa uzito. Walipoletewa Injili walifundishwa kwamba Mungu ni Mtakatifu kabisa na walio wake wapaswa kuwa watakatifu.

k.3 Paulo aliweka jambo hilo mahali pa juu: "ndiyo mapenzi ya Mungu kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati". Walipomwamini Kristo walisamehewa dhambi zao na kupewa **Roho** Mtakatifu ili waishi maisha safi. Wametengwa **na** Mungu na kutengwa **kwa** ajili ya Mungu, ili wayafanye mapenzi yake aliyewaita na kuwaokoa. Na mapenzi yake ni "waepukane na uasherati" ki-matendo. Wachukue hatua za kuuepa.

Sote twajua ni nini "kuepa" kitu fulani - kwa mfano: mtu anayetaka kumwepa mtu fulani afanye juu chini asikutane naye, atapiga korna haraka akimwona, akisikia yupo mahali fulani hatakwenda pale. Vivyo hivyo mkristo apaswa kufanya hivi kuhusu uasherati.

k.4. Haitoshi asifanye tu, yampasa auheshimu mwili wake na kuutawala.
k.5 Wamataifa hawamjui Mungu. Paulo alisema katika Rumi 1:18-24 kwamba wamekataa kujua Mungu ndiyo sababu wameshindwa na tamaa mbaya.

k.6. Pia uasherati ni "kumpunja mwingine" - neno la ajabu kwa sababu kupunja lahusu eneo la haki. Kwa hiyo haki inaingia wapi" Mtu anapoingia maisha ya ndoa ana haki gani? Ana haki ya kutazamia mwenzake atakuwa "bikira" au "mseja safi". Vilevile katika ndoa kila mmoja ana haki ya kuwa mwenzake ameachana na wengine wote. Kwa hiyo aliyefanya uasherati au atakayezini atakuwa amempunja mwenzake!! amekosa kumpatia mwenzake haki yake.

Paulo alifundisha kwamba uasherati na uchafu huleta ghadhabu ya Mungu. Ef.5:5; Ebr.13:4; Rumi 1:24, 26; 28. Mungu hawezi kuachilia dhambi hiyo iwapo "usafi wa maisha kimwili" ni jambo geni kabisa kwao. Hakuna kuridhiana na kuwaingiza polepole katika Ukristo.

k.7-8. Wameitwa na Mungu kuishi maisha matakatifu, kwa hiyo anayekataa kuishi hivyo anamkataa Mungu si wanadamu. Pamoja na wito wake Mungu hutoa Roho Mtakatifu ili aishi ndani yao na kuwapa uwezo wa kushinda tamaa za mwili. Paulo alisema "anayewapa" dalili ya kuwa Roho yu tayari kuwasaidia mara wanaposikia kujaribiwa - ling. 1 Kor.6:19; 10:13

4:9-10 Wapendane:
Wao wenyewe walipendana 1:3; 3:6. wamejifunza neno hilo kwa Mungu kwa sababu Mungu **ni** pendo na kwa kuwa ni Mungu aliye pendo alifanya kazi maishani mwao ni sawa na kusema pendo lilifanya kazi maishani mwao, na kwa vyo vyote tunda la kazi hiyo litakuwa kupendana. Paulo alitaka wazidi sana, wamruhusu Mungu kuendelea kufanya kazi hiyo kubwa maishani mwao - 3:12.

Alama hizo mbili za utakatifu na upendo ni ushuhuda mkali mbele za watu na ni ishara thabiti ya ngubu ya Injuli na Mungu kufanya kazi ndani yao.

4: 11-12: Waishi kwa utaratibu na adabu:
Baadhi ya waamini walishikwa na hali ya msimuko kwa sababu ya kudhani kwamba Bwana Yesu yu karibu kabisa kurudi hata kuwaza kwamba kufanya kazi ni bure.

Paulo alitaka watulie, waendelee na kazi na shughuli za kawaida. Wawe na adabu, wajitegemee kwa riziki bila kuwalemea wengine ili wautoe ushuhda mzuri mbele za wasioamini, Injili isilaumiwe, na kuzuia farakano lisitokee kati yao.

4:13-5:11_ MATATIZO KUHUSU KURUDI KWA BWANA YESU:
Mara nyingi katika waraka huo habari ya Kurudi kwa Bwana Yesu imetajwa. Ni dhahiri kwamba Paulo alihubiri neon hilo na kulikaza, ila tuelewe kwamba neon kuu la kwanza lilikuwa Msalaba

4:13-18: Wakristo waliamini neno hilo kwa dhati, na kwa kulishikilia wamefikiri kwamba Yesu hatakawia.
Bila shaka hawakupata nafasi ya kumwuliza Paulo maswali yote kuhusu jambo hilo, na mpaka baadhi yao kufa hawakufikiri juu yao na mahali pao.
Swali lilizuka "itakuwaje kwao" "Je! watakosa kumwona Yesu atakaporudi?" "Je! watashiriki kwa ukamilifu katika Kurudi Kwake?"

k.13: Paulo aliwataja hao wafu kwa lugha ya "waliolala mauti", neno "kulala" ni neno zuri la kuieleza mauti ya Mkrista kwa sababu ya tumaini la ufufuo wafu

hao wataamka tena na kuishi tena, hivyo kufa kwao ni "kulala" tu. Mauti imebadilishwa na ushindi wa Bwana Yesu kuwa mlango wa kupitia ili tuingie kwenye uzima wa milele.

Hivyo wakristo wanapofiwa hawana haja kuhuzunika kupita kiasi kama wengine wasio na matumaini. Kule kutengana huleta huzuni ila tumaini la kuonana tena linapunguza uzito wa huzuni yetu na kutufanya kumshukuru Mungu na hata kwa upande wa imani kufurahi kwamba wapendwa wetu wamekwenda kwa Bwana.

k.14. Msingi wa tumaini letu ni katika Kufa na Kufufuka kwa Bwana Yesu. Si wazo tu wala bahati nzuri au fundisho fulani la filosofia, bali ni kwa sababu ya matendo makuu ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, hasa alipomfufua kutoka kwa wafu baada ya kifo chake cha ukombozi na upatanisho. Tunayo hakika kwa kuwa matendo hayo yalifanyika kweli ki- historia - Kristo alikufa - Kristo alifufuka.

k.15: Waliowahi kufa hawatakosa jambo lo lote, maana atakapokuja Yesu atawaleta pamoja naye. Tena Paulo alitumia lugha ya kuuonyesha ukweli na uhakika wake, "twaambiwa hayo kwa neno la Bwana". Licha ya kukosa kitu waliokufa katika Kristo watafufuliwa **kwanza,** ndipo waliosalia hai duniani watanyakuliwa.

k.16: Tutakutana na Bwana Yesu Mwenyewe hewani pamoja na kukutana na wakristo wenzetu na ushindi wa Bwana Yesu utakuwa dhahiri kwa watu wote. Bila shaka tunapenda kujua zaidi kuhusu hali za baadaye, ila jambo kuu la kwanza ni tutakuwa **pamoja na Bwana Yesu milele.**

k.18: Matumaini hayo ni msaada mkubwa kwa Mkristo akijua atayashinda maovu yote na upinzani wote ndipo mwishowe Yesu Kristo atakuwa Bwana wa Mabwana na Mfalme wa Wafalme. Tunapoishi au tukifo hatuwi nje ya uwezo wake wala mipango yake, kwa hiyo wajibu wetu ni kufarijianeni

5:1-3: Wakati wa Kuja Kwake:
Pamoja na wasiwasi juu ya waamini waliokufa inaonekana walitaka kujua zaidi juu ya wakati wa Yesu kurudi. Kama ambavyo tumekwisha kuona walimtazamia mapema sana na kumbe muda unaendelea. Yawezekana baadhi yao wamelikamata habari hiyo na kuitumia isiyo halali, wakianza kuleta mafundisho ambayo Paulo hakuyaleta.

Kwanza Paulo alisema kwamba hana haja ya kuandika mengi juu ya habari hiyo, aliyosema alipokaa nao yalitosha. Jambo moja kubwa ni kukumbuka kwamba Bwana Yesu atakuja "ghafula" na "ghafula" si sawa na "mara", ndiyo sababu wahitaji kuwa watu wanaomngojea Bwana wao, atarudi ghafula, siku ambapo hatazamiwi. Usalama wao hata na wetu ni katika kuwa tayari kila siku. Kama watu wangejua wangejiandaa, huenda bila upendo wa kweli, wasingejua wasingejiandaa.

5:4-11 : Kuwa watoto wa mchana:
Waamini hawafanani na wengine, hawana haja ya Siku ya Bwana kuwakuta katika hali ya kutokuwa tayari. Tumaini lao ni kushiriki kikamilifu katika Siku hiyo na haja yao ni kukesha, kuwa macho, kujiandaa ki- maisha na kuwa na kiasi. Hali zilizotakikana ni zile zilizokwisha kutajwa kuwa wanazo 1:3, imani, upendo na tumaini.

Shabaha ya Mungu alipowaokoa ilikuwa waupate wokovu wa Bwana Yesu. Paulo amekwisha kuwafundisha kwamba kwa Kifo cha Bwana Yesu wametolewa chini ya ghadhabu ya Mungu 1:11. Hawana sababu ya kuhofu, wakiwa hai wanashirikiana na Yesu aliye hai, wakifo bado watashirikiana naye - hawotengwi naye. Kwa hiyo waendelee kusaidiana na kujengana. Tukumbuke bado wangali wakiteswa na kuwa na dhiki kwa ajili ya imani yao.

5:12-22: KUWASIHI MAMBO MBALIMBALI:
k.12-13: Katika vifungu hivi Paulo aliwaelekeza juu ya viongozi wao. Paulo aliweka wazee katika makanisa mapya Mdo.14:23, hao wazee walikuwa na wajibu mkubwa wa kuwasimamia wakristo wenzao katika Bwana. Jambo moja lilikuwa kuwaonya. Pengine Paulo aliwaza kwamba wamepaswa kuwakemea wale walioacha kazi kwa kumngojea Bwana na wale ambao hawakutulia. Wasipojali viongozi wao na kupokea maonyo watafarakana, vikundi vitatokea. Huenda ndiyo sababu alisema "iweni na amani ninyi kwa ninyi".

k.14-15 Paulo aliona ni vema wasiokaa kwa utaratibu waonywe, hasa kuhusu kufanya kazi na kujitegemea kwa riziki. Labda hao walijiona kuwa wa kiroho kuliko wenzao. Pia wafuate kanuni ya Bwana Yesu ya kutokurudisha baya kwa baya.

k.16-20: Katika sehemu hiyo tunayo mashauri mafupi mafupi, hayo yatuonyesha alama za maisha ya Kikristo, furaha, maombi, shukrani, kuongozwa na Roho Mtakatifu, na kuuruhusu unabii.

Wapime kila jambo ndipo washike lililo jema na kukataa lililo baya. Ni shauri zuri sana kupima kwanza.

5:23-28. MWISHO:

Paulo alijua kwamba mwenendo huo aliowafundisha waamini wa Thesalonike hauwezekani nje ya msaada wa Mungu. Aliomba "Mungu awatakase kabisa" maisha yao yote yaguswe na Mungu. Alitaka wawe "kamili" na "bila lawama" mpaka Bwana Yesu atakaporudi, katika nafsi zao, roho zao, na miili yao. Wasiridhike bali wasonge mbele na kukua kiroho na kukamilika. Tena ni neno la Kurudi kwa Bwana linalotawala mawazo ya Paulo, alitaka wawe "safi kabisa" kwa siku ile kuu. Wameitwa na Mungu kwa maisha hayo, na kwa sababu ni Mungu aliyewaita ni Yeye pia atakayewawezesha watimize wito huo, na Mungu aweza kutegemewa kabisa.

k.25. Paulo alihitaji maombi yao. Aliwaombea wakristo wote katika makanisa yao akiwakumbuka mmoja mmoja. Ni mtu aliyeweka mipango yake yote mbele za Mungu ili afanye mapenzi yake. Na alitaka hao nao wawe watu wa maombi.

k.26-27: Alitaka wote washirikishwe waraka huo, yawezekana watajaribiwa wasiwashirikishe baadhi yao ambao Paulo amewaonya. Aliwaapisha, kwa hiyo aliwaza kwamba watawaacha wengine asiposema wote wasomewe. Alitaka wote wazipokee salaam zake.

"busu takatifu" hatujui ni busu ya aina gani, kwa mikono, au kwa uso, wanawake kwa wanawake, na wanaume kwa wanaume, au vipi; Ila ni "takatifu" halitaleta shida yo yote.

Ndipo aliufunga waraka kwa "neema" ambayo ni msingi na asili ya imani yao na chanzo cha Kanisa kuwepo kati yao.

Waraka wa Pili kwa Thesalonike

Paulo aliona vema kuwaandikia Wathesalonike tena, baada ya muda mfupi, kwa sababu ya mateso na dhiki kuendelea. Alihofu kwamba kwa jinsi hali hiyo inavyoendelea watakata tamaa.

Pia ilionekana kwamba wengine ama hawakumwelewa vizuri kuhusu Kurudi kwa Bwana, au walitaka kuingiza mafundisho ambayo hayakuwa ya kweli, wakidai kuwa wamepata barua kutoka kwa Paulo, 2:2,15; 3:17; na baadhi yao hawakufanya kazi wala kuishi kwa utaratibu, wakidhani Kristo yu mlangoni

Barua ya kwanza ilifaulu kuondoa mashaka juu yake, kwa sababu katika waraka wa pili hakujitetea kama alivyofanya katika waraka wa kwanza. Alikuwa bado angaliko Korintho alipouandika, na kabla ya kwenda Makedonia Mdo.20:1.

Katika huo wa pili twapata mafundisho juu ya "ukengeufu mkuu ambao utatokea kabla ya Kristo kurudi, na habari za "mtu wa kuasi".

Tunakumbushwa kwamba wakristo wachanga huhitaji msaada wa kujengwa ki-imani na kupewa uongozi kuhusu mwenendo. Kwa kweli walikuwa wakiendelea vizuri sana katika imani na maisha yao, wakiwa vielelezo vema, hata hivyo walihitaji msaada katika mambo kadha na hasa kutiwa moyo kukabili mateso yaliyoendelea kuwapata

Tunaona Kanisa lina mamlaka juu ya watoto wake kuwaonya na kuwotenga 3:14,15, tena lina mapokeo yenye madaraka ya ki-mitume. Pia tunayo maombi ya Paulo 1:11,2:16-17, 3:16.

1:1-2 Salaam:: Zinafanana na za waraka wa kwanza isipokuwa kwa nyongezo mfupi ya "zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Bwana Yesu Kristo". Bwana Yesu amefungana na Mungu Baba kuwa asili ya neema na amani, ushuhuda wa Uungu mmoja.

1:3-12: KUWATIA MOYO KATIKA MATESO NA DHIKI:

1:3-4: Shukrani na sifa:
Kama alivyofanya katika waraka wa kwanza Paulo alimshukuru Mungu kwa hali yao njema ya imani na upendo, jinsi walivyozidi kuamini na kupendana iwapo dhiki zao ziliendelea. Yawezekana walijitetea kwamba hawakustahili sifa walizopewa katika barua ya kwanza, lakini Paulo amesisitiza ni vema na ni

wajibu kuwasifia na kumshukuru Mungu - "imetupasa". Aliona ni jibu la Mungu kwa maombi yake - ling. 1 Thes.3:12.

k.4. Paulo alisema habari zao katika makanisa mengine akiona fahari juu yao na bila shaka shabaha yake ilikuwa kuwatia moyo ili hao nao wawe na imani na upendo kama waamini wa Thesalonike; pia wawe tayari kupambana na dhiki na mateso katika kumfuata Kristo.

1: 5-10: Hukumu ya Mungu:
Paulo aliendelea kwa kusema juu ya hukumu ya Mungu na uhusiano wake na dhiki na mateso yao. Alisema dhiki zao ni ishara ya hukumu iliyo haki ya Mungu - wazo la ajabu! kwa sababu dhiki zao si za haki! Maana yake ni kwamba Mungu hutumia dhiki kama njia ya kuwakamilisha "ili mwahesabiwe (si mwafanyiwe) kuwa mmestahili kuingia ufalme wa Mungu". Si njia ya kuwafanyia au kuwapatia ufalme, bali ni njia ya **kuonyesha** wamestahili. Ni kwa neema ya Mungu wameuingia na ni kwa neema wanastahimili kwa ajili yake.

Ndipo Paulo alielezea hukumu ya Mungu iliyo haki kwa wale waliokuwa wakiwotesa waamini. Hukumu yao itatokea mbeleni wakati Bwana Yesu atakapofunuliwa, yaoni atakapokuja tena. Hao waamini wataachwa kuteswa; watapata raha na pumziko. Wotesi watapata mateso ya adhabu ya Mungu. Tabia mojawapo ya Mungu ni haki, na kuadhibu dhambi, katika haki hiyo ni "kuwalipa".

1:7-9: Bwana Yesus atatokea katika uwezo mwingi pamoja na jeshi la malaika, tena katika “mwali wa moto”. Atakuja kwa utukufu na vitisho vikali kwa wasiompenda, wale waliomkataa kumjua na kumtii, wale ambao Injuli ilipohubiriwa hawakumwamini. Siku ile atawalipiza Kisasi, watapata hasara mkubwa sana, lugha aliyotumia Paulo inatisha sana “maangazizi ya milele, yaani hasara ya milele siyo ya muda. Hasa hasara itakuwa katika kutengwa na Bwana na baraka zake zote - neema zote ambazo tumepewa katika kuwa viumbe vyake Math.5:45.

k.10: Utukufu wa Bwana umekazwa, na waliomwamini watamrudishia utukufu wake, mfano wa kioo jinsi kinavyomrudishia mtu sura yake: 1 Yoh.3:2. Waamini wenyewe watashangazwa mno kwa vile utukufu wake unavyozidi sana mawazo yao “tutamstaajabia”.

Hilo ni tukio la baadaye, atakaporudi Bwana Yesu, lakini chanzo chake kilikuwa katika Paulo na wenzake kuja kwao na kuwahubiri na wao kuitika na kumwamini Kristo.

Kwa hiyo yatupasa kuthamini sana kazi ya kuihubiri Injili na kukumbuka matokeo ni makubwa, mema kwao wanaoipokea na hasara ya milele kwao wanaoikataa.

1:11-12 :Maombi ya Paulo kwa ajili yao:
Paulo alikuwa mtu wa maombi, kila siku aliwakumbuka wakristo katika makanisa mbalimbali. Si kwamba alikuwa na nafasi ya kuomba ila aliweka nafasi kati ya shughuli nyingi. Tukitazama safari zake nyingi na ugumu wa maisha yake tunashangaa jinsi alivyopata nafasi ya kuomba. Ni siri ya hao waamini kusimama imara; waliombewa na walifundishwa kuomba kama msingi wa maisha ya Kikristo.

Aliwaombea nini? Kwanza, aliomba Mungu awahesabu wamestahili kuitwa kwao, yaoni Mungu anapowatazama aridhike kwamba aliwaita kwa njia ya Injili. Picha ni ya mtu anayeitwa na mwingine kufanya kazi fulani, matazamio ya yule aliyemwita yatimizwe, aliyeitwa afanye ile kazi vizuri. Hao wakristo wameitwa na Mungu kufanya mapenzi yake. Kusudi lengo hilo litimizwe Paulo alimwomba Mungu awape msaada wa kufanya mema, kila jema awawezeshe kulifanya, na awape nguvu kufanya kila kazi ya imani yao, kwa jumla waendeshwe na uwezo wa Mungu.

Shabaha ni kumtukuza Bwana Yesu, watakapoishi maisha yaliyotofautiana na kawaida ya wenzao, yasiyo na maelezo nje ya nguvu ya Mungu, ndipo watu watatambua ni Mungu anayefanya kazi ndani yao na Yesu atatukuzwa.

"kwa neema ya Mungu wetu na ya Bwana Yesu Kristo" Paulo alifahamu hakika kwamba maisha ya namna inayompendeza Mungu hayatokani na lolote ndani yetu, ni kwa kuruhusu neema ya Mungu ifanye kazi ndani yetu. Twaona kwamba Paulo alimweka Yesu karibu sana na Mungu Baba, dalili ya Uungu wake na umoja wao na kazi yao kuwa moja.

2:1-17: KUWATIA NURU KWA MAFUNDISHO

2: 1 - 2: Siku ya Bwana haijaja bado:
Wakristo wa Thesalonike walitatanishwa kuhusu Siku ya Bwana kwamba imekwisha kuwapo. Habari hii ilitoka wapi? K.2: Paulo ametaja njia mbalimbali, huenda mojawapo imesababisha jambo hilo. i."kwa roho" yawezekana mmoja wao amedai kuwa yeye au Paulo amefunuliwa na Roho Mtakatifui; ii."kwa

neno" yaoni mtu fulani amesema Paulo ametamka neno hilo katika mahubiri yakei; iii. "kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu" yaoni mmoja amesema kwamba ameipata barua akifikiri imetoka kwa Paulo.

Paulo hakujua kwa uhakika chanzo chake. Aliwasihi wasifadhaishwe wala kushtushwa. Iliyopo ni kwamba Siku ya Bwana haijaja bado. Tumekwisha kuona kwamba Paulo alikaza sana Kurudi kwa Bwana, kwa hiyo isingalikuwa vigumu watu kuwaza mambo mbalimbali juu yake.

2: 3 - 12: Ukengeufu mkubwa utatokea:
Katika sehemu hiyo sisi tunapata shida katika kufahamu mengine kwa sababu Paulo alikuwa amewaambia mambo fulani ambayo sisi hatuyajui: taz. k.5.
Katika habari ya Kuja kwa Bwana tuna haja ya kuwa macho ili tusidanganyike.
Bwana Yesu alituonya vivyo hivyo - Math.24:4,5,11.

Paulo aliwafundisha kwamba kabla ya Bwana Yesu kurudi ukengeufu mkubwa utatokea, yaoni wengi watamwasi Bwana, enzi za uovu zitampinga Mungu kwa nguvu kwa sababu ya kutambua mwisho wao unakaribia Math.24:9-12, Tim.4:1-3; 2 Tim.3:1-9; 4:3ku.

Ufunuo 12:7-12. Picha ni kwamba mwisho utakapokaribia Shetani atatupa yote aliyo nayo katika jaribio lake la mwisho la kumshinda Mungu na Bwana Yesu.

Katika uasi huo mtu wa kuasi atafunuliwa (tukumbuke ya kuwa hali moja ya dhambi ni uasi 1 Yoh.3:4) Katika historia yote ya wanadamu wamekuwepo watu ambao wamefanya kazi ya Shetani, wapinga Kristo wengi walikuwa wameisha kutokea, hata karne ya kwanza - 1 Yoh.2:18. Kwa hiyo inatazamiwa watatokea waovu sana mpaka atakcapotokea mmoja atakayewazidi wote waliomtangulia, naye atatokea karibu na wakati atakapokuja Bwana Yesu. Kwa hiyo hatatokea mpaka mwisho umekaribia sana. Si Shetani 2:9; ila ni chombo chake na kwa nia amefanana naye.

k.4: Ameitwa "mwana wa uharibifu" maana yake atakwenda kwenye uharibifu. Tabia yake ni kuharibu na kupinga na hapa twaona uhusiano wake na Shetani, kwa sababu maana ya neon "shetani" kwa Kiebrania ni "mpinzani".

Tabia nyingine ya mtu wa kuasi ni "kujiinua" 2 Kor.12:7; anajiinua kwa kiasi kikubwa akitaka kuwa juu ya Mungu na chote kinachoabudiwa. Ataketi mahali patakatifu, maana yake ni kuchukua nafasi ya Mungu Mwenyewe – akidai kuwa ndiye Mungu.

k.5. Paulo alirudia habari alizowaambia alipokuwa pamoja nao. k.6. Walielewa "lizuialo", ila sisi hatujui, maana hakutoboa zaidi ili sisi tuelewe. Wazo moja la maana kuhusu "lizuialo" ni kuliwaza kuwa "msingi wa sheria na madaraka" kwa sababu kwa njia ya sheria za nchi n.k. ubaya huzuiliwi na kutawaliwa. Wengine wameliwaza kuwa malaika, au Roho Mtakatifu.

Mtu wa kuasi atafunuliwa kwa “wakati wake”, lugha hiyo inatuonyesha jinsi Mungu alivyo na madaraka juu ya hayo yote. Hata sasa uasi upo katika ulimwengu, ila bado haujafikia upeo wake mpaka “lizuialo” au “azuiaye” ameondolewa - 1 Yoh.2:18.

k.8: Mara baada ya kutaja kufunuliwa kwake Paulo alitaja kuangamizwa kwake - Mungu anatawala yote mawili. Kumbe! Bwana Yesu atammaliza kwa urahisi sana, iwapo ni wa kutisha kuliko wote waliomtangulia. Yatosha Bwana Yesu atokee tu, utukufu wake utamaliza nguvu zake zote, ataishiwa na kuyeyuka mbele zake. (neno "kumwangamiza" kwa Kiyunani halina maana ya kumfuta kabisa, ila ni kumfanya asiweze lo lote).

k.9: Huyo "mtu wa kuasi" hufanana na Kristo katika mambo kadha. Ana "kuja kwake" kama Bwana Yesu. tena hufanya kazi katika nguvu za Shetani, na Bwana Yesu alifanya katika nguvu za Mungu. Atafanya maajabu na miujiza kama Yesu alivyofanya. Ila atatumia hilo na udanganyifu, tabia yake ni udhalimu. Ni mdhalimu wa hali ya juu kwa sababu ndiye aliyewaongoza "wanaopotea". Paulo aliona hatua hizo zilikuwa zikitokea wakati wake.
2:10b-12: Wafuasi wa mtu wa kuasi: Kwa nini watadanganyiwa?" - jibu la Maandiko ni "hawakukubali kuipenda ile kweli", hawakukaribisha kweli kama rafiki wa kuwasaidia (ling. 1 Thes.2:13), kweli ni Injili, na kama wangeipokea wangeokolewa.

k.11: kifungu hiki chashangaza kwa sababu upotevu wao umeelezwa kuwa umetokana na Mungu, iwapo hapo juu tumesoma ni Shetani aliyewadanganya (Taz. 1 Waf.22:23; 1Nya. 21:1; 2 Sam.24:1). Katika mtindo wa kuwaza kwao Waebrania waliwaza kwamba hakuna kitu kilicho nje ya uwezo na madaraka ya Mungu, hata nguvu za uovu hazina asili nje ya Mungu; maana yake bila Mungu kuziachilia nafasi haziwezi kuwepo au kufanya kazi: Taz.Zab.76:10.

Mungu hutekeleza makusudi yake akiyatumia maovu ya wanadamu na Shetani. Mara kwa mara Mungu hutumia matokeo mabaya ya dhambi kuwa sehemu ya adhabu yake kwa dhambi iliyotendewa Rumi 1:24, 26, 28. Wala si matokeo yake tu ila ni mkono wa Mungu juu ya njia hiyo ya kumpatia mwenye kutenda dhambi adhabu yake.

Kwa hiyo Mungu ndiye anahusika katika hao watu kuuamini uongo, ila twapaswa kuona ya kuwa ni baada ya wao wenyewe kuikataa Injili. Katika sentenso hiyo neno "Mungu" limetawala, kusudi mkazo uwe kwamba matokeo hayo si bahati wala sheria ya kawaida tu, bali hasa ni tendo la Mungu. "nguvu ya kupotea" lugha hiyo inatoa picha ya mtu anayeuendeleza si amenaswa tu. Ni wazo zito la kuona kwamba wanaokataa wema, mwisho wao ni kuuendeleza uovu.

k.12: Kuuamini uongo sio mwisho wa mambo, baada ya hapo ni hukumu ya Mungu. Ajabu ni kwamba baada ya kuikataa kweli na baada ya kuuamini uongo, watu walijifurahisha katika maovu yao. Badala ya kujifurahisha katika Mungu waliifurahia dhambi, na hivyo wameupotosha kabisa shabaha ya Mungu katika kuwaumba.

2:13 - 15: Shukrani na kuwatia moyo:
Daima alipowakumbuka Paulo alisikia kumshukuru Mungu kwa ajili yao. Msingi wa shukrani zake ni katika Mungu Mwenyewe kuwachagua tangu mwanzo waupate wokovu kwa sababu ya upendo wake. Kweli Paulo alikuja kwao na kuhubiri, ila alifanya hivyo kwa sababu ya kuitwa na kutumwa na Mungu. Chanzo kabisa ni katika Mungu kumtuma Kristo ili afe kwa ukombozi wao na wetu.Yoh.3:16.

Neno la kuwashukuru ni kwamba walipohubiriwa Injili walisikia wito wa Mungu kumwamini Kristo, wakaitika.

Wito wao ni kutakaswa dhambi zao na kuishi maisha matakatifu jinsi Paulo alivyofundisha. Mwisho wa imani yao ni kushirikishwa utukufu wa Bwana Yesu. Katika sehemu hiyo, Mungu, Bwana Yesu, na Roho wametajwa pamoja, ushuhuda wa Utatu na Umoja wao.

Wajibu wao ni kusimama imara, wasitishwe na dhiki zao, wala kwa mateso yao, vilevile wasikubali kuondoshwa katika mafundisho ya kweli waliyopewa Paulo alipokuwa pamoja nao na kwa nyaraka alizowaandikia.

2: 16 - 17: Maombi kwa ajili yao:
Kila wakati katikati ya kuwaandikia Paulo aligeukia kuwaombea Tunaona tena kwamba alimweka Bwana Yesu sawa na Mungu akitumia lugha ya "mmoja", iwapo ametaja "wawili". aliyetupenda", "akatupa faraja ya milele", na "tumaini jema" -alipoomba alikumbuka hali yao ya upendo, na vipawa vyao vyema vya faraja na tumaini; na Mungu wa mambo hayo hakosi kuleta msaada wanaohitaji - faraja kwa ajili ya dhiki zao, na nguvu ya kusimama imara kwa sababu ya mateso yao, ili waendelee kutenda mema bila kukata tamaa.

3:1-15: KUWAWEZESHA KUISHI MAISHA YA KIKRISTO:

3:1-2 : Paulo alitaka wamwombee:
Siri kuu ya maendeleo ya Injili na makanisa kupandwa na kuimarishwa ilikuwa maombi. Paulo na wenzake walikuwa watu wa kuomba daima. Nguvu yao ya kuendelea kuihubiri Injili katika vipingamizi vingi na taabu nyingi iltokana na maombi. Walifundisha waamini wapya kuomba.

Kwa hiyo alipokaribia kuumaliza waraka huo wa pili neno hilo la kuombeeni liliwekwa - ling. na 1 Thes.5:25. Yeye alihitaji maombi yao kama wao walivyohitaji maombi ya Paulo na wenzake.

Paulo alifahamu kabisa kwamba yeye na wenzake ni watu wanaopasua njia mpya, njia kwa Injili kufikia watu wengi katika nchi mbalimbali - mfano wa watu wanaofyeka pori kubwa ili kufungua njia. Ni Neno la Mungu linalofanya kazi maishani mwa watu, linakwenda mbio kuyatimiza mapenzi ya Mungu kuuleta wokovu wa Bwana Yesu kwa watu.

Shetani husimama kama mpinzani mkuu akitafuta kuwazuia watumishi wa Neno. Aweza kutumia watu wabaya kuleta fitina na kuinuka juu ya wahubiri, aweza kutumia hali ngumu za usafiri, maradhi n.k. mradi Neno lisiendelee.
Kwa hiyo Paulo aliwasihi waombe ili Neno liendelee.

3: 3-5: Uaminifu wa Mungu:
Tumaini lao li wapi? Ni katika uaminifu wa Mungu, maana kazi hiyo yote ni ya Mungu. Mungu ndiye asili ya wokovu ni Yeye aliyemtuma Kristo, ni Yeye aliyewatuma wahubiri, na ni Yeye atakayewahifadhi katika imani yao. Wakidumu waaminifu kwa maagizo na mafundisho waliyopewa watashinda na watazidi kuuonja upendo wa Mungu na kukaa katika subira ya Kristo aliyevumilia mateso makali ya msalabani kwa ajili yao. Mungu anapoanza kazi njema ataitekeleza hadi ifikie lengo lake, Fil:1:6.

3: 6 - 9: Neno la Mungu na kielelezo cha Paulo:
Kufuatana na mkazo juu ya Kurudi kwa Bwana Yesu baadhi ya wakristo, huenda ni wachaohe tu, waliamua kuacha kazi na kumngojea hali wakidhani atatokea mara. Pengine walilemea wenzao kwa riziki. Pia walisemasema wenzao walioendelea kama kawaida.
Paulo alitoa maagizo yaliyo wazi ili awasaidie. Kwanza wapaswa wajitenge na hao ambao wameacha kazi. Budi waishi kwa utaratibu. Hata Paulo na wenzake walipokuwa pamoja nao wakisongwa na kazi ya kuhubiri Injili, walifanya kazi kwa masumbufu makubwa ili wajipatie riziki zao bila kulemea

watu. si kwa sababu hawakuwa na haki ya kutunzwa ila walitaka kutoa kielelezo chema. Katika hekima waliyopewa na Mungu walitambua kwamba baadaye watu watadai kutunzwa wasiyo na haki hiyo.

3: 10-15:Kuwaonya wasioenenda kwa utaratibu na wasioshika maagizo:

Shida moja ya hao watu ambao walikuwa wameacha kufanya kazi ilikuwa vigumu kwao kutulia bila kujiingiza katika mambo ya wenzao walioendelea na kazi. Kwa kukosa shughuli zao walijishughulisha na mambo ya wengine.

k.12 Paulo alitilia mkazo maagizo yake na kuwaonya kwa uzito, lugha aliyoitumia “katika Bwana Yesu Kristo”.

Ila aliandika kwa uangalifu sana akisema “hao” hakusema “ninyi”. Mashauri yake yalikuwa “watulie” “wafanye kazi” na “wale chakula chao wenyewe”

Aliwaita wote “ndugu”, waraka wake ni kwa wote, iwapo imembidi ataja "hao" wasioenenda kwa utaratibu; waraka si kwao tu, bali ni kwa wote. Wote waendelee kufanya mema, wasichoke, wasikate tamaa.

k:14,15. Itakuwaje kama mtu hatakubali maonyo ya Paulo. Waamini wenzake wa pale wafanyeje? Wajitenge naye, wasizungumze naye, wasijadiliane naye, kusudi katika "upweke" atakayeusikia ajirudi na kujirekebisha. Waendelee kumwaza kuwa ndugu yao katika Kristo na kumwonya kwa upendo.

3:16-18: MWISHO:

Paulo aliufunga waraka katika hali ya baraka. Aliwatakia amani ya Bwana, na Uwepo wake maishani mwao. Bwana akiwemo maishani mwao amani itakuwemo Yoh.14:27. Twaweza kusema Amani **NI** Kuwepo kwa Bwana - ni kipawa chake. Paulo aliomba **wote** wawe naye na nayo.

k.17: Kwa desturi Paulo alitumia mkalamani, halafu mwishoni mwa barua alichukua kalamu mkononi mwake mwenyewe - Ling. 1 Kor.16:21; Ko1.4:18. "alama" ni kitambulisho kwa njia ya mwandiko wake kwa kuithibitishia barua kuwa yake - ling. 2 Th.2:2, na "barua iliyodhaniwa kuwa yetu". Inaonekana kwa sababu ya barua hiyo aliona vema kuwapa alama ya kuwasaidia kuzitambua barua zake.
k.18: Alimaliza kwa "neema" kama alivyofanya katika waraka wa kwanza, akiongeza neno moja "nyote". Ni ishara ya upendo wake na upole wake hata kwa wasioenenda kwa utaratibu, akiwaingiza katika salaam za kuagana nao.
Mzigo wake ni kwa wote, wala si kwa wale wazuri tu wasio na matatizo.

MASWALI

1. *Tumeona hali na tabia za Paulo na wenzake katika kuieneza Injili na kupanda makanisa. Je! hali na tabia hizo bado zinahitajika kama Injili itaenezwa kwa wakati wetu?*
   Zungumza jinsi makanisa yaweza kupandwa mahali papya?
2. *Kuhusu fundisho la Kurudi kwa Bwana. Je! siku hizi fundisho hilo linapewa umuhimu wa kutosha kama Paulo na wenzake walivyolipa? Fundisho hilo ni msaada gani kwa Mkristo na maisha yake ya kila siku?*
3. *Ipo hatari gani kwa wanaolikaza sana?*

WARAKA WA KWANZA KWA TIMOTHEO

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Sababu za kuitwa Nyaraka za Kiuchungaji.
b) Shabaha.
c) Mwandishi.
d) Tarehe ya kuandikwa.

UFAFANUZI

1:1-20 UHUSIANO KATI YA PAULO NA TIMOTHEO

1: 1- 2 Salaam za Paulo
3-11 Tofauti kubwa kati ya Injili na mafundisho yaliyopotoka
12-17 Kazi ya Injili katika maisha ya Paulo
18-20 Agizo la Paulo kwa Timotheo

2:1 - 4:16 IBADA NA TARATIBU KATIKA KANISA

2: 1- 8 Umuhimu wa sala za watu
9-15 Mahali pa wanawake katika ibada za Kikristo
3: 1-13 Sifa na tabia zilizotakiwa katika watumishi wa Kanisa
14-16 Kanisa
4: 1- 5 Paulo alikemea mafundisho ya uongo
6-16 Kupambana na mafundisho ya uongo

5:1 - 6:2 MARUDI NA WAJIBU

5: 1- 2 Marudi kwa vikundi na marika mbalimbali
3-16 Wajane
17-20 Wazee/Waangalizi
21-25 Timotheo na mwenendo wake
6: 1- 2 Watumwa

6:3 – 21 MASHAURI MBALIMBALI

6: 3- 5 Waalimu wa uongo
6-10 Hatari za mali
11-16 Mausia kwa Timotheo
17-19 Mashauri kwa matajiri
20-21 Neno la mwisho la Paulo kwa Timotheo

UTANGULIZI

(a) Sababu za Kuitwa Nyaraka za Kiuchungaji

Tangu mwanzo Nyaraka hizo tatu zimewekwa pamoja na kuitwa Nyaraka za Kiuchungaji kwa sababu ziliandikwa kwa watu binafsi, na nyingine zote, isipokuwa Waraka kwa Filemoni, ziliandikwa kwa makanisa mbalimbali. Tangu mwaka BK 1703 zimepata kuitwa Nyaraka za Kiuchungaji kufuatana na mambo yaliyomo. Katika nyaraka hizo Paulo ameshauri mengi kuhusu uchungaji wa watu wa Mungu na wajibu wa viongozi kuwatunza vizuri na kuwafundisha jinsi ilivyowapasa kuishi. Aliwashauri waepukane na kuyakataa mafundisho yaliyopotoka ambayo licha ya kuwajenga Wakristo yaliwapotosha. Aliwashauri Timotheo na Tito kuweka viongozi wa kufaa katika makanisa akizitaja sifa na tabia zilizotakikana kwa wale wa kuchaguliwa kushika madaraka katika sharika zao.

(b) Shabaha

Paulo alitaja shabaha yake katika 1 Tim.3:l5. Iwapo ni barua kwa watu binafsi, ni wazi kwamba zinagusa mambo yahusuyo Wakristo katika sharika zao. Katika Waraka wa Pili kwa Timotheo, Paulo aliandika kama mtu aliyetazamia kwamba karibuni hivi atauawa, akionyesha mzigo mkubwa wa kutoa mwongozo kwa wale watakaomshikia. Mwongozo huo utawasaidia Timotheo na Tito kusema kwa mamlaka juu ya mipango ya Kanisa. Hata Paulo mara kwa mara alitumia maneno “nakuagiza....” (1 Tim.1:18; 4:11; 5:7,21; 6:13).

(c) Mwandishi

Tangu mwanzo nyaraka hizo zilihesabiwa kuwa zimeandikwa na Paulo. Zinataja mambo ya kibinafsi ya Paulo, Timotheo, na Tito. Kwa mfano, karibuni hivi Paulo alikuwa amemwacha Timotheo pale Efeso (1 Tim.1:3) na Tito pale Krete (Tito 1:5). Paulo alijishuhudia maisha yake ya zamani pia alisema yeye ni wa kwanza wa wenye dhambi (1 Tim. 1:13-15). Ni vigumu kufikiri kwamba mtu mwingine angalithubutu kusema hivyo.

Baadhi ya watalaamu hawakubali kwamba Paulo aliziandika nyaraka hizo tatu. Sababu yao kubwa ni lugha, maana zina maneno mengi ambayo Paulo hakuyatumia katika nyaraka zake zingine. Jambo lingine ni kuona nafasi kwa Paulo kuwa Efeso na Krete na Nikapoli n.k. katika safari zilizotajwa katika Matendo ya Mitume. Ila ikikubalika kwamba Paulo aliruhusiwa baada ya kufungwa pale Rumi (Mdo.28) akasafiri tena kabla ya kukamatwa tena, basi tatizo hilo limetatuliwa.
Wazo la kufikiri kwamba Paulo alifunguliwa limejengwa juu ya tumaini lake alilolitaja katika Nyaraka za Wakolosai, Wafilipi, na Filemoni, Nyaraka ambazo wengi hukubali kwamba ziliandikwa alipokuwa kifungoni huko Rumi.(Taz. Flp 1:18-19; 24-26; 2:24) Katika Filemoni k.22 alitarajia kuja kumwona Filemoni,

akaomba amwekee mahali tayari. Kwa hiyo aliona uwezekano wa kufunguliwa upo, pia, atakapofunguliwa ataelekea sehemu za mashariki. (Zamani aliwaza kwenda magharibi mpaka Spania (Rum.15:23-29).

Baadhi ya wataalamu hufikiri kwamba picha tuliyo nayo ya makanisa katika Nyaraka hizo ni ya Kanisa ambalo ni la muda mrefu, ambalo limeendelea na kuwa na mipango kamili na sababu za kufikiri hivyo ni katika kuona dalili za Ukiri wa Imani na Taratibu za Uongozi n.k.

Twajua kwamba tangu kutokea kwa sharika za Kikristo baada ya uinjilisti uliofanyika na wale wa kwanza waliosafiri huko na huko na kuhubiri Injili, Paulo na wenzake waliwaweka wazee katika makanisa (Mdo.14:23) na makanisa hayo yalipewa "mapokeo" ya kushika, ambayo yalikuwa chanzo cha mipango na taratibu katika Kanisa (Mdo.16:4; 2 Thes.2:15; 1 Kor.11:2; 14:33). Kwa hiyo si ajabu kwamba Paulo alizidi kutoa ushauri na maagizo kwa wale watumishi kama Timotheo na Tito hali akikaribia kufa na wakati ulisogea wa wao kushika madaraka baada yake.

Twaweza kujumlisha hayo yote kwa kusema Nyaraka hizo tatu zilitoka kwa Paulo. Yawezekana alitumia mkalimani, au pengine aliziandika mwenyewe. Sababu za kukaza kwamba barua hizo tatu ni zake kwa asili ni kwa sababu ya ushuhuda uliomo unaokubaliana na wakati wake, na kutaja mengi ya kibinafsi.

(d) Tarehe ya Kuandikwa kwa Waraka wa Kwanza

Ni karibu mwisho wa maisha ya Paulo na baada ya kufungwa Rumi. Ni kati ya BK. 64 na BK.66. Alikuwa Makedonia (1 Tim.1:3) akitarajia kuja kumwona Timotheo pale Efeso karibuni hivi.

UFAFANUZI

1:1-20 UHUSIANO KATI YA PAULO NA TIMOTHEO

1:1-2 Salaam za Paulo

Paulo alianza kwa kumkumbusha Timotheo kwamba alimwandikia katika hali ya kuwa Mtume aliye chini ya amri ya Mungu, ili iwe dhahiri kwamba ujumbe wake ndani ya barua hiyo, iwapo ni kwa mtu binafsi, una mamlaka ya Mungu. Yawezekana huko Efeso baadhi ya waumini hawakumpokea Paulo kama Mtume halisi. Iwapo barua ni kwa Timotheo mwenyewe ina mengi yaliyowahusu jamii ya Wakristo, hivyo ina hali ya kuwa barua ya kibinafsi pamoja na kuwa barua rasmi kwa Kanisa.

Paulo alitilia mkazo cheo chake cha kuwa Mtume kwa kuongeza maneno “kwa amri ya Mungu”. Hakuwa Mtume kwa kutaka mwenyewe bali aliwekwa na Mungu Mwenyewe. Wakati wote alijua kwamba yeye yuko chini ya amri na uongozi wa Mungu.

k.1 “Amri ya Mungu Mwokozi wetu na Kristo Yesu, taraja letu”, si kawaida ya Paulo kutumia maneno hayo. Pengine ametumia lugha hiyo kwa sababu katika Dola ya Kirumi ziko dalili za kuanza kwa desturi ya kumwadhimisha Kaisari, mkuu wa Dola na baadaye walifikia hatua ya kumwaza kuwa mwokozi na kumwabudu kama ni mungu. Kwa lugha hiyo alisisitiza kwamba yuko mmoja tu aliye Mkuu, mwenye Ufalme, Mtawala wa yote. Mungu ndiye Mwokozi na Yesu ni mtekelezaji wa wokovu huo ambaye Mungu amemweka kuwa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.

Mungu aliyemweka Paulo ni Mungu aliye asili ya wokovu. Ni Yeye aliyemtuma Yesu Kristo ili atuokoe. Kristo ni taraja letu la uhakika. Ni Yeye Yesu aliyeshinda, kwa hiyo ni Yeye wa kuaminiwa kwa sababu amewekwa na Mungu. Hivyo Baba na Mwana ni asili ya utume wa Paulo.

k.2 “kwa Timotheo, mwanangu hasa katika imani”. Timotheo alilelewa katika imani yake na Paulo. Paulo alimtunza kiroho, alimshauri na kumwongoza, alimchukua na kumwingiza katika kazi ya kuhubiri Injili (Mdo.16:1-3). Walipendana sana na kushirikiana pamoja katika kazi ya Bwana, hasa katika safari za uinjilisti.Mara kwa mara Paulo alimtuma kwa makanisa kwa kusudi la kuyatengeneza shida zao. Paulo alimsifu sana. (Flp.2:20-22). Inaonekana kwamba Timotheo hakuwa mjasiri, ila daima alidumu mwaminifu, na Paulo alimwamini. Bila shaka barua hiyo ilikuwa na shabaha ya kumfariji na kumtia nguvu na moyo wa kukabili matatizo yaliyomo katika Kanisa la Efeso. Kanisa la Efeso lilipaswa kumtambua kuwa mwana wa kweli wa Paulo mwenye mamlaka yake.

k.2b Paulo alimtakia baraka za neema, rehema, na amani zitokazo kwa Mungu. Paulo alizipenda sana salaam hizo, (ila si wakati wote alitaja rehema) na alizitumia alipowaandikia waumini wa makanisa pamoja na watu binafsi. Hasa hizo ni msingi wa Imani ya Kikristo.

Timotheo alifaa sana huduma ya Kikristo, maana alifahamu kikamilifu Injili ya kweli pamoja na kujua “mapokeo” yaani masharti na taratibu ambazo Paulo aliwaongoza waumini kuzishika. Wakati wote Paulo aliuadhimisha Utume wake akiistaajabia neema ya Mungu katika kumwita. Vivyo hivyo yawapasa watumishi wote ambao Mungu amewaita kutumika Kanisani waone fahari kubwa juu ya wito wao na utumishi wao.

1:3-11 Tofauti kubwa kati ya Injili na mafundisho yaliyopotoka

Katika sehemu hiyo twajifunza sababu kubwa ya Paulo kumwacha Timotheo pale Efeso, wakati ambapo yeye alikuwa akienda Makedonia. Kwa kuweka wazi katika maandishi sababu yake wote walifahamu kwa nini Timotheo ameachwa pale Efeso. Bila shaka, kwa njia hiyo, Timotheo alisaidiwa kuwakabili wale wa Efeso ambao walikuwa wakifundisha elimu iliyo kinyume cha Injili. Efeso ulikuwa mji mkubwa na wa maana sana, kwa hiyo, Kanisa la pale lazima liwe na nguvu katika kuishikilia kweli.

Inaonekana hao waalimu wa elimu nyingine ni wa palepale, huenda baadhi yao walikuwa wazee katika sharika za pale. Hata Paulo alipoagana na wazee (Mdo.20:17-35) aliwaonya kwamba mbwa mwitu wakali wataingia katika kundi na katika wao wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu. Katika k.7 Paulo alisema “wapenda kuwa waalimu wa sheria” na twajua kwamba wajibu mmoja wa wazee ulikuwa kufundisha (5:17, 3:2). Tayari Paulo alikuwa amewahukumu wawili na kuwatenga (1:19-20). Pia katika Waraka alionyesha mzigo juu ya wazee na kusema juu ya marudi yao, na tabia za wale wanaowekwa kuwa wazee.

Kutokana na jinsi alivyoandika Paulo katika sehemu hiyo twapata kufahamu namna ya mafundisho yaliyowapotosha watu. Watu walipenda kuzishughulikia hadithi na nasaba na kuchochea majadiliano mengi, wakifurahi kuamsha maswali mengi yasiyo na maana wala faida katika kujenga roho za watu na imani zao. Kwa mtindo huu watu walipoteza muda wao katika mambo ya ubatili badala ya kujifunza na kujitia chini ya mapenzi ya Mungu na kumtii.

Yalimpasa Timotheo ajiingize kwa nguvu na kuwakataza wale waalimu ili wakristo warudishwe katika hali njema.

k.5 Shabaha ya mafundisho ya Kikristo ni kugusa maisha yetu ili tujirekebishe na kufanya mapenzi ya Mungu. Hatari ipo wakati wote na hasa kwa upande wa theologia kwa watu kujadili maneno badala ya kutenda yanayowapasa.
Twajibika kujua yaliyomo katika Imani yetu ya Kikristo, na ni vema tuzidi kujifunza Neno la Mungu katika hali ya kufuata lengo ambalo ni upendo, upendo unaotoka katika moyo safi na dhamiri njema na imani ya kweli.

Paulo alimwagiza Timotheo “uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine”. Neno hilo ni la maana kwa siku zetu ambazo ni siku za wengi kuridhiana na mafundisho ya uongo. Hewa iliyopo ni hewa ya kuruhusu kila mtu kuamini atakavyo, kana kwamba hakuna kweli ambayo ni kweli hasa. Ni hatari sana. k.7ku: Inaonekana elimu ya uongo ilikuwa ya namna ya Kiyahudi, kwa sababu twajua Wayahudi walithamini sana mambo ya nasaba n.k. Ajabu ni kwamba Paulo alisema kwamba hata wale waalimu wa elimu hiyo hawakuelewa yale ambayo walikuwa wakiyafundisha.

Ni rahisi zaidi kuingia majadiliano kuliko kuishi Kikristo; ni rahisi kujua vifungu vya Biblia kuliko kuvitii. Watu hupenda kusikia mambo mapya, kukuza elimu kuliko maadili, kusema kuliko kutenda, kujiona kuliko kujinyenyekea, kujua mambo kichwani kuliko kuwa na ujuzi wa kimaisha. Mafundisho mazuri, yenye uzima, huleta afya rohoni.

Paulo aliona ni vema aseme machache kuhusu Sheria. Paulo aliona kwamba Sheria hasa yawahusu wasiomcha Mungu na wakosaji, ila hakuendelea kuonyesha kwa njia gani ni hivyo. Taz. Gal.3:23-4:7; Rum.7:7-25. Katika sehemu hizo Paulo alisema lengo la sheria ni kufunua na kuchokoza dhambi na kuzuia dhambi, na kuonyesha jinsi wenye dhambi hawana njia yoyote ya uponyaji isipokuwa kujitupa kwa Mungu na rehema zake. Hao waalimu wa sheria hawakuelewa sababu hizo. Sheria ni njema ikitumiwa kwa halali, si halali kuitumia kwa majadiliano juu ya hadithi na nasaba.

k.9-10 Paulo alitaja matokeo mabaya yaliyosababishwa na mafundisho ya uongo.

k.11 Paulo alieleza Injili kuwa Habari Njema ya Utukufu wa Mungu (2 Kor.4:4- 6) ambayo yeye alikuwa amekabidhiwa, halafu Paulo ameikabidhi kwa Timotheo na Tito, na waumini wote. Ni wajibu wao kuilinda kwa nguvu zao zote na kuikabidhi kwa wengine. Huu ndio “mfuatano wa KiMitume” si kupokezana kwa cheo cha Uaskofu bali ni kupokezana, kizazi baada ya kizazi, kwa mafundisho ya kweli, yale mafundisho ya Mitume wa kwanza, waliyofundishwa na Yesu Mwenyewe. Kazi kubwa ya Timotheo pale Efeso ni kuwakabili waalimu wa uongo na kuwakataza wasifundishe elimu yao ya uongo.

1:12-17 Kazi ya Injili katika maisha ya Paulo

Paulo alimshukuru Yesu Kristo kwa kumrehemu na kumwokoa na kumweka katika utumishi wa Injili. Paulo hakuweza kutaja Injili bila kushikwa na mshangao mkubwa alipokumbuka jinsi Mungu alivyomtendea makuu alipomgeuza kutoka kuwa mpinzani mkuu na kumfanya kuwa mtumishi wake mtiifu sana. Alimshukuru Bwana Yesu kwa sababu alikuwa ameonja nguvu zake maishani mwake. Zaidi ya kumwokoa Mungu alimwamini kiasi cha kumweka katika kazi ya kuitumikia Injili na kumpa uwezo wa kutimiza huduma aliyopewa. Nguvu zote za Paulo zilitokana na habari hii. Hapo nyuma alikuwa mkatili, mjeuri, mtu aliyekosa huruma, aliyekusudia kumaliza kabisa Kanisa na watu wake. Lakini Mungu alimkamata, akambadili, akamfunulia Yesu na maana ya tendo kuu la Yesu kutoa maisha yake pale Msalabani kuwa dhabihu ya dhambi.

k.13 Alitambua rehema ya Mungu kwa hali yake ya kuudhi Kanisa, kwa sababu iwapo alikuwa amefanya dhambi kubwa, hata hivyo, alifanya akidhani alikuwa akifanya mapenzi ya Mungu, kumbe, siyo.

k.14 Ni neema ya Mungu iliyomvuta kumwamini na kumpenda Kristo. Lilikuwa itikio lake kwa tendo kuu la Mungu kumhurumia. Hayo yote ni tofauti sana na wale wazee ambao wameyageukia mambo ya ubatili (1:6) na baadhi yao wamemtukana Mungu (1:20) nao wamesababisha fitina Kanisani, (6:4), na kwa sababu hizo wameiacha Injili ya neema.

k.15 Paulo alipofunuliwa na kufahamu neno hilo, basi alijiona na kujihesabu kuwa wa kwanza katika wenye dhambi. Hakusema “alikuwa” bali aliandika kama bado angali ni mwenye dhambi, ila tofauti ni kwamba sasa ni mwenye dhambi aliyesamehewa na kupokelewa na Mungu.

Kifungu cha 15 ni kama Ukiri ambao Wakristo walizoea kusema. Katika Ukiri huo mambo mawili yametajwa: (1) Yesu kuja ulimwenguni; na (2) Yesu kuokoa wenye dhambi. La pili ndiyo sababu kuu ya Yesu kuja ulimwenguni humo. Wenye dhambi ni wanadamu wote, Wayahudi kwa WaMataifa (Rum.3:19-20, 23). Na wokovu huo wa Yesu unahusu “mwisho” wa watu, yaani uzima wa milele au mauti ya milele, pia ndani yake ni uwezo wa watu kuokolewa sasa, maana yake, wasitawaliwe na dhambi.

k.16 Paulo alitambua ya kuwa amewekwa awe kielelezo chema na mfano bora kwa wote watakaomfuata katika utumishi wa Kikristo. Hakuona kwamba yeye amestahili chochote ila kwa rehema za Mungu peke yake amekuwa kama alivyo. Kama Mungu amefanya hayo makuu katika maisha yake, Mungu aweza kufanya makuu katika maisha ya wengine.

Aliona kwamba Mungu huwa Mvumilivu wa ajabu, mwenye subira nyingi katika kuukabili uasi wa wanadamu.
k.17 Alipokumbuka hayo yote alirudia kumsifu Mungu. Kwa Paulo Mungu ni asili ya yote. Mungu ni wa milele, yule wa kudumu, hataharibika wala hatatoweka, hamna mwingine kama Yeye. Kwa hiyo, daima apewe sifa na heshima na utukufu. Yawezekana maneno hayo ni ukiri uliotumiwa katika ibada, msalishaji akisema maneno na watu wakiitika kwa kusema “amina”.

Watumishi wote na hasa wale ambao wamejaliwa kushika nafasi za uongozi na kuwa na vyeo katika Kanisa wapaswa kukumbuka hali zao kabla ya kuokolewa na jinsi walivyokuwa na jinsi walivyo sasa kutokana na rehema za Mungu, kusudi wasijione na kushikwa na kiburi.

1:18-20 Agizo la Paulo kwa Timotheo

Paulo na Timotheo walikuwa kama baba na mwana katika Imani. Lakini hapo twamwona Paulo kama Jemadari Mkuu akimwagiza askari wake Timotheo. Huduma aliyo nayo Timotheo ni nzito, yeye yumo vitani, naye anao wajibu wa kupigania vita ya Injili vizuri. “kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako”. Maneno hayo yanatuelekeza kufikiri kwamba Paulo alijaliwa ufunuo juu

ya Timotheo, na ufunuo huo ulimwongoza kumchukua na kumweka kuwa mtumishi. Kwa hiyo, twaweza kumaanisha kwamba ni Roho Mtakatifu, siye Paulo peke yake, aliyemweka pale Efeso. Bila shaka Timotheo alipata msaada na kutiwa moyo na nguvu alipokumbuka kwamba wito wake ulitoka kwa Mungu na ya kuwa Paulo alijua kwamba Mungu alikuwa amemchagua kutumika pamoja naye halafu kumshikia baadaye, Paulo atakapofariki dunia. Imani na dhamiri safi ni silaha zake katika vita hiyo.

k.19 Alipotaja imani na dhamiri safi Paulo aliwakumbuka wawili ambao hawakujali vitu hivi. Waliingia shida kwa sababu walipoanza kuteleza katika imani yao walipuuzia mashtaka ya dhamiri zao.

k.20 Mmoja aliitwa Himenayo, naye ametajwa tena katika 2 Tim. 2:17. Mwingine aliitwa Iskanda. Jina hilo latokea katika Mdo.19:33 na 2 Tim.4:14. Kama ni huyo aliyetajwa hapo, au ni mwingine, hatujui kwa hakika. “nimempa Shetani watu hao” (taz.1 Kor.5:5). Ni lugha ya kueleza marudi makali. Pengine maana yake ni kwamba walitolewa nje ya sharika la Kikristo. Au yawezekana walipatwa na madhara ya kimwili (Mdo.5:1-11; 1 Kor.11:30). Ni vema kuona ya kuwa shabaha ya marudi hayo ilikuwa “wafundishwe wasimtukane Mungu”. Marudi yalitolewa katika matumaini kwamba hao watu watajirekebisha na kupona.

2:1 - 4:16 IBADA NA TARATIBU KATIKA KANISA

Hapo Paulo alifikia neno kuu la barua yake kwa Timotheo. Katika sehemu hiyo ametoa maagizo na mashauri juu ya mipango ya Kanisa. Je! ni kwa njia gani Timotheo atadumisha mafundisho yenye uzima na kuwatunza waumini? Paulo alimwelekeza kuangalia Ibada ya Kanisa.

2:1-8 Umuhimu wa sala za watu

Jambo kubwa la kwanza ni umuhimu wa maombi katika mikutano yao. Alitaja mambo ya kuombewa. Maombi ni silala kubwa katika vita ya Imani.

k.1 Maneno “kabla ya mambo yote” hayahusu orodha ya maombi ila ni kukaza umuhimu wa mambo fulani. Paulo alitumia maneno mbalimbali kuonyesha upana na utajiri uliomo katika jambo la Maombi - dua, sala, maombezi, na shukrani. Hizo zote ni sehemu mbalimbali katika Maombi. Tena alisema kwamba maombi yawe kwa ajili ya “watu wote”; Wakristo wajibika kupanua mawazo yao, wasikumbuke mambo ya Kanisa na ya kiroho tu. Mkazo ni juu ya maombi kwa watu wote taz.k.1, 4, 6.

Twashauriwa kuwaombea viongozi wa mataifa, wale wenye madaraka, wale walio na uwezo wa kuleta amani na utulivu. Kwa nini? ni kwa sababu hali hizo njema huwasaidia Wakristo kuishi maisha mazuri ya kumcha Mungu. Pia hali

hizo zasaidia uenezi wa Injili na kurahisisha mawasiliano kati ya mataifa mbalimbali. Katika kutaja “wote wenye madaraka” alikuwa akiwalenga wale waalimu wa uongo na wazee ambao walisababisha watu wa nje kuwaza Injili na Kanisa vibaya - (taz. 3:7; 5:14; 6:1).

k.3-4 “hilo ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu”. Ni lipi lililo zuri? Kutokana na mazingira ya maneno hayo jibu ni “maombi kwa ajili ya watu wote”. Neno hilo lampendeza Mungu sana. Kwa maana Yeye ni Mwokozi, na Yeye hutaka watu wote waokolewe, hivyo twaitwa kuwaombea watu wa kila hali na kila mahali. Katika kuwaombea watu twajua kwamba haja yao kubwa ni kupata wokovu. Ndiyo sababu twawaombea watawala ili amani na utulivu uwepo, kusudi Habari Njema ienezwe mahali pote na kwa watu wote.

“hutaka watu wote waokolewe” siyo kusema kwamba kila mtu ataokolewa ila kwamba nia ya Mungu hasa ni kwa watu kupata nafasi ya wokovu kwa kujua yaliyo kweli. Tunapomwomba Mungu kwa ajili ya watu twamwomba Yule ambaye tabia yake ni kuokoa. Daima Mungu huonyesha huruma na fadhili kwa watu bila kujali kabila, rangi, hali na cheo. Tena, mkazo ni juu ya Injili kuwa kwa wote, hivyo wote wahitaji kusikia ujumbe wake ulio kweli. Iwapo itikio lao ni la imani, ni imani katika kweli, si katika mafundisho yaliyopotoka.

k 5-6 Msingi wa maombi na wokovu wa watu ni katika Mungu kuwa Mmoja, hamna miungu mingine, kwa hiyo ni wazi kwamba Yeye ni Mungu wa wote. Vilevile yuko Mpatanishi Mmoja kati ya huyo Mungu mmoja na wanadamu wote, naye ni Yesu Kristo. Kwa njia ya Kifo chake Yesu amefanya ukombozi kwa ajili ya wote. Hivyo, watu hupata wokovu mmoja, na hutendewa sawa kwa kuokolewa kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo. Yeyote atakayemkubali Yesu Kristo na kumpokea kama Mwokozi wake ataokolewa. Paulo aliukaza Ubinadamu wa Kristo kwa sababu ilimbidi Kristo afanyike mwili ili astahili kuwa mjumbe wetu na kuchukua mahali petu ili upatanisho ufanyike.

Kwa sababu Yesu ni Mkombozi, Yesu amelipa fidia ya Nafsi yake kwa ajili ya wote (Mk.10:45) hivyo Mungu hutaka watu wote waokolewe na ni wajibu wetu kuwaombea watu wote ili hayo mapenzi ya Mungu yatimizwe kwao. Tendo hilo la ukombozi budi lishuhudiwe kotekote ulimwenguni.

k.7 Alipozidi kuwaza jambo hilo Paulo alishangaa kwa jinsi Mungu alivyomweka yeye kuwa mhubiri, na mtume, na mwalimu wa WaMataifa katika mambo hayo makuu sana. Katika kusema “wa WaMataifa” aliendelea kusisitiza Injili kuwa kwa watu wote. Huenda wale waalimu wa uongo walijikusanyia watu kadha tu na kuwa kama kundi tofauti na wakristo wengine, wakijiona kuwa bora. Kazi ya Paulo ilikuwa kuitangaza Habari hizo Njema, alitumwa kwa kusudi hilo, na tena, zaidi ya kuwa mtangazaji wa Injili aliieleza na kuifanafua kinaganaga kama mwalimu. Timotheo hakuwa na haja ya kukazwa habari za Paulo kuwa Mtume halisi isipokuwa hiyo barua pia ni kama barua rasmi kwa

Wakristo, na Timotheo atatiwa nguvu atakapokutana na wale waliompinga Paulo huko Efeso. Kwa vile alivyotumwa na Paulo ameshirikishwa mamlaka yake ya KiMitume. Yeye yuko Efeso kwa kulitii agizo la Paulo la kuyatengeneza mambo fulani. Paulo alihesabu kwamba uhalali wa Huduma yake kwa WaMataifa ulitegemea uhalali wa Utume wake, yaani kutumwa na Mungu.

k.8 Paulo alisema kwa nguvu “nataka...” akiagiza wanaume wasalishe watu kila mahali. Ni wajibu wa Wakristo kuomba daima mahali walipo. “kuinua mikono” ilikuwa desturi ya Wayahudi kuinua mikono walipoomba. “iliyotakata” maana yake wayatengeneze makosa yao kabla ya kuomba. Wayahudi walizoea kunawa mikono kabla ya kuomba.(Zab.26:6). “pasipo hasira wala majadiliano” hali hizo ni kinyume kwa mtu anayemkaribia Mungu katika ibada na maombi. Mtu awe na nia safi na matendo safi. Maneno hayo yanatukumbusha maneno ya Yesu (Mt.5:23-24) Mkazo wa Paulo si juu ya wanaume hasa bali ni juu ya watu kuomba katika hali njema bila hasira na majadiliano tofauti na waalimu wa uongo waliosababisha fitina na majadiliano.

2:9-15 Mahali pa wanawake katika ibada za Kikristo

Katika makanisa mengine shida zilitokea kutokana na wanawake waliookolewa. Walikuwa wamehakikishiwa usawa wao na wanaume katika ubinadamu wao na katika wokovu wao. Jambo hilo liliwafanya kuufurahia sana uhuru wao na baadhi yao walizidi wakifanya kila kitu walichofanya wanaume hata kuwazidi. Waliingizwa katika Kanisa kwa ubatizo bila tofauti yoyote na wanaume. Walisali pamoja bila ubaguzi wowote. Kwa kweli hali yao ilibadilika sana. Huenda pale Efeso wale waalimu wa uongo walivuta wanawake kadha kwa upesi, wakawadanganya.(1 Tim.1:5:11; 2 Tim.3:6).

Hivyo, Paulo aliona vema kusema kwa nguvu juu yao. Kwanza, aligusa hali zao za nje, mavazi na kuonekana kwao, ndipo alisema juu ya hali zao za ndani. Kwa nje, wavae vizuri bila mapambo na umalidadi. Tena, wawe na adabu. Si ajabu kufikiri kwamba wengine walithubutu kujiinua juu ya waume zao na kusemesema. Kwa ndani, wajipambe kwa moyo uliotulia, waonyeshe imani yao ya kumcha Mungu kwa njia ya kufanya matendo mema. Kwa njia hizo watatoa ushuhuda mzuri bila kujionyesha na kujiweka mbele. Paulo hakutaka watu wa nje wawe na wasiwasi juu ya yaliyotendeka katika mikutano ya Kikristo na kuwaza vibaya juu ya uhusiano kati ya wanaume na wanawake wa Kikristo.

k.11-12 Paulo alifundisha kwamba ni kazi ya wanaume kufundisha na ni vema wanawake wajifunze katika hali ya utulivu na utii. Katika hali hizo mwanamke hupata utukufu wake. “kumtawala mwanamume” neno “mwanamume” ni katika lugha ya mmoja si wengi, kwa hiyo yawezekana Paulo alikuwa akisema juu ya uhusiano wao katika ndoa.

Tusifikiri kwamba wanawake hawakuwa na nafasi yoyote katika Ibada, Tazama 1 Kor.11:5 juu ya wanawake kusali na kuhutubu, na katika 1 Kor.14:26ku. maneno “kila mmoja”, yanaonyesha kwamba wanawake walihudhuria ibada na kuruhusiwa kuchanga kitu sawa na wanaume. Katika Tito 2:3-4 wanawake wazee walipewa wajibu wa kufundisha wanawake vijana. Katika Rum.16:1 Fibi ameitwa “mhudumu”. Paulo hakutaka wanawake wakae kimya kabisa, la. Yawezekana amesema kwa nguvu hapo kwa sababu ziko dalili za wanawake kadha kuwa wamepotea kwa upande wa imani, na wamekuwa wepesi wa kudanganywa, huenda kwa sababu ya hali ya pale kutokana na waalimu wa uongo.

k.13 Msingi wa mafundisho hayo ya Paulo ni katika Utaratibu wa Uumbaji. Mungu alitangulia kumwumba mwanaume ndipo akamwumba mwanamke. Iwapo ubinadamu wao ni sawa na wote wawili wameumbwa katika sura na mfano wa Mungu, wa kwanza kuumbwa alikuwa mwanaume. Katika 1 Kor.11:9 Paulo alieleza habari hiyo zaidi. Paulo aliona utaratibu huo ufuatwe katika maisha ya wanadamu.

k.14 Sababu nyingine iliyomwongoza Paulo ni katika Hawa kudanganywa na nyoka. Aliona ya kuwa mwanamke asimwongoze mwanaume kwa sababu Hawa alimshawishi Adamu hata akaanguka. Katika Warumi 5:12ku. Paulo alifundisha kwamba ni kwa njia ya Adamu dhambi iliingia ulimwenguni, kwa hiyo Adamu ni mjumbe wa wanaume wote. Ilimpasa Adamu kumsaidia Hawa, akawa na hatia katika wote wawili kumwasi Mungu. Hawa ni kama mjumbe kwa upande wa wanawake.

k.15a Hawa alipewa adhabu kuhusu uzazi wa kimwili, aliambiwa atazaa kwa shida na maumivu (Mwa.3:16). Hapo Paulo amesema kwamba mwanamke atazaa kwa usalama. Katikati ya kifungu alibadili na kusema kwa wingi si kwa mmoja tu. Kwa jumla, wanawake watabarikiwa katika maisha yao ya Kikristo, wakidumu katika imani, upendo, utakaso, na moyo wa kiasi. Neno la “kiasi” lilihusu na kugusa yeyote aliyezidi mpaka katika kujionyesha na kusemasema n.k

Siku hizi, siku ambazo wanawake wengi wamejaliwa nafasi za juu katika maeneo mengi ya kazi, maneno hayo ya Paulo yamesababisha maswali mengi. Mageuzi makubwa yametokea katika jamii. Hivyo wengi katika Kanisa wameona ya kuwa maagizo hayo ya Paulo hayana mamlaka kwa siku zetu. Yalifaa wakati ule lakini hayafai wakati wetu.

Ni vigumu kujua kwa uhakika tuseme nini. Neno moja ni kutambua kwamba msingi wa mafundisho hayo ya Paulo ulikuwa Utaratibu wa Uumbaji, si mazingara yaliyokuwepo. Kwa hiyo, swali kubwa kwetu sisi ni “Je! Mungu alitaka tuufuate utaratibu wa uumbaji wakati wote au siyo?

Pamoja na hayo, Je! kielelezo cha Bwana Yesu katika kuwainua na kuwaheshimu wanawake chapita madai ya utaratibu wa uumbaji au siyo? Twaweza kusema kwamba, kwa jinsi alivyofanya, Yesu alisababisha wanawake kuamka na kushirikiana bega kwa bega na wanaume katika mengi ya maisha.

Neno jingine la kutafakari ni kuhusu wanawake wengi kusikia wito wa kumtumikia Mungu katika Kanisa. Hao wanawake husema kwamba wamesikia wito kwelikweli. Kama ni hivyo, Je! hao wote wamedanganywa? La, siyo, ni vigumu kuwakataa, kwa sababu kama wito wao umetoka kwa Mungu ni wazi kwamba Mungu hupenda wamtumikie katika Kanisa.

Kwa kujumlisha twaweza kusema ni vema tukumbuke mazingara ya kuwepo kwa waalimu wa uongo ambao waliwachochea wanawake na kuwaruhusu kuwa uhuru wa kusema na kufanya jinsi walivyosikia.

3: 1-13 Sifa na tabia zilizotakiwa katika watumishi wa Kanisa

3:1-7 Kwanza alisema juu ya Maaskofu/Waangalizi. Katika habari hiyo tusiwawaze watu hao kuwa kama walivyo siku hizo. Maana siku zile walikuwa wa palepale, katika sharika fulani, wakiwa na madaraka palepale tu. Hawakuwa na eneo kubwa. Tena katika nyakati za Agano Jipya, si mtu mmoja aliyewekwa kuwa askofu au mwangalizi bali walikuwa kundi la watu, mfano wa wazee katika sharika au mtaa wa leo. Neno “askofu” ni sawa na neno “mwangalizi”. Maneno hayo mawili yalionyesha kazi na wajibu wake pamoja na cheo na heshima yake. Ni kabla ya kuwekwa kwa Madayosisi au Uaskofu. Yeyote aliyepewa uangalizi wa aina yoyote aliitwa hivyo. Polepole katika karne ya pili kwa jinsi Kanisa lilivyopata kukua na kuenea, badiliko lilitokea, kisha twakuta mmoja wa waangalizi kuwekwa juu ya waangalizi wengine na kupewa madaraka juu ya makanisa yote katika eneo fulani, na “wazee” walianza kuitwa mapresbyter neno lililo sawa na mapasta, wachungaji, makasisi, watu walioshika mitaa. Halafu baadaye Kanisa lilionekana kuwa na mpango wa Askofu, Wachungaji/Mapasta, na Mashemasi. Mpango ambao upo katika Kanisa la Kianglikana na makanisa mengine mpaka leo.

Ni msaada kutazama vifungu hivi vya Agano Jipya: Mdo.20:17, 28; Flp.1:1; Tito 1:5, 7.

Twaona ya kwamba iwapo shida zilikuwepo katika masharika mbalimbali, hatuoni kwamba barua zilitumwa kwa waangalizi wa sharika, wala hatuoni Paulo aliwapa madaraka ya kupinga mafundisho ya uongo.

k.1 Paulo alianza na “ni neno la kuaminiwa”, ni mara ya pili kutumia usemi huo (1:15) Lakini neno la pili halikuhusu “imani”, ni kama njia yake ya kutilia mkazo jambo fulani.

Timotheo hakuachwa Efeso ili awaweke waangalizi/wazee, tofauti na Tito aliyeachwa Krete ili afanye hivyo.(Tito 1:5) Neno hilo la kuaminiwa ni neno zuri. Lipi ni zuri? Jibu ni mtu kutaka kuwa mwangalizi katika Kanisa. Kwa nini? ni kwa sababu ni kazi njema. Mkazo ni juu ya kazi, si juu ya mtu wala cheo. Kazi hii ni nzuri kwa sababu ni kazi ya kiroho na wote wanaothamini mambo ya kiroho huthamini wale wanaowaongoza katika maisha yao ya kiroho. Hivyo Paulo alihesabu kwamba ni jambo jema kwa mtu kutamani kazi hiyo.

k.2ku Katika sehemu hiyo Paulo alitaja wazi zile hali na tabia zifaazo kwa kazi hiyo.

“mtu asiyelaumika” yaani awe mtu mwenye sifa nzuri kati ya watu. Mtu ambaye kwa kutazama maisha yake ya nje hashtakiwi neno. Itakuwa vigumu mtu awe na nguvu ya kuwasimamia Wakristo ikiwa yeye mwenyewe ameshindwa kupata kibali cha watu katika maisha ya kila siku. Kwa kawaida watu wa nje hutambua kwa haraka mtu mnafiki.

“mume wa mke mmoja”, maana ya neno hilo si wazi kwa sababu Wakristo wote walidaiwa kuwa na mke mmoja. Yawezekana maana yake ni kwamba awe mtu aliyeoa mara moja tu. Kabla ya kuokolewa Wakristo wengi walizoea kuwa na wake wengi, kwa hiyo, inawezekana maana yake ni kwamba asiwe mtu ambaye hapo nyuma alikuwa na wake wengi. Maana nyingine ni asiwe mtu aliyefiwa halafu akaoa tena. Kwa vyovyote twaweza kusema kwamba mkazo ni juu ya waangalizi kuwa na ndoa nzuri kinyume cha kawaida ya siku zile ili wawe kielelezo kwa wenzao.

k.2 “mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu” Mambo hayo matatu huandama pamoja na kwa jumla ni kusema kwamba mwangalizi awe na maisha ya utulivu na utaratibu mwenye uwezo wa kujitawala na kuongoza maisha yake mwenyewe, kwa sababu ni dhahiri kwamba mtu aliyeshindwa kuongoza maisha yake atashindwa kabisa kuwaongoza wengine.

“mkaribishaji” Wajibu mmoja wa kazi yake ilikuwa kupokea wageni, kwa sababu katika hali ya siku zile za kwanza, wakristo waliojitoa kwenda huko na huko katika kufanya uinjilisti, pamoja na wakristo wa biashara waliosafiri huko na huko, walihitaji mahali pa kufikia, mahali pa usalama kimwili na kiroho. Tukumbuke ya kuwa walizungukwa na umati wa wapagani, hivyo katika nyumba za wageni wangalipata shida na majaribu mengi. Wakristo wote walishauriwa kuwa na tabia ya ukaribishaji, kwa hiyo, si ajabu viongozi wao watoe kielelezo chema. (Taz. 5:10; Rum.12:13; 1 Pet.4:9).

“ajuaye kufundisha” Neno hilo lahusika na kazi ya mwangalizi. Alikuwa na wajibu wa kufundisha Wakristo na kuwasaidia watu. Kwanza, waielewe Injili na Imani ya Kikristo, pia waelekezwe katika maisha yao jinsi ya kuishi iwapasavyo kama Wakristo. Tena tukumbuke ya kwamba wengi waliotoka katika upagani

karibuni hivi walihitaji sana kupewa mwongozo. Hivyo kazi moja kubwa ya waangalizi ilikuwa kufundisha, kwa hiyo wawe na maelekeo na uwezo wa kufundisha na kupinga mafundisho ya uongo.

k.3 Baada ya kutaja hali zilizotakiwa Paulo alitaja jambo moja la kuepa yaani ulevi. Ulevi umekatazwa katika Maandiko, ila kutumia mvinyo kidogo hakukatazwa 3:8; 5:23; Tito 1:7. Ukali, ugomvi, na kupenda fedha ni tabia zinazokwenda pamoja, nazo ni kinyume cha Imani ya Kikristo. Wale wazee wa shida walikuwa na tabia hizo (6:3-5; 2 Tim. 2: 22-26; Tito 3:9). Wazee wa kweli wawe wapole, hata katika kukemea wengine (2 Tim.2:23-25). Ni tabia ambayo Bwana Yesu Mwenyewe aliionyesha katika maisha na huduma yake. Hata alipofanyiwa ujeuri na kupigwa hakurudisha matukano wala mashutumu. Alidai "Mimi ni mpole - njooni Kwangu, mjifunze Kwangu" (Mt.11:28). Mtu anayewasimamia Wakristo wenzake na awe amekolea tabia ya upole, dalili ya ushirikiano wake na Yesu, Bwana wake.

Kuhusu kupenda fedha, katika 1 Tim. 6:5-10 Paulo aligusa neno hilo akidokezea ya kuwa tabia hiyo ndiyo sababu moja ya wazee wengine kuanguka.. Hali hiyo imetajwa tena kuhusu mashemasi (1:8; Tito 1:7; Mdo.20:33).

k.4 Kiongozi atakayefaa ni yule ambaye kwanza amefaulu kuisimamia nyumba yake vizuri pamoja na kuwalea watoto wake vizuri. Kama mtu ameshindwa kuisimamia nyumba yake atawezaje kusimamia familia ya Wakristo, watu wasio wa damu moja na yeye. Kazi ya kusimamia familia yake mwenyewe na familia ya Wakristo hufanana sana, hivyo Paulo aliona ya kuwa mwenye kufaulu kusimamia familia yake tumaini lipo kwamba ataweza kusimamia familia ya Mungu, yaaani Wakristo, na kinyume chake atakayeshindwa kuisimamia nyumba yake itakuwa vigumu asimamie familia ya Mungu. Maneno hayo yaonyesha umuhimu wa maisha ya kifamilia kwa upande wa Wakristo. Haina maana kwamba watu watawale kwa nguvu hata kulazimisha utii, ila ni kuwaongoza na kuwatunza kwa hali zitakazosaidia watu kutii.

k.6 Neno lingine ambalo Paulo alifikiri ni neno jema ni kuhusu mwangalizi kuwa mtu ambaye amekuwa Mkristo kwa muda mrefu, mwenye uzoevu katika maisha ya kiroho. Huyo atakuwa na ujuzi mwingi juu ya Imani yake, na kutokana na ujuzi wa kibinafsi atajua jinsi ya kukabili magumu na shida na majaribu. Hatari moja kwa Mkristo mpya kupewa uangalizi ni kushikwa na kiburi, kabla hajaimarika, na kabla hajapata nafasi ya kutosha kuthibitika katika Imani ya Kikristo na kabla ya kuwa na uzoevu katika maisha ya Kikristo. Itakuwa rahisi kwa watu kuleta mashtaka juu yake, pia itakuwa vigumu kwa Wakristo wenzake kumjali. Paulo alimkumbusha Timotheo kwamba Shetani alianguka kwa sababu ya kiburi. Wazee walioteleza walikuwa watu wa kujivuna

(1 Tim.6:4), huenda baadhi yao walikuwa watu walioongoka karibuni hivi, ila hatujui.

k.7 Hapo twakumbushwa maneno ya k2. Iwapo imani ya Kikristo ilipingwa sana, hata hivyo watu wa nje waliweza kuwatambua wale waliokuwa Wakristo wa kweli na pia walitambua wale ambao hawakuwa waaminifu katika imani yao. Kwa hiyo lilikuwa jambo la maana kwa mtu aliyewekwa kuwa msimamizi kushuhudiwa vema na watu wa nje. Ilikuwa vigumu kuleta mashtaka juu yake, pia ilikuwa vigumu kwa Shetani kumnasa. Wakati wote Paulo alikuwa na mzigo juu ya Wakristo kuwazwa vema na watu wa nje, kusudi Injili ipate kibali machoni pa watu, Shetani asije akafurahi.

3: 8-13 Mashemasi

Katika makanisa walikuwapo kundi la watu, pamoja na waangalizi, na pengine chini yao, walioitwa watumishi au mashemasi. Huenda asili yao ni katika Wale Saba waliowekwa kuhudumu mezani (Mdo.6:1ku.). Katika hao watu kama Filipo na Stefano walihubiri Injili. Hatusomi Wale Saba waliitwa “mashemasi”. Katika Filipi 1:1 mashemasi wametajwa pamoja na waangalizi. Huenda walifanya kazi za kiutendaji kama kuwatembelea watu, kutunza fedha za Kanisa na kuzigawa kwa maskini na wajane n.k. Neno la kuona ni kwamba walitakiwa kuwa na maisha mema, watu wa kiroho. Tusifikiri ni maaskofu tu waliohesabiwa viongozi, yawezekana hao mashemasi pia walifikiriwa hivyo. Hali moja ambalo halitajwi kwa mashemasi ambalo lilitajwa kwa waangalizi ni “ajuaye kufundisha”.

k.8 Kwanza wawe wastahivu, watu waliojiheshimu na kuheshimiwa kati ya watu. Halafu Paulo alitaja neno kuhusu mazungumzo yao, wasiwe na kauli mbili, wanyoke katika maneno yao, ili wapate kuaminika kuwa watu wa kweli. Wawe na uwezo wa kutunza siri za watu, pia wasieneze habari zisizo na uhakika, wala wasifulize uvumi zilizotokea.

Neno la mvinyo limetajwa kama lilivyotajwa kwa waangalizi. Yawezekana katika kuwatembelea watu walipewa kinywaji cha divai, maana divai ilikuwa kama chai ya siku hizi. Wawe na kiasi katika kuitumia.

Fedha imetajwa kama ilivyotajwa kwa waangalizi. Pengine walijaribiwa kutazamia kupewa vipawa kwa huduma yao. Pia kama walihusika na ugawaji wa fedha kwa wajane na maskini lazima wawe waaminifu. Wakiwa na tamaa ya fedha, basi, itakuwa vigumu wasijipendekeze kwa watu na kukosa uaminifu.

k.9-10 Iwapo mashemasi waliwashughulikia watu kiutendaji, pia walipaswa kushikilia vizuri Imani na kumtii Kristo. Wasiwekwe kuwa mashemasi mpaka kwanza wameonekana kuwa Wakristo waaminifu. Twakumbuka ya kuwa wale saba wa kwanza waliochaguliwa (Mdo.6) iwapo walichaguliwa kufanya huduma

ya mezani kwa wajane, walitakiwa kuwa na hali nzuri za kiroho (Mdo.6:3) Kutokana na 1:5-6 na 1:19-20 twajua kwamba wale waalimu wa uongo pale Efeso walikuwa wameacha dhamiri safi na kuteleza kwa upande wa Imani ya kweli. Kwa hiyo, hao mashemasi wajali ushuhuda wa dhamiri zao.
“wajaribiwe kwanza” siyo kusema wapewe muda wa majaribio, ndipo wawekwe, ila kwanza wawe wamechunguzwa kuona kama wanazo hali na tabia zifaazo ndipo wawekwe.

Hapo twajifunza kwamba ni jambo muhimu sana kwa Kanisa kuwa na uangalifu sana katika kuwachagua watumishi, haidhuru ni maaskofu, mapasta, wainjilisti, au watumishi kama makatibu, watunza fedha, madreva n.k. Lazima wachunguzwe kuhusu hali zao za kiroho na tabia zao za Kikristo, pamoja na maelekeo yao kwa kazi ili wasiwe na malawama, wala kuleta malawama kwa Kanisa.

k.11 Kuna mawazo mawili kuhusu sehemu hiyo, kwa sababu neno katika Kiyunani laweza kuwa na maana ya “wake” au “wanawake”. Kwa hiyo katika kifungu hicho yanayosemwa yaweza kuwahusu wake za mashemasi au kundi la watumishi wa kike kama mashemasi wa kike. Sababu ya wengine kufikiri ni mashemasi wa kike ni kwa sababu vifungu vya 8 na 11 vinalingana. Pia maneno “vivyo hivyo” ni kama maneno ya kuelekeza mawazo kwa sehemu iliyotangulia juu ya mashemasi. Pamoja na hayo hatuoni Paulo alisema lolote kuhusu wake za waangalizi.

Kwa kweli, hatujui kwa uhakika. Iliyo wazi ni kwamba ama ni wake za mashemasi ama ni mashemasi wa kike walidaiwa hali na tabia kama zile za watumishi wanaume. Wawe wastahivu, wasiwe wasingiziaji, maana baadhi ya wanawake huelekea kuwa na shida hiyo.

Kama halikuwapo kundi la mashemasi wa kike, inaonekana wanawake waliruhusiwa kushiriki shughuli kadha za Kanisa, hasa kwa upande wa wanawake wenzao, pengine kuwaandaa kwa ubatizo n.k. Walihesabiwa washiriki wa kazi za waume zao.

Picha tuliyo nayo ni ya Kanisa kudai uaminifu wa hali ya juu katika watumishi wake, upande wa wanaume na wa wanawake.

k.12 Kifungu hicho chahusu mashemasi. Paulo alirudia mkazo wa uaminifu katika ndoa zao na kusimamia nyumba zao vizuri. Bila shaka Paulo alifahamu kwamba kupendana kwao na uaminifu wao ni ushuhuda mkali kwa uwezo wa Injili, maana watu wengi walishindwa kuishi maisha safi.

Kama k11 kilihusu mashemasi wa kike, basi katika k12 Paulo alikumbuka neno kwa mashemasi na kuliingiza hapo.

k.13 “hujipatia daraja nzuri” Maneno hayo yana maana gani? Yawezekana maana yake ni kwamba shemasi mwaminifu atapata kupandishwa cheo hata awe msimamizi. Au, pengine, maana yake ni kwamba shemasi mwaminifu atazidi kuheshimiwa kati ya watu kwa sababu ya kazi yake nzuri. Au, pengine ni kwamba, mbele za Mungu, atahesabiwa kuwa wa kufaa.

Sababu ya kwanza ni kama kinyume cha tabia ya Kikristo. Sababu ya pili ni nzuri kwa sababu jambo la kushuhudiwa vema limetajwa kuwa hali moja iliyotakiwa. Sababu ya tatu pia ni nzuri nayo yapatana na maneno yanayofuata katika kifungu hicho “na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu”.

Kwa kweli, yeyote aliyetimiza hayo matakwa yaliyoandikwa katika sehemu hiyo hakosi aliendelea kiroho na kupata ujasiri wingi katika Imani

3:14-16 Kanisa

Paulo alikuwa na mzigo juu ya Kanisa na mipango yake, ila neno kubwa la kwanza lilikuwa hali yake ya kiroho. Wakati wote alishikwa na mshangao mkubwa alipouwaza utukufu wa Ujumbe wa Kanisa. Kwake mipango ya Kanisa iliandama na ujumbe wake wa utukufu, ila iliyozidi ni Ujumbe Mtukufu.

k.14 Paulo alitoa sababu ya kumwandikia Timotheo mambo hayo. Alikusudia kuja kwake karibuni hivi ila alimshauri la kufanya ikiwa atachelewa kumfikia, na mashauri hayo ni katika sura za kwanza hadi tatu.

Timotheo alikuwa ameachwa Efeso ili ayatengeneze mambo fulani kwa hiyo, barua ni kwa Timotheo (upate kujua) ila pia iliwahusu Wakristo na mienendo yao. Kikazi Timotheo aliwajibika kuweka viongozi katika makanisa kufuatana na maagizo aliyopewa na Paulo pamoja na yeye mwenyewe kuishi vizuri na kutoa kielelezo chema na kuwahimiza wakristo kuishi jinsi ilivyowapasa.

“katika nyumba ya Mungu” Kila kundi la Wakristo mahali walipo ni “nyumba ya Mungu” na sehemu katika Kanisa Zima. Ni familia ya Mungu Hai, Mungu akiwa pamoja nao akiishi ndani yao na kufanya kazi kwa njia yao. Hawafanani na hekalu ambalo ndani yake zimo sanamu zisizo hai, zisizosema wala kufanya lolote, tofauti na Mungu Hai wa Wakristo.

Paulo aliendelea kueleza kwamba Kanisa amekabidhiwa “kweli” yaani Injili na ni juu ya Kanisa kuihifadhi hiyo kweli, watu waifahamu vizuri, waifundishwe vema, tena wawe tayari kuishi kufuatana nayo. Kiongozi, kama Timotheo, alipewa wajibu wa kukomesha waalimu wa uongo (6:5; 2Tim 2:18; 3:8; 4:4) na kuwarudisha wale walioondoka katika kweli. Lengo ni kwa Mungu wa kweli kujulikana katika ulimwengu.

k.16 Maneno yanayofuata ni kama wimbo unaokiri “siri ya utauwa” na siri hiyo wale wamchao Mungu wenye moyo safi hufunuliwa. Ni siri kubwa, ila si fundisho fulani, bali siri yenyewe ni Kristo Maana Mungu, yaani Kristo alidhihirishwa katika mwili, kwa kuwa Kristo wa milele aliyekuwako kabla ya kuja duniani, akafanyika mwili, akaja duniani, akakaa kwetu kama Yohana alivyosema katika Injili yake (Yo.1:1-18). Kwa upande wa roho alikuwa Mwana wa Mungu, na Mungu alimthibitishia kuwa Mwana wake kwa kumfufua kutoka kwa wafu. (Rum 1:3-4).

“akaonekana na malaika” ni vigumu kujua maana ya maneno hayo. Pengine maana yake ni kwamba malaika walipata ujuzi mpya kutokana na Mungu kujifunua kwa ulimwengu kwa njia ya Yesu Kristo. Ujuzi huo uliwashangaza sana (Ef.3:10; 1 Pet.1:12).

Wazo lingine tofauti sana na hilo ni kwamba baada ya Kufufuka Yesu alijifunua kwa “mamlaka na enzi zilizo kinyume cha Mungu, katika ulimwengu wa roho” ili wapate kujua kwamba amewashinda na ya kuwa imewabakia hukumu tu. (Kol.2:15; Ef. 6:12; 2 Pet.2:4; 1 Pet.3:19-20; Yud.6).

Wazo lingine ni kamba Yesu alipofufuka na kutukuzwa huko juu malaika nao walimtukuza sana sana.

Ni vigumu kujua hasa maana halisi, ila ile maana ya kwanza inapatana na maneno yanayofuata “akahubiriwa katika mataifa” Malaika walipata kumfahamu Yesu vizuri zaidi, Ukuu wake, na ya kwamba Yesu Ndiye kifunguo cha historia yote. Ndipo baada ya Yesu kuuawa, kufufuka, na kupandishwa juu kama Mshindi Mkuu ndipo WaMataifa huhubiriwa habari zake.

Ufunuo wa Mungu katika Mwana wake ni mpana sana, katika eneo la kiroho, malaika na enzi zote wamejulishwa habari zake. Katika eneo la kimwili wanadamu wote hutangaziwa habari zake.

“akaaminiwa katika ulimwengu” Ushindi wa Yesu unaonekana katika maitikio ya watu kumwamini. Thawabu yake ni kupata umati wa watu kumwamini na kujitoa kuwa Wake, na thawabu yake kibinafsi ni kupandishwa kwenye Utukufu wa Mungu juu.

Wimbo hautaji habari za Kifo na Kufufuka kwa Yesu, ila yaliyotajwa ni matokeo yake. Pengine tunayo sehemu tu ya wimbo.

Kanisa ni nyumba ya Mungu, Kanisa halikubuniwa na wanadamu. Ni sharika la watu walioumbwa mpya na Mungu aliye Hai. Lilitokea kutokana na Injili. Kanisa halikuunda Injili ila Injili ilitokeza Kanisa.

4:1-5 Paulo alikemea mafundisho ya uongo

Katika sehemu hiyo Paulo alimwonya na kumwagiza Timotheo juu ya kutokea kwa mafundisho ya uongo na waalimu wake.

k.1-2 Wasingalishtuka kwa kutokea kwa waalimu wa uongo kwa sababu Roho alikuwa amenena waziwazi juu yake. Kwa jinsi gani Roho amenena waziwazi? Hatuambiwi. Twajua ya kuwa katika Kanisa walikuwapo manabii waliotabiri mambo mbalimbali ili Kanisa liandae tayari kwa ajili yake. Agabo alikuwa mmoja wao (Mdo.11:28; 13:1; 20:23; 21:10-11). Wao na kipawa chao walithaminiwa sana. Yawezekana nabii fulani alikuwa ametoa unabii wa habari hiyo.

Pengine Paulo alikuwa akiwakumbusha mausia yake alipoagana na wazee wa Efeso, maana aligusa habari hiyo ya kutokea kwa shida hiyo (Mdo.20:28-31). Bila shaka Wakristo walifundishwa kwamba Yesu Mwenyewe alisema wazi juu ya kutokea kwa wadanganyaji na uasi utakaotokea, hasa kabla ya Kurudi Kwake kwa mara ya pili (Mt.24:11).

“nyakati za mwisho” Katika Agano Jipya muda wote wa tangu Yesu Kuja mara ya kwanza hadi Kuja Kwake kwa mara ya pili umehesabiwa ni “mwisho” kwa sababu yote yaliyotakiwa kufanywa kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu yametendeka. Ila ndani ya nyakati za mwisho “mwisho” wao, mwisho kabisa utafika. Paulo aliona ya kuwa uasi ni dalili na malimbuko ya Kuja kwa Yesu mara ya pili (2 The.2:1ku.). Lakini hapo Paulo alimwelekeza Timotheo juu ya wakati ulio karibu.

Ni nini hasa ambalo Roho alilifunua? Roho alifunua kwamba katika Kanisa baadhi ya waumini wataondoka katika kweli za Imani. Kwa nini wataondoka katika kweli? Wataondoka kutokana na shughuli za waalimu wa uongo watakaowashawishi watu vibaya kwa kutumia uongo. Katika k.2 Paulo aliwaita “wanafiki wasemao uongo” (2 Tim.2:16-18; 3:13; 4:3-4). Nyuma yao ni Shetani ambaye tabia yake ni kudanganya na tangu mwanzo silaha yake kubwa imekuwa uongo. Yeye ni mpinga Kristo na Injili. Maneno “roho zidanganyazo” na “mafundisho ya mashetani” ni lugha ya kueleza asili ya mafundisho yote yaliyo kinyume cha Injili kuwa Shetani. Hao watu wamekufa ganzi kwa sababu wamefisha dhamiri zao na kwa kufanya hivyo wamekosa kitu cha ndani ambacho kingaliwasaidia kutambua vema. Onyo ni kwamba tusipojitoa kwa kweli mlango u wazi kwa kukamatwa na uongo.

Jambo hilo lilikuwa likitokea pale Efeso na ndiyo sababu ya Paulo kumwandikia Timotheo ili aanze mara moja kuchukua hatua za kuyatengeneza mambo, hata kabla ya yeye kufika.

Twafundishwa umuhimu wa kuipigania Injili na kuwafundisha waumini kweli zake ili wawe na msingi imara tayari kupambana na wale watakaojaribu kuwapotosha. Katika siku zetu ajabu ni kwamba ni wachache tu walio tayari kuyakemea mafundisho yasiyo kweli yanayoenezwa na kuaminiwa katika makanisa yetu.

k.3-5 Ndipo Paulo alitoboa wazi hali ya hayo mafundisho. Yalihusu mambo mawili hasa: ndoa na vyakula. Walifundisha kwamba watu wasioe, pia wasile vyakula fulani (Kol.2:16ku.).

Mafundisho yao ni kinyume cha kweli, kwa sababu ni Mungu Mwenyewe ambaye ameviumba vyakula vyote ili vipokelewe kwa shukrani. Waumini wa Injili wamewekwa huru mbali na sheria na miiko kuhusu vyakula (Mko.7:19; Mdo.10:19-26; Mwa.1:31; Tit.1:14-26). Tukitazama 1Kor.10:23-33 na Rum.14:1-23 Paulo alifundisha kwamba watu wasihukumiane kuhusu kula au kutokula, na zaidi watu wasitoe amri kwa wengine, maana chakula chenyewe hakina upande (ni “neutral”).

Kwa neno la ndoa, ni Mungu aliyeamuru ndoa ambayo kwayo wanadamu huendelezwa hapo duniani. Kuzuia watu wasioe ni kupinga mapenzi na mpango wa Mungu. Kilichoumbwa na Mungu, na kilichoamriwa na Mungu ni chema nacho kipokelewe kwa shukrani. Shetani hawezi kuvitia unajisi chakula wala kuchafua ndoa, mradi tu, watu wavitumie kwa makusudi mema yaliyowekwa na Mungu. Mungu ni Mwumba mwema, na mipango yake ni mema.

Jambo la maana ni shukrani, kwa sababu ni Yeye aliyepanga tuishi kwa kula na wanadamu kuendelezwa kwa kuzaa watoto kwa njia ya watu kuungamanishwa kwa halali katika ndoa. Mambo hayo ni baraka ambazo zinatuhakikishia Wema wa Mungu. Wakristo hushiriki baraka hizo pamoja na watu wengine. Tofauti kati yao na wengine si katika hayo bali ni katika kuwa na maisha ya kiroho kwa kuhuishwa na Mungu. Katika maisha ya kiroho Wakristo hutambua kwamba maisha yao ni zaidi ya chakula na ndoa. Yesu alisema “Wanadamu hawataishi kwa mkate tu” (Mt.4:4) neno “tu” ni la maana katika jibu la Yesu.

Tukumbuke ya kuwa daima Shetani hujitahidi kulishambulia Kanisa na silaha moja kubwa analotumia ni mafundisho ya uongo. Yeye hubadili aina zake, kama mtu anavyobadili mavazi yake, ila kamwe hachoki kuitumia silaha hiyo. Yatupasa kuwa macho na kuwa tayari kumpinga. Neno la Mungu ni msaada wetu.

Paulo alikaza jambo la kumshukuru Mungu kwa vipawa vyake. Ni desturi ya Wakristo kutoa shukrani kabla ya kula, na ni desturi nzuri.

4:6-16 Kupambana na mafundisho ya uongo

k.6 Katika sehemu hiyo Paulo alimshauri Timotheo mwenyewe. Timotheo awe na hali gani anapokabili hatari iliyo mbele ya Kanisa la Efeso? Wajibu wake mkubwa ni kuwaelekeza Wakristo wayashike mafundisho ya kweli na kuyakataa yale yasiyo kweli ili wawe na ufahamu mzuri. Ni juu yake kuwakumbusha, kuwashauri na kuwaonyesha msimamo uliofaa. Ila kwanza yeye mwenyewe apaswa kuyazingatia mafundisho mazuri ili azidi kujijenga na kuwa mzoevu katika imani na mafundisho ya kweli, awe mwalimu, pia awe mwanafunzi. Timotheo alikuwa na baraka kubwa kwa sababu alijifunza Imani kwa Paulo.

Mkristo anayekazana kujifunza kweli za Imani atakuwa na nguvu wala hatanaswa na mafundisho ya uongo.

Vilevile Kanisa lapaswa kuwa na mzigo juu ya mafundisho kwa watu wake ili ikitokea dini nyingine au mafundisho mageni wataweza kuyatambua ndipo kuyakataa. Yapo madanganyo mengi katika eneo la dini. Watu hudanganywa kwa upesi kwa sababu maneno kama “dini” “mungu” huvuta wengi kutega masikio na Shetani ni mwerevu wa kuukamata usikivu wao na kuwadanganya.

k.7 Timotheo na ayakatae mafundisho ya ubatili yasiyomfaidi chochote bali ajitoe kabisa kwa kuyazingatia sana mafundisho ya Injili kusudi ushirikiano wake na Mungu ujengwe, ajizoeze kupata utauwa. Paulo alitumia neno “kujizoeza” akifanya ulinganifu kati ya mazoezi ya kimwili na mazoezi ya kupata utauwa. Alikubali kwamba mazoezi ya kimwili yaweza kufaa kidogo kwa maisha ya sasa ya kimwili, ila mazoezi ya kiroho yafaa zaidi sana kwa maisha ya sasa na zaidi kwa maisha ya baadaye katika uzima wa milele. Katika maisha yetu yapo mengi ya kufanya, tena mengi ni mazuri, ila budi tuchague yale yatakayotufaidi kiroho.

k.9-10 Hapo tunalo “neno la kuaminiwa” ni la tatu katika Waraka huo (1:15; 3:1). Neno hilo la hapa ni nini hasa? Je! maneno yahusu yaliyotangulia au yale yaliyofuata. Kuna kama majibu manne: wengine husema neno lahusu kifungu chote cha 8; wengine wasema lahusu kifungu cha 10: wengine husema ni 10b; na wengine husema ni 8b kuanzia maneno “utauwa hufaa...” Pengine jibu la 8b laelekea kuwa maana yake, kwa sababu k.10 chategemea k.8 na ni sehemu ya 8b iliyo na maana kuliko 8a.

Kwa sababu mazoezi ya kupata utauwa yafaa sana ni vema mtu akazane kabisa katika maisha ya kiroho akijitaabisha na kuwa na bidii ili afaulu kuishika Imani potelea mbali ashambuliwe na mafundisho ya uongo ili amalize mwenendo wake vizuri. Ni vema kukazana kwa sababu ya faida yake kwa maisha ya sasa na ya baadaye. Upo uhusiano mkubwa kati ya maisha ya sasa ya Mkristo na maisha atakayoishi baadaye katika uzima wa milele. Picha ni ya mtu ambaye amekata shauri kabisa kumwekea Mungu tumaini lake lote, hali

akijua hakika Mungu wake yu hai na ni Mwokozi, asili ya baraka zake zote na usalama wake. Hasa Mungu ni Mwokozi wa wale wote wanaomtumaini. Iwapo awapenda wote na kutaka kuwa Mwokozi wao, si wote wanaomkubali, na wote wasiomkubali hawaonji baraka za wokovu. Hamna bahati katika mambo ya kiroho, tupandavyo ndivyo tuvunavyo - bidii nyingi na kujizoeza kwingi huhitajika. Mazoezi hayo si bure!

k.11-15 Paulo alirudia kusema moja kwa moja kwa Timotheo, hali akiyakumbuka mazingara yake pale Efeso. Alitaka awe na nguvu na ujasiri wa kuyaagiza na kuyafundisha mausia na mashauri yake. Mawili hayo ya kufundisha na kuagiza yametajwa mara kwa mara kwa Timotheo na Tito (1:3, 5, 18; 5:7; 6:2b; 2 Tim.2:2; Tito 2:15).

Asiwe mwoga pia asiwajali wale walioudharau ujana wake. Huenda hakuwa kijana hasa ila kwa kulinganisha na wengine alionekana hivyo, na katika jamii nyingi wazee huwa na heshima zao za pekee. Umri wake si kitu, jambo kubwa ni hali yake ya kiroho na uthabiti wake kiimani. Awe kielelezo bora ndipo atawanyamazisha wale waliomsemasema na kumhukumu. Tena awe na busara katika maongezi yake, wala asijiingize katika majadiliano ya wale waalimu wa uongo. Awe na hali nzito akitia maanani mambo. Awe mtu wa kutegemewa, mtu aliyeshinda tamaa zake. Tena azidi wengine katika upendo na imani, na usafi, kusudi apate kuwaoongoza waumini ili hao nao wazikolee hali hizo nzuri. Kwa kielelezo chake awachochee hali hizo katika waumini wa kweli walio tayari kuyazingatia maisha yao ya kiroho.

Hapo twajifunza umuhimu wa sisi wenyewe kutoa kielelezo kizuri ili watu wajifunze kwetu na kusaidiwa.

k.13 Paulo hakutaka Timotheo amsubiri bali aanze kazi hiyo mara moja. Katika huduma hiyo mambo makubwa ni kuyasoma Maandiko wazi mbele za watu, na kuwaonya, yaani kuwasihi walishike Neno la Mungu, tena awafundishe. Bila shaka Paulo aliyakaza hayo kwa sababu ya kuwepo kwa waalimu wa uongo.

k.14 Paulo alimkumbusha juu ya karama aliyopewa alipowekwa kazini zamani, kufuatana na unabii uliotolewa juu yake na wazee (1 Tim.1:18; 2 Tim.1:6). Mawili yametajwa, unabii na kuwekwa mikono, na inaonekana Paulo alishirikiana na wazee katika kumwekea mikono. Ilikuwa juu yake kuitumia karama aliyopewa ili yeye na wengine waifaidi. Kwa hiyo ni wazi kwamba Paulo alimchukua kwa kazi kufuatana na mathibitisho hayo. Katika Mdo.16:2 twasoma “ndugu wa palepale walimshuhudia vizuri” halafu manabii walitoa unabii juu yake, ndipo akawekewa mikono na wazee. Karama yake ilitoka kwa Roho Mtakatifu kwa kusudi la kumwezesha kufanya kazi za Injili. Kwa hiyo Paulo alimkumbusha hayo yote ili asiwe mwoga iwapo kazi mbele yake ni ngumu, ataiweza kwa kipawa alichopewa.

k.15 Yampasa Timotheo awe anatafakari hayo yote daima, adumu kuyazingatia hayo, yawe kama hewa yake, ndipo atazidi kufaulu na kuutimiza wito wake, ndipo watu watautambua ukweli wake na kuona maendeleo yake. Neno hilo la kuendelea lafaa sans watumishi wa Mungu, maana ni rahisi baada ya kuzoea kazi kufanya mradi tu. Twaweza kuendelea na kazi za kuhubiri na kusalisha watu kama kawaida lakini tutafanya bila moyo na bila mzigo, kama desturi tu. Tumo safarini, hatujafika bado, na tumo vitani.

k.16 “Jitunze nafsi yako na mafundisho yako”. Kwa maneno hayo Pauli aliweka pamoja mwalimu na mafundisho yake. Kwanza mwalimu ajiangalie sana na kutunza sana maisha yake, na awe mtiifu katika yale yote ambayo anawafundisha wengine. Pia, ayaangalie sana mafundisho anayotoa. Kama maisha yake ni mazuri hata mafundisho yake yatakuwa mazuri. Kwa watumishi wa Kanisa hayo mawili ni makubwa na yanakwenda pamoja. Ni lazima maisha yetu yasiwe na malawama, pia lazima mafundisho yetu yawe ya kweli ili yote mawili yapate kibali cha Mungu.

Hivyo, mtu mwenyewe ataokolewa, na atakuwa sababu ya wengine kuokolewa pia. Upo usemi unaosema “siwezi kusikia unayosema kwa sababu ya maisha yako kupiga kelele”. Hata Paulo aliogopa kwamba aweza kukataliwa (1 Kor.9:27). Mapasta na wainjilisti husema sana kutokana na kazi zao, kwa hiyo wawe na tahadhari wakijua kwamba iko hatari ya kusema bila kutenda. Paulo alisema hayo yote akilenga jambo lililo muhimu kupita yote, wokovu wa watu.

5:1- 6:2 MARUDI NA WAJIBU

5:1- 2 Marudi kwa vikundi na marika mbalimbali

Vifungu viwili vya kwanza ni kama daraja kati ya 4:11-16 na 5:3ku. Paulo aliendelea kumshauri Timotheo juu ya vikundi mbalimbali katika masharika jinsi ya kuwafanyia wakosaji.

Wa kwanza kutajwa ni wazee, yaani waangalizi wa sharika, watu walioheshimiwa katika jamii ya waumini. Tukumbuke ya kuwa Timotheo alikuwa kijana. Paulo alimwambia asiwakemee bali awaonye kama baba. Kama mzee amekosa hawezi kuachiliwa, eti, ni mzee. Kwa hiyo ni wajibu wa Timotheo kumwonya kwa upole na adabu, maana Timotheo aliachwa pale Efeso kwa kusudi la kuyatengeza shida za pale. Mzee aliyekosa alistahili kuonywa. Vivyo hivyo Timotheo awakabili vijana waliokosa akiwafanyia kama ni ndugu zake wa rika moja naye. Kwa upande wa wanawake wazee awafanye kama ni mama na kuwaonya kwa upole na adabu. Kwa wanawake vijana awafanyie kama ni dada zake ila asijihusianishe nao kwa ukaribu ili yeye na wao wasijaribiwe na kuanguka. Huenda wanawake wakubwa wenye ushuhuda wa maisha mema walitumiwa na Kanisa katika kuwasaidia wanawake vijana (Tito 2:3-5).

5:3-16 Wajane

Paulo alisema mengi kuhusu wajane wa Kikristo. Tangu mwanzo Kanisa lilikuwa na mzigo juu yao (Mdo.6:1ku; Yak.1:27). Kwa sababu Wakristo wengi wa kwanza walikuwa Wayahudi walikubali neno hilo bila shida, maana katika dini ya Kiyahudi walikuwa wamezoea kuwasaidia wenye shida na katika Agano la Kale Mungu aliitwa “Mungu wa wajane”. Yawezekana Paulo alitaja “wajane wa kwelikweli” ili mbeleni aseme kuhusu wajane vijana ambao wengi wao walifanya vibaya. (k.11-15).

Ni wajane gani watakaotunzwa na Kanisa? wote? au vipi? Paulo alitoa mwongozo kwamba ni wale tu wasio na jamaa ambao Kanisa lapasa kuwatunza. Ilitazamiwa kwamba wajane wa kutunzwa na Kanisa wawe wameishi maisha ya utauwa, wakitumia nafasi zao katika maombi, sala, na kutenda matendo mema. Twakumbushwa habari za Ana (Lk.2:26-38).

Ni wajibu wa watoto na wajukuu “kuwalipa” mama na bibi zao, maana ya kulipa ni kuwarudishia ahsante kwa jinsi walivyotunzwa wakati walipokuwa wadogo. Tena Paulo aliongeza kusema kwamba jambo hilo lampendeza Mungu.

k.7 Umuhimu wa habari hiyo unaonyeshwa katika Paulo kumwambia Timotheo ayaagize mambo hayo.

k.8 Alirudia jambo la wajibu wa watoto kutunza mama zao akitoa hukumu kwa wale watakaokosa kuwatunza. Itahesabiwa kuwa wameikana Imani na kuwa wabaya kuliko wale wasio Wakristo.

k.9-10 Orodha iliandika ya wajane wenye umri wa miaka 60 na zaidi ambao pia wameolewa mara moja tu. Pamoja na hayo wawe na sifa za kulea watoto wao vizuri, kukaribisha wageni hasa watumishi wa Kanisa, kusaidia wale walioteswa, yaani wenye shida na wale ambao pengine waume zao waliwasumbua, na wawe wamefanya matendo mema. Wengine wamefikiri kwamba Kanisa lilikuwa na daraja la wanawake wazee waliotumika Kanisani, ila neno hilo si wazi kutokana na vifungu hivi.

k.11-16 Wajane vijana: Paulo alifikiri hao wasiandikwe. Alikuwa na mashaka juu yao akiwaza kwamba baada ya muda hawatatulia bali watatafuta kuolewa tena, hata kuwa tayari kuolewa na wasio Wakristo. Labda ndiyo maana ya k.12 na k.15. Wengine wamekwisha kuteleza, wamekuwa wavivu, wakipenda kutembelea nyumba za watu na kudadisi mambo na kuzungumzia mengi yasiyofaa. Kwa hiyo, afadhali waolewe na kuzaa watoto na kutulia nyumbani. Inawezekana wajane walioandikwa walitakiwa kutoa ahadi au kiapo cha kutokuolewa tena na Paulo hakuona ni vizuri kuwatazamia wajane vijana kufanya hivyo, maana wakibadili mawazo yao baadaye itaonekana kuwa wamevunja ahadi yao kwa Kristo.

Ni dhahiri kwamba Paulo alifikiri kutokuolewa tena kwa mjane ni jambo la sifa sana na heshima kubwa (1 Kor.7:8, 9, 39, 40).

Paulo alitoa mashauri yake kuhusu wajane vijana kwa sababu amekwisha kuona yanavyotokea. Iwapo angalipenda wajane wote wakae walivyo, hata hivyo, aliona ni vema waolewe tena kuliko kuwaka tamaa na kuanguka.

Bila shaka katika mazingara ya pale Efeso na kwa kuwepo kwa waalimu wa uongo ilikuwa rahisi wanawake na wajane vijana wanaswe kwa upesi na kuambukizwa tabia za hao waalimu wa uongo wakipenda kudadisi mambo na kuchochea majadiliano ya bure. (2 Tim.3:6-7).

5:17-20 Wazee/Waangalizi

Hao walikuwa viongozi katika masharika, na bila shaka wengi wao walijitoa kabisa kwa shughuli za kuhubiri na kufundisha. Ila inaonekana baadhi ya waalimu wa uongo walitoka kwao.

Ilikuwa juu ya Timotheo kuona ya kuwa hao wazee wazuri wapate heshima zilizo haki yao. Kazi zao zithaminiwe na hao wenyewe waheshimiwe. Sehemu katika kuheshimiwa kwao ni kule kupewa ujira mzuri. “heshima maradufu” huenda maana yake ni kama hapo juu, wapewe heshima pamoja na kupewa ujira. Pengine kuna wazo kwamba walipiwe kwa ukarimu. Huenda si vizuri kumaanisha kwamba wapewe mshahara maradufu.

Katika k.18 Paulo alilithibitishia wazo hilo kwa kutumia Maandiko, na kuonyesha kwamba hata Yesu Mwenyewe alisema hivi. (1 Kor.9:14; Luk.10:7). Neno hilo lahusu wote waliofanya vizuri kinyume cha wale wazee waliogeuka kuwa waalimu wa uongo.

k.19 Paulo aliendelea kumwongoza Timotheo juu ya wazee waliokosa. Kwanza kabisa asifuate uvumi wala kukubali shtaka mpaka amelihakikishia kwa mashahidi wawili au watatu. Kwa njia hiyo sifa za mtu zitalindwa, na adui za Kanisa watashindwa kuingiza mashtaka ya uongo, na hata wale wenye wivu au wenye sababu zao zingine hawatafaulu kumwangusha mtu.

Timotheo akisikia mashtaka kutoka watu wawili au watatu, ndipo itambudi ayachunguze na kuuhakikishia ukweli wake. Yakionekana ni kweli basi amwonye yule mzee na kumvuta atubu dhambi yake. Mzee anayeendelea katika dhambi yake ni wajibu wa Timotheo kumleta mbele ya jamii ya wazee au waumini wote ili akemewe wazi. Si wazi aletwe mbele ya wazee tu au mbele ya waumini wote. Kwa njia hiyo tumaini lipo kwamba atatambua uzito wa dhambi yake na kuitubu. Hata ikiwa yeye mwenyewe hajirekebishi inawezekana jamii ya waumini wataogopa wakijua kwamba Kanisa linao msimamo wake, wala

halitaruhusu watu wake kufanya wanavyotaka tu. Kanisa likikosa kufanya marudi basi litadhoofu. Kwa jinsi Paulo alivyoandika twaelekezwa kufikiri kwamba tayari walikuwepo wazee waliokuwa wakifanya dhambi.

5:21-25 Timotheo na mwenendo wake

Ndipo Paulo alimwagiza Timotheo kwa uzito sana ayatimize hayo yote aliyomshauri. Maneno “mbele za Mungu, na mbele za Yesu Kristo, na mbele za malaika wateule” yalimkumbusha Timotheo kwamba yeye na wenzake wanafanya hayo niaba ya Mungu na ya kuwa siku moja wao wenyewe watasimama mbele za Mungu na kuhukumiwa. Timotheo alihitaji kutiwa moyo, maana, kwa tabia ya asili hakuwa mjasiri, na hayo aliyoagizwa ni magumu.

Kwa sababu mambo hayo yalikuwa mazito ni lazima asifanye kwa haraka. Kabla ya kuchukua hatua afanye uchunguzi wa kutosha. Pia asifanye kwa upendeleo bali afuate mambo jinsi yalivyo, potelea mbali yeye mwenyewe asikiavyo.

k.22 Itambidi Timotheo aweke mikono wazee wengine badala ya wale waliokosa. Paulo alirudia neno la kutokufanya haraka. Amchunguze mtu kwa muda, auhakikishie mwenendo wake na imani yake. Neno hilo ni la maana kutokana na jinsi wazee wengine wa pale walivyoanguka. Akifanya haraka na kuweka mtu asiyefaa basi atakuwa mshiriki wa dhambi zake. Pamoja na hayo Timotheo awe na tahadhari juu ya maisha yake mwenyewe. Twajifunza kwamba Kanisa lapaswa kuwa na uangalifu sana juu ya hali za watumishi wake na viongozi wake. Mahali pengine neno hilo si rahisi, kwa sababu katika maeneo mapya ambapo Kanisa halijatia mizizi chini ni vigumu kupata watumishi na hasa linapotaka watu wenye kisomo na uwezo kwa kazi zingine. Kanisa lisiogope kufanya marudi kwa viongozi na watumishi wanaokosa, tena wawarudi wakosaji bila upendeleo!!

k.23 Paulo alikumbuka kwamba Timotheo hakuwa na afya nzuri, alisumbiliwa na shida ya tumbo na kuugua mara kwa mara. Basi Paulo alimshauri atumie mvinyo kidogo, maana alikuwa akitumia maji tu. Huenda Timotheo alidhani kwamba si vizuri atumie mvinyo, lazima ajinyime, lakini katika kumkazia awe na maisha safi Paulo hakuona kutumia mvinyo ni kinyume cha maisha safi, mradi tu atumie “kidogo” tu.

k.24-25 Paulo alitoa sababu ya haja ya kuwa na subira katika kuweka wazee wengine. Watu wengine hudhihirisha hali zao kwa upesi lakini sivyo ilivyo kwa wote. Hali halisi ya mtu itajulikana mbeleni. Ni vigumu kuwa na uhakika juu ya watu, kwa hiyo si vizuri kuchagua kwa haraka, wengine huficha hali zao mbaya. Kwa hiyo inawezekana wengine walichaguliwa wasiostahili kuchaguliwa na wengine hawakuchaguliwa iwapo walistahili kuchaguliwa. Iliyopo ni kwamba kazi ya kuchagua wazee ni kazi ngumu, inahitaji busara.

6:1-2 Watumwa

Injili ilipohubiriwa watumwa wengi waliuitika wito wa kumwamini Kristo. Kanisa liliwapokea sawa na wengine kwa kuwabatiza na kuwakaribisha katika mikutano yao bila ubaguzi. Nje ya Kanisa hawakuwa na haki yoyote, walikuwa mali ya mabwana wao, na maisha yao yalitegemea wema wao.

Katika Dola ya Kirumi yadhaniwa kwamba watumwa walizidi milioni sita, wengine wakiwa watu wa elimu mbalimbali, pengine walitekwa vitani n.k. Kwa hiyo katika nyakati zile Kanisa halikufundisha kwamba hao wote waachiliwe, maana fujo nyingi zingalitokea katika jamii. Katika Agano Jipya neno hilo la utumwa halikuzungumzwa, ila twakuta mafundisho jinsi Kanisa ilivyopaswa kuwafanyia, watumwa, na wajibu ulikuwa nini. Haikosi hali zao zilipata nafuu walipokuwa na mabwana walioamini.

k.1 Katika kifungu hicho Paulo alimwongoza Timotheo kuwashauri na kuwaonya watumwa juu ya wajibu wao kwa mabwana wao. Pengine kifungu hicho chasema juu ya mabwana wote, waumini kwa wasioamini. Budi wawaheshimu, na kujitia chini yao, wala wasijaribu kuupindua hali iliyopo ya kuwepo kwa watumwa katika jamii. Zaidi walipaswa kutimiza wajibu wao kikazi kusudi Jina la Mungu lisitukanwe na Injili isipate kudharauliwa. Twaona Paulo alikuwa na mzigo juu ya Ukristo kuwazwa vema kati ya watu. Bila shaka Mitume na viongozi wa Kanisa waliwaza kwamba siku za mbeleni, Injili itakapokuwa imeenea sana na kupokelewa na wengi zaidi ndipo tumaini la kufanya mageuzi na kuuondoa utumwa litapata nguvu.

k.2 Hapo Paulo amewaza wale watumwa waliokuwa na mabwana walioamini. Bila shaka watumwa walijaribiwa wasiwajali kwa sababu sasa wamekuwa ndugu zao katika Kanisa walio sawa nao kwa upande wa imani. Huenda walitafuta mapendeleo mengi kwao. Ila Paulo alifundisha kwamba wafanye kazi zao kwa moyo wakitambua ya kuwa watakaofaidi kazi zao ni ndugu wapendwa katika Kristo.

Hivyo Timotheo alipewa kazi ya kuwafundisha na kuwaonya watumwa mambo hayo. Haikosi watumwa wa Kikristo walipata nafuu katika hali zao kwa mabwana walioamini. Zaidi sana katika Kanisa hamna ubaguzi, na bila shaka jambo hilo liliwatia moyo na kuwarudishia hali ya kujiheshimu.

6:3-21 MASHAURI MBALIMBALI

6:3-5 Waalimu wa uongo

Ndipo Paulo alirudia kusema juu ya waalimu “wagonjwa” na elimu yao “nyingine”. Hao waalimu walikuwa wamemwacha Kristo na mafundisho yenye uzima, mafundisho ya kuleta afya rohoni na akili timamu, ambayo tunda lake ni utauwa.

Kimafundisho wamepotoka na kimaisha wamepotoka, kwa hiyo watatambuaje mafundisho ya uzima? Kiini cha mafundisho ya uzima ni Kristo Mwenyewe, na waalimu wa mafundisho ya uzima wataishi maisha ya kumpendeza Mungu.

Hao waalimu wa uongo walijivuna, walikosa ufahamu, walipenda majadiliano na kudadisidadisi mambo, walichokoza maswali yasiyo na lengo wala kujenga imani. Ni kama walilogwa na hali hizo, na hali hizo zilisababisha ugomvi, wivu, matukano, n.k. Akili zao ziliharibika kwa sababu walikuwa wameondoka katika kweli na kwa sababu hiyo hawakuwa na nanga katika maisha yao, wala kipimo cha kweli kwa mafundisho yao. Kwao mambo ya dini yalikuwa njia ya kupata faida, wakiongozwa na mfuko kuliko moyo. Siku zile waalimu na mafilosofia waliishi kwa kupata riziki kwa kutoza ada wanafunzi wao.

6:6-10 Hatari za mali

k.6 Katika k.5 Paulo alidokezea kwamba wale waalimu wa uongo walidhani utauwa ni njia ya kupata faida. Walikuwa wameondoka katika kweli na kufundisha yasiyofaa kwa ajili ya faida yao wenyewe. Lakini katika k.6 Paulo alikaza jambo la utauwa akisema kwamba utauwa una faida kubwa hasa ukiandama na kuridhika, yaani mtu kuwa radhi na hali na vitu alivyo navyo bila kutafuta kuongeza mali yake. Hapo Paulo alikuwa akiwalenga waalimu wa uongo na choyo yao. Utauwa, yaani ushirikiano mwema na Mungu ndio faida kubwa zaidi ya faida zote zingine.

k.7-8 Maneno ya k.7 ni ukumbusho wa maana sana, na twajua maneno hayo ni kweli kabisa. Paulo alitoa sababu mbili juu ya utauwa pamoja na kuridhika kuwa faida kubwa. Sababu moja ni kwamba hatutaondoka duniani na kitu chochote sawasawa na jinsi tulivyoingia duniani bila chochote, tulizaliwa uchi!!. Kwa sababu tutaacha kila kitu nyuma ni dalili ya mali kuwa si kitu katika maisha yetu ya kiroho na maisha ya baadaye.

Sababu ya pili ni kwamba yatosha tuwe na kifuniko, maana yake nguo au “kibanda” na chakula, mahitaji ya lazima kwa mwanadamu awaye yote. Mafundisho hayo ni ukumbusho wa jinsi Yesu alivyosema katika Luka 12:22-32 na Mt.6:25-34. (Yesu alitoa mafundisho hayo baada ya kusema juu ya choyo Lk.12: 16-21 na Mt.6:24). Utauwa ndio faida kubwa hasa tukiridhika na hali yetu, mradi tu tunayo mahitaji ya lazima. Lakini kinyume chake choyo haina maana wala faida yoyote.

k.9 Bado Paulo alikuwa akiwalenga waalimu wa uongo ila pia maneno yake yahusu yeyote anayetamani kuwa na mali. Ni bure kutumia maisha yetu katika kujitafutia mali tu. Isiwe kitu cha kwanza katika mawazo na maisha yetu, kwa sababu ni ya muda tu, mali pamoja na dunia ni “wasafiri” zitapita. Sisi nasi tu wasafiri, ila tofauti na “wasafiri” hao, sisi twasafiri mpaka mbinguni kwa Mungu. (1.Yoh.2:15ku.).

Ndipo Paulo alieleza matokeo kwa wale wanaojisumbua kuongeza mali. Hao wajiingize kwenye majaribu mengi na kunaswa. Ni kama mtego wa Shetani. Waanza kwa kusikia kuvutwa na mali na kuitamani. Ndipo hiyo tamaa huwashika, halafu wamekuwa tayari kufanya vibaya ili wafaulu lengo lao. Mwishowe mtu hujikuta ametawaliwa na tamaa yake na mali yake, amepata "bwana" mpya, yaani mali, badala ya mali kuwa mtumishi wake.

k.10 Kosa si katika mali yenyewe, kosa ni katika kuipenda. Mtu aliye na mali huwa na wajibu mkubwa wa kuitumia vizuri. Paulo hakusema kwamba mali ni kitu kibaya, ila ni tamaa yake iliyo mbaya. Mali ina hali ya kumfanya mtu asiridhike. Tena mali humdanganya mtu ili afikiri kwamba akiwa nayo atakuwa salama; kumbe usalama wetu ni katika kuwa na uhusiano mwema na Mungu. Shida nyingine ya kutamani mali ni mtu kujiwaza mwenyewe tu. Badala ya mtu kuwa na amani mara nyingi mali humletea masumbufu mengi na mahangaiko. Kwa ajili yake wengine wamefanya vibaya, wengine wameikana imani yao ya Kikristo, na Paulo alitumia lugha ya "kujichoma" maana yake ni kama mtu amejikata kutokana na jitahada za kuipata mali.

Iwapo Paulo alisema hayo yote kwa kulenga hali ya pale Efeso na kuwepo kwa waalimu wa uongo, pia alitaka kumwonya Timotheo ajiangalie na hali yake. Hata hivyo maneno hayo ni onyo kubwa kwetu sisi. Tusimaanishe kwamba Paulo alitaka kukuza hali ya umaskini, au kufundisha kwamba tusiwe na chochote. La! Kitu alichokemea ni kuipenda fedha, na kujitoa kwake, na kuiruhusu ichukue utiifu wetu. Kuwa na mali si vibaya, kuipata kwa njia zilizo halali si vibaya, ila kuwa tayari kufanya lolote mradi tu tuipate, hii ndiyo vibaya.

6:11-16 Mausia kwa Timotheo

Katika Waraka huo mara tatu Paulo aliwakemea waalimu wa uongo (1:3-7; 18-20; 4:1-5), na pamoja na makemeo hayo kila mara aliweka neno kwa Timotheo binafsi (1:3, 18-19; 4:6-16) akimsihi awapinge na yeye mwenyewe aishi maisha mazuri, yaliyo tofauti na maisha yao. Hata hapo alifuata kawaida hiyo. Katika 6:3-10 aliwasemea waalimu wa uongo ndipo akamgeukia Timotheo na kutoa mausia yake ya mwisho.

k.12-14 "maungamo mazuri" maneno hayo yahusu nini hasa? Kwanza yalihusu ahadi zake alipobatizwa. Pamoja na hayo huenda yalihusu wakati alipowekewa mikono na wazee na kuingizwa katika Huduma ya Injili. Hata inawezekana yahusu maagizo hayo ya Paulo katika k.11-12 kwa sababu maneno ya Paulo yalikuwa mazito. Kwa vyovyote ni wazi Paulo alilitoa agizo zito kwa Timotheo la kuilinda vizuri ile amri. Alikaza sana kwa kutumia maneno "mbele za Mungu..na mbele za Yesu Kristo.." Hao ni mashahidi wa agizo hilo la Paulo kwa Timotheo. Pia alimkumbusha kwamba hata Yesu mbele za Pilato alikiri kwa ujasiri Umasihi wake, iwapo katika kufanya hivyo aliweka maisha yake katika hatari kubwa.

Sababu kuu ya kupiga vita na kudumu kuwa waaminifu ni kwamba Kristo atakuja tena, ni tukio moja kubwa ambalo limebaki na ni lengo kuu la historia yote. Mungu kwa nguvu zake na mamlaka yake atamleta tena. Kwa hiyo Timotheo aishi maisha yasiyo na mawaa wala malawama (1 Thes.3:13; 5:23; 1 Kor.1:8; Flp.2:15-16). Awe mshindi katika vita ya imani, akijilinda mwenyewe pamoja na kuilinda Injili aliyokabadhiwa, kisha aikabidhi kwa watu waaminifu. Ndiyo sababu yampasa aangalie sana hali za wale watakaochaguliwa kuwa wahudumu.

k.15-16 Kama ambavyo tumeona mara kwa mara Paulo aliingia katika hali ya shauku akimwadhimisha Mungu sana. Maneno ni kama wimbo wa sifa, labda ni sehemu ya wimbo uliotumika katika ibada. Mungu, peke yake, ni Mwenye uweza wote, hamna mwingine mfano wake. Yeye ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana. Katika Ufu.17:14 na 19:16 Kristo ameitwa hivyo.

Tena Mungu ni Mungu aliye hai milele na milele, hafi wala hapatikani na mauti. Yeye ni asili ya uzima. Pamoja na hayo yote Yeye huwa mbali kabisa katika nuru ambayo hakuna mtu awezaye kusogea karibu na kumwona. Mwishowe alimaliza sifa zake kwa kutaja heshima na uwezo wa Mungu. Kwa njia ya wimbo huu wa sifa Paulo alimkumbusha Timotheo utukufu na ukuu wa Mungu ili katika matatizo na magumu yote ya huduma yake azidi kuwa na uhakika juu ya Mungu wake. Yeye Mungu hategemei kitu chochote, bali Yeye peke yake adumu hali amestahili kupewa heshima zote. Timotheo alizungukwa na dini na imani na mafundisho ya uongo, ambavyo miungu yake haikuwa na nguvu wala uwezo, kwa hiyo azidi kukazana.

6:17-19 Mashauri kwa matajiri

Katika sehemu hiyo Paulo alimwagiza Timotheo juu ya kuwashauri wale ambao tayari walikuwa matajiri, ili wafahamu vizuri jinsi ilivyowapasa kuishi. Bila shaka Wakristo wengine walikuwa na mali, na huenda walizoea kukutana katika nyumba zenye nafasi kubwa za walio matajiri. Twakumbuka Lidia aliyewakaribisha Paulo na wenzake walipofika Filipi akiwatunza vizuri mpaka walipoondoka. Inaonekana yeye alikuwa na biashara nzuri. (Mdo.16:15).

Paulo alimwambia Timotheo asiwalaumu, maana kuwa na mali si kosa. Ila awaagize wasijivune, maana ilikuwa rahisi wajione kwa sababu ya mali yao. Pia wasiweke tumaini lao katika mali zao, kwa sababu mali haina uhakika. Katika siku zetu tumeona ya kuwa neno hilo ni kweli. Thamani ya fedha hubadilishwa bila taarifa; wako wasio waaminifu katika eneo la fedha, hata bank zetu na makumpani; wizi wa bunduki upo na mara kwa mara watu wamekuwa tayari kumnyanganya mtu maisha yake pamoja na mali zake. Kwa hiyo neno hilo la kuweka tumaini letu kwa Mungu si kwa mali ni shauri jema. Tusiweke uzito wetu wote kwa mali au tutafanana na mtu avukaye daraja ambalo mbao zake si imara. Ni faraja kubwa kujua ya kwamba Mungu wetu ni

Mwema na Mkarimu, si Mungu mnyimavu, naye hupenda tufurahie na kuvitumia vipawa vyake kwa shukrani.

Ni juu ya matajiri wenye uwezo wa kufanya mema kuwasaidia wengine wahitaji. Wakifanya hivyo watakuwa wanajiwekea akiba nzuri kwa Mungu na kwa maisha yao ya baadaye. Badala ya kuweka akiba ya fedha waweke akiba ya matendo mema, maana fedha haitawafuata mpaka uzima wa milele, ila matendo mema yatawafuata. Hawatapata hasara. (Mt.6:19).

6:20-21 Neno la mwisho la Paulo kwa Timotheo

Tazama jinsi Paulo alivyoanza neno lake la mwisho kwa Timotheo “Ee Timotheo” maneno ambayo yamejaa upendo. Alimsihi ailinde amani imani ya kweli, ni wajibu wake wa heshima sana. Amana ni hazina ya thamani. Yawezekana amani hiyo si imani ya kweli tu, bali ni yote aliyopewa kufanya katika Waraka huu. Amepewa wajibu wa kuwakataza waalimu wa uongo na mafundisho yao, amepewa wajibu wa kutunza maisha yake yawe safi kabisa na kufundisha mafundisho ya kweli. Ni heshimu kubwa sana kuteuliwa kufanya huduma ya namna hiyo.

Kwa hiyo ilimpasa ajitenge kabisa na waalimu wa uongo, wala asithubutu kamwe kuyafikiria mafundisho yao, wala kushirikiana nao, wala kujadiliana nao. Kwa huzuni kubwa Paulo alifahamu kwamba pale Efeso wengine wamehusisha nao, wakanaswa nao na kuanguka. Neno hilo lilimsikitikisha Paulo sana sana, na ndiyo sababu aliyaandika hayo yote kwa Timotheo, hataki afanane nao.
Paulo aliufunga Waraka kwa baraka, baraka aliyeyozoea kutumia, ya “Neema”. Neno moja la kuona ni kwamba alitumia neno “ninyi” kwa kuonyesha kwamba iwapo barua yake ni kwa Timotheo kibinafsi lakini si yeye tu, bali pia ni kwa waumini wa pale Efeso.

MASWALI KUHUSU WARAKA ZIMA

(Kwa sababu Paulo aliyarudiarudia mambo fulani maswali hayafuati mpango wa sura. Majibu yapatikana katika sura mbalimbali).

1. *Twajifunza nini kutokana na bidii za Paulo katika kulinda Kanisa na mafundisho ya uongo? Je! Katika siku zetu Kanisa lifanye nini ili lihifadhi Injili na kweli zake pamoja na kuzuia mafundisho ya uongo? Je! umetambua mafundisho yoyote ambayo si ya kweli katika Kanisa? Eleza ni mafundisho gani?*

2. *Kuhusu watumishi wa Kanisa ni matayarisho gani yaliyo mazuri, ukikumbuka jinsi Paulo alivyokuwa "baba" wa Timotheo na kumlea vizuri katika Imani?*

   Katika kuwachagua watu wa kufaa ni lazima tuangalie nini?

   Katika orodha ya tabia na hali zilizotajwa na Paulo katika Sura ya 3, waonaje? Tabia hizo bado zinahitajika? Unawaza tabia au sifa zingine ambazo zingefaa kwa mazingara ya leo?

3. *Twaona mara kwa mara Paulo alimwadhimisha Mungu sana, hali akishangaa jinsi Mungu alivyomwokoa na kumweka kuwa Mhudumu. Ni nini itakayowasaidia watumishi wa leo kufanya huduma yao vizuri na kuepukana na hali ya kufanya mradi tu?*

4. *Tumeona Timotheo alishuhudiwa vema na wazee wa pale alipoishi ndipo Paulo akamchukua kwa kazi. Neno moja ambalo Paulo alirudiarudia ni kwa viongozi kushuhudiwa vema na watu wa nje. Waoneje neno hilo? Kwa nini akaze jambo hilo?*

5. *Kuhusu marudi katika Kanisa kwa wahudumu na watumishi wengine Je! Kanisa la leo linafanya marudi? Ikiwa linafanya Je! linafanya vizuri bila kuogopa na bila kupendelea watu? Toa mawazo yako juu ya jambo hilo. Kanisa likiacha kuwarudi watumishi wake litadhoofika. Je! hii ni kweli?*

6. *Hali inayotakiwa katika watumishi ni "utauwa" ili watoe kielelezo chema kwa watu wao? Mtumishi wa Mungu afanye nini ili awe na hali hiyo? Je! unafikiri ni jambo kubwa kuliko elimu na uwezo au siyo? - eleza.*

   Kanisa lifanye nini kupata watumishi wazuri hasa katika sehemu zile mpya na katika madayosi mapya?

7. *Paulo alitoa mashauri kuhusu wajane na watumwa. Je! Kanisa la leo linashauri watu namna ya kufanya kuhusu matatizo ya leo, kwa mfano,*

kwa wale wenye ugonjwa wa ukimwi na jamaa zao. Eleza jinsi unavyoona Kanisa laweza kuwasaidia. Iwapo hatuna watumwa wako wengine wanaodhulumiwa kwa kulipwa mshahara mdogo n.k. Je! mapasta na wainjilisti wanawasaidiaje ili wapate haki zao, hasa ikiwa wanadhulumiwa na Wakristo wenzao?

8. *Kwa sababu kumetokea mageuzi makubwa katika jamii unafikiri mashauri ya Paulo kuhusu wanawake ni mazuri kwa kulingana na hali za kisasa? Eleza.*

9. *Paulo aliona jambo la Ibada na Maombi ni la maana katika Kanisa? Je! upo mkazo wa maombi katika makanisa yetu? Je! kuna vikundi vya maombi? Je! Ibada zinafanyika katika hali ya kumtukuza Mungu? Umeona hali yoyote ambayo unafikiri kwamba haileti uchaji wa Mungu? Katika makanisa mengine kwaya zinatawala ibada, Je! hii ni nzuri? Toa mawazo yako.*

10. *Katika vyuo vya theologia na shule za biblia hatari moja ya kuepa ni hali ya kutafiti mambo yasiyo na maana, utafiti usiolenga kujenga watu kiroho. Unayo mawazo yoyote kuhusu matayarisho ya mapasta na wainjilisti wakati wa kusoma kwao?*

WARAKA WA PILI KWA TIMOTHEO

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Sababu
b) Shabaha
c) Mwandishi

} Tazama utangulizi wa kitabucha 1 kwa Timotheo

d) Tarehe ya kuandikwa
Paulo alikuwa Rumi akitazamia kufa (2 Tim.4:6) naye alitaka Timotheo aje kwake bila kukawia kabla ya wakati wa baridi. (2 Tim.4:21). Tito alikuwa ameondoka Krete na kwenda Dalmatia.

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam za Paulo
3-5 Shukrani
6-14 Paulo amsihi Timotheo awe mwaminifu kati ya magumu mengi
15-18 Waliokosa uaminifu wametajwa pamoja na Onesiforo mwaminifu

2: 1-7 Paulo amsihi Timotheo tena
8-13 Msingi wa ombi la Paulo
14-19 Mashauri juu ya waalimu wa uongo
20-21 Mfano wa vyombo katika nyumba
22-26 Wajibu wa Timotheo kuhusu waalimu wa uongo

3: 1-9 Maovu yanayokuja
10-17 Kwa mara nyingine Paulo amsihi Timotheo

4: 1-5 Agizo la mwisho la Paulo kwa Timotheo
6-8 Ushuhuda wa mwisho wa Paulo
9-18 Maagizo na maneno ya kibinafsi ya Paulo
19-22 Salaam za mwisho.

UTANGULIZI

Paulo alikuwa mzee, alikuwa ametumika katika Injili kwa muda mrefu kama miaka thelathini hivi. Alipomwandikia Timotheo Waraka huu wa Pili alikuwa amefungwa huko Rumi, akitaabika sana katika gereza mbaya, pengine katika chumba cha baridi na unyevu, hali amefungwa na minyororo. Hakutumaini kwamba atafunguliwa. Bila shaka alisikia upweke na kukosa habari za makanisa.

Kwa kusoma Waraka huo wa pili twaona kwamba alihesabu siku zake za kuishi duniani zimekaribia mwisho. Alisema “mwenendo nimeumaliza” (4:7). Jambo muhimu ni kuhakikisha kwamba Imani ya kweli ikabidhiwe kwa kizazi kifuatacho, hali Injili halisi ilindwe kwa ajili yao. Kwa vyovyote Injili ihifadhiwe, na iwekwe kwa watu waaminifu watakaoifundisha kwa wengine (2:2). Ndiyo sababu kwa mara nne Paulo alimwambia Timotheo “bali wewe” lazima Timotheo awe tofauti na wale waalimu wa uongo.

Waraka huo wa pili ni barua kweli ya Paulo. Katika Nyaraka tatu za Kiuchungaji Paulo ameanza kwa kujitaja. Pia alitaja kuongoka kwake na kuitwa kwake kuwa Mtume, pamoja na kutaja mateso yake kwa ajili ya Injili. Katika Waraka huo wa pili alisema na Timotheo kwa moyo wa ndani kabisa.

1:8 Paulo alikuwa kifungoni, lakini si katika nyumba iliyopangwa kama mara ya kwanza alipofungwa (Mdo.28:16,30). Onesiforo alipata shida sana alipotafuta kujua mahali alipofungwa (1:17) na alitaja mnyororo wake (1:16; 2:9). Alitamani sana kuonana na watu mbalimbali (4:9-13). Kesi yake ilikuwa imeanza, bila shaka utangulizi wa kunyosha mashtaka n.k.na alitazamia kwamba kesi yenyewe itasikika karibuni hivi (4:16,17; 6-8).

(KIPENGELE: Safari za Paulo kati ya kufungwa mara ya kwanza na kukamatwa tena: Inaonekana alikwenda Krete na kumwacha Tito pale (Tito.1:5) ndipo akaenda Efeso na kumwacha Timotheo pale (1 Tim.1:3-4). Yawezekana alikwenda Kolosai ili amwone Filemoni (Fil.22) maana alikusudia kufanya hivyo. Ndipo akafika Makedonia (1 Tim.1:3). Mji mmoja wa Makedonia aliotembea ni Filipi (Flp. 2:24) Alikuwa Makedonia alipomwandikia Timotheo Waraka wa kwanza na Tito Waraka wake. Alimjulisha Tito nia yake ya kushinda Nikapoli wakati wa baridi, mji penye pwani ya magharibi ya Uyunani.(Tit.3:12). Kwa hiyo, inaonekana yeye na Tito walikutana pale. Ikiwa Paulo alifaulu kufika Spania kama alivyotamani kufanya inawezekana alifanya safari hiyo wakati huo (Rumi 15:24, 28).

Alikuwa amemwahidi Timotheo atakuja Efeso kumwona, na inafikiriwa ndivyo alivyofanya (1 Tim.3:14,15) na baada ya hapo akaenda Mileto uliokuwa karibu, hapo ilimbidi amwache Trofimo hali hawezi (2 Tim.4:20). Ndipo huenda

akaenda Troa na kukaa na Karpo, ambapo aliacha vitabu kadha na joho lake. (2 Tim.4:13). Akaenda Korintho, hapo Erasto akamwacha (2 Tim. 4:20 ling. na Ru.16:23) ndipo akaenda Rumi. Njiani akakamatwa tena. Je! alikamatwa pale Troa? na ndiyo sababu akakosa kuchukua joho na vitabu vyake. Au labda alikamatwa alipofika Rumi? Hatujui. Wakati huo Mateso makali ya Kaisari Nero yalikuwa yameanza kama BK.64. Mapokeo husema kwamba Paulo aliuawa kwa kukatwa kichwa (kifo cha walio na uraia wa Kirumi) na wakati huohuo Petro naye aliuawa kwa kusulubiwa).

Paulo alishuhudia kwamba hakuna mwingine kama Timotheo, kwa kuwa walikuwa wametumika bega kwa bega, kama baba na mwana, katika kuieneza Injili. Sasa kwa kuwa wakati wa kufa kwake umekaribia Paulo alitaka kutilia mkazo wajibu wa Timotheo kuhusu Injili. Lazima ailinde amana (1:14) awe tayari kuteswa kwa ajili yake (2:3,8,9) adumu mwaminifu kwake (3:13-14) na aihubiri (4:1-2).

UFAFANUZI

1:1-2 Salaam za Paulo

Paulo alianza Waraka huo kwa salaam zilizo kawaida yake, nazo zafanana na zile za Waraka wa kwanza, ila pia ziko tofauti ndogondogo.

Kwa nini Paulo ataje tena Utume wake na asili yake katika mapenzi ya Mungu? maana Timotheo alijua jambo hilo. Ni kwa sababu katika Waraka huo Paulo alikuwa akikikaribia kifo chake, kwa hiyo alikusudia kumsihi sana sana Timotheo awe mwaminifu kwake na kwa Injili aliyoihubiri.

“kwa ajili ya ahadi ya uzima ulio katika Kristo Yesu”. Paulo alitumwa kuhubiri Injili ya uzima, Injili ya habari njema kwa wenye dhambi walio chini ya adhabu ya mauti. Katika Yesu Kristo Mungu ameahidi uzima wa milele (k.10: Yoh.14:6; Gal. 2:20; 1 Yoh.5:12). Bila shaka Paulo alikuwa akiwaza sana uzima wa milele katika hali yake ya kutazamia kuuawa. Iwapo huo uzima ni kwa baadaye, hata hivyo wahusu wakati wa sasa kwa wote wanaompokea Kristo aliye huo uzima (1 Yoh.5:12).

Paulo alimwita Timotheo “mwanangu mpendwa” tofauti kidogo na 1 Tim.1:2 (1Kor.4:17). Waraka huo ni kwa Timotheo mwenyewe. Katika wajoli wake wote Timotheo alikuwa karibu naye zaidi (Flp.2:20-22). Pengine ni Paulo aliyemleta Timotheo kwa Yesu alipohubiri Injili pale Listra (Mdo.14:8ku.) ndipo alipofika tena pale Listra akamchukua kufanya kazi pamoja naye (Mdo.16:12) akishuhudiwa vema na waumini wa pale.

1:3-5 Shukrani

Katika shukrani zake Paulo alikiri ya kuwa Mungu aliyemwabudu ni Mungu wa baba zake, yuleyule aliyemwabudu alipokuwa Myahudi kabla ya kuwa Mkristo. Ni Mungu wa baba zake ambaye pia ni Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, hivyo Ukristo una mizizi kihistoria katika dini ya Kiyahudi.

Daima alimwombea Timotheo, akimshukuru Mungu kwa ajili yake. Ilikuwa desturi yake kukumbuka sharika za Kikristo pamoja na waumini wake akiwaombea (Rum.1:9; Flp.1:3, Kol.1:3). Alikumbuka nini kuhusu Timotheo? Alikumbuka machozi yake. Yawezekana Timotheo alilia alipoachwa kufanya kazi ngumu pale Efeso (1 Tim.1:3). Katika dhiki nyingi za gerezani Paulo alimkumbuka Timotheo sana sana na kutamani kumwona tena.

Kitu kingine alichokumbuka Paulo ni imani ya Timotheo, alikuwa mtu wa kweli na mwaminifu kwake na kwa Injili. Paulo aliwataja bibi yake Loisi na mama yake Eunike ambao wote wawili walimwamini Kristo na kumlea Timotheo katika imani hiyo. Walimfundisha Maandiko (Mdo.16:1; 2 Tim.3:15).

Waraka huo umejaa mambo ya kibinafsi, majina ya watu yametajwa, watu zaidi ya ishirini.

Twajifunza jinsi ilivyo baraka kubwa kulelewa katika nyumba ya Kikristo, kufundishwa Maandiko tangu utoto, na umuhimu wa maombi. Tena twajifunza umuhimu wa kuwatunza waumini wapya. Paulo alimtunza Timotheo vizuri akimzoeza kazi kwa kumchukua pamoja naye, halafu kumtuma kwa makanisa ili ayatengeneze shida mbalimbali.

Je! katika maombi yako unakumbuka watu kwa majina na kwa kutaja mazingira yao na mahitaji yao?

1:6-14 Paulo amsihi Timotheo awe mwaminifu kati ya magumu mengi

Kwa sababu Paulo aliamini kwamba imani ya Timotheo ni ya kweli aliendelea kumkumbusha juu ya Mungu kumjalia karama ya kumwezesha kuitimiza huduma yake na wajibu zake mzito. Hana haja ya karama nyingine au karama mpya, ila iliyopo ni kuichochea ile aliyo nayo. Paulo hakuwa na maana kwamba alikuwa amepoa, la!. Mkristo yeyote apaswa kufanya hivyo mara kwa mara.

Karama yake si uwezo fulani wa kibinafsi bali ni kipawa alichopewa na Roho Mtakatifu, nacho kilikaa ndani yake. Alipewa wakati alipoingizwa katika huduma kwa kuwekwa mikono na Paulo na wazee. Ni faraja kubwa kujua kwamba tunapoitwa na Mungu kwa huduma fulani Mungu hutuwezesha. Katika 1Tim.4:14 unabii ulitolewa juu yake, na bila shaka ni unabii huo uliomwongoza Paulo na wazee kumwekea mikono na kumwingiza katika Huduma ya Injili.

Kwa hiyo twaona ya kuwa Mungu alikuwa amemtayarisha Timotheo kwa huduma, kwanza kwa njia ya malezi ya nyumbani, halafu kwa utunzaji wa Paulo na wengine, halafu kwa kujaliwa karama iliyotoka kwa Mungu Mwenyewe kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kwa kusema hayo Paulo alitaka kumtia moyo ili asifikiri hali yake ya kimwili ya kuuguaugua, wala hali yake ya ujana, wala tabia yake ya kusikia haya na kuogopaogopa. Ajipe moyo kwa sababu ni dhahiri kwake na kwa wote kwamba Mungu alikuwa amemwita na kumtumia na ataendelea kumwezesha na kumtumia.

k.7 Pamoja na kumkumbusha Timotheo juu ya karama aliyopewa alimkumbusha pia juu ya Roho Mtakatifu aliyepewa alipoamini. Kwa Roho alipewa nguvu, kwa hiyo hakuwa na haja ya kuogopa. Pia alipewa upendo ili awe tayari kunyenyekea na kuwatumikia watu, na moyo wa kiasi ili ajitawale na kufanya kazi kwa utaratibu na adabu na heshima.

k.8 Ndipo Paulo alimwambia Timotheo “usiuonee haya ushuhuda wa Bwana” na “usinionee haya mimi mfungwa wake”. Hata Bwana Yesu alitaja habari ya kumwonea haya. (Mko 8:38). Inaonekana Paulo alikuwa amekata shauri kabisa huhusu jambo hilo (Rum.1:16). Si rahisi kusimama imara tunaposikia dhihaka za watu na kuona Injili inadharauliwa na Yesu na Msalaba wake kuhesabiwa duni; eti! mtu aliyekufa katika udhaifu na aibu ya kuwa uchi, chini ya laana, kama mhalifu wa hali ya juu, awezaye kutuokoa? Fumbo kubwa! (1 Kor.1:23ku.)

Basi Paulo alimshauri Timotheo kuyakataa mawazo ya kuona haya yakizuka ndani yake. Tusifikiri hayo yametokea ila Paulo alimtayarisha Timotheo awe tayari kupambana na mawazo kama hayo.

Kwanza asiuonee haya ushuhuda wa Bwana, yaani Timotheo awe mjasiri katika kumshuhudia Kristo na kutangaza habari zake. Pili usinionee haya, yaani Timotheo asiwe na haya kwa sababu Paulo yu kifungoni na wengine walikuwa tayari kumwacha, hata wengine katika Asia walimwacha (k.15; 2 Tim.4:16). Dema mmoja wa wale waliofuatana na Paulo kwa muda mrefu (Kol.4:14) alimwacha baadaye (4:10). Lazima Timotheo awe macho ili asivutwe au kushawishiwa na wengine.

Paulo alijiita “mfungwa wa Bwana” (Ef.3:1), hakufungwa kwa sababu ya makosa bali kwa ajili ya Kristo na Injili yake, kwa hiyo alisema kwamba ni mapenzi ya Mungu.

Timotheo naye alifungamana na Paulo katika neno hilo la kuteswa, ilimpasa azishiriki taabu ya kuwa mhudumu wa Injili (2:3). Pia wamefungamana na Bwana Yesu aliyeteswa vibaya sana na kuuawa kwa kutundikwa mtini. Neno hilo la kuhusu taabu na mateso linarudiwarudiwa katika Agano Jipya. Ila Timotheo haitwi kuvumilia magumu katika nguvu zake mwenyewe, Mungu

atamjalia nguvu ili ayastahimili yote yatakayompata. Kwa ujuzi wake wa kibinafsi Paulo alikuwa amezionja nguvu za Mungu katika magumu mengi yaliyompata, na Timotheo atazijua kwa kadiri atakavyoshiriki taabu za Injili, pamoja na wote watakaofuata katika nyayo zao.

k.9-10 Paulo aliendelea kwa kueleza mambo makuu yaliyomo katika Injili. Kwa nini Timotheo asiionee haya? Kwa nini awe tayari kushiriki taabu za kuwa mhubiri wake? Ni kwa sababu Injili ni Injili ya Wokovu, kwa njia yake Mungu ametuokoa. Ni habari njema ya matendo makuu ya Mungu yaliyofanyika kwa njia ya Yesu Kristo, aliyefanya yote yaliyotakiwa kwa kuwaokoa wenye dhambi. Katika Kristo tumeokolewa kwa neema na wito wa Mungu. Paulo alikuwa ameipigania Injili hiyo tangu mwanzo wa Huduma yake, tukikumbuka msimamo wake katika Waraka wake kwa Wagalatia na sasa anapokaribia mwisho wa maisha yake bado angali akiipigania hata yu tayari kufa kwa ajili yake. Katika miaka yote tangu mwanzo hata wakati ule hakuibadili au kuinyoshanyosha kusudi aepukane na mateso. Ipo Injili hiyo moja tu iliyo Injili ya Wokovu. Hatuna ruksa ya kuibadili kufuatana na hali ya hewa ya vizazi mbalimbali, ila kila kizazi kinawajibika kuieleza kwa mazingara ya wakati wake ili ieleweke vema.

Kwa neema yake tumeokolewa na maisha ya dhambi ili tuishi maisha matakatifu kwa sababu Yeye anayetuita na kutuokoa ni Mtakatifu (1 Kor.1:2; 1 Thes.4:7). Jambo hilo halina msingi katika matendo yetu bali katika mapenzi ya Mungu (Tito 3:5; Rum.8:28; 9:11; Ef.1:11). Neema ni bure wala hatuistahili. Katika k.9 na k.10 “wokovu” unaotajwa ni wokovu gani? Ni zaidi ya kusamehewa dhambi. Mungu alipotuokoa alituita kwa maisha matakatifu. Pamoja na kusamehewa dhambi na kuitwa kuishi maisha matakatifu kuna uzima na kutokuharibika. Mungu hutuhesabia haki, na kututakasa siku hadi siku ili tufanane na Mwana wake (2 Kor.3:16-18) ndipo mwishowe tutafika mbinguni na kupewa miili mipya katika ulimwengu mpya na kuwa kama Kristo (Rum.8:14-17). Katika Ebr.2:3 twakuta maneno “wokovu mkuu”.

Wokovu mkuu wa namna hiyo umetoka wapi? Si kwetu kwa matendo yetu, la! Asili yake ni katika umilele, kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu na kabla ya kuwepo kwa wakati na mahali. Ni fumbo kubwa kwa sisi wanadamu, wala haielezeki, hata hivyo, kwa wote waliookolewa ni neno la faraja kubwa tukijua usalaam wetu ni katika mapenzi ya Mungu. Vilevile neno hilo latunyenyekeza sana na kutufanya kuwa na shukrani nyingi.

Kiutendaji na kihistoria wokovu umejengwa juu ya matendo makuu aliyofanya Yesu Kristo alipofanyika mwili na kuja duniani kwa mara ya kwanza. Iwapo tulipewa neema katika Kristo tangu milele imedhihirishwa katika Kuja Kwake. Kuhusu jambo la kutupalia wokovu ni jambo lililopangwa katika umilele na kwa siri. Kule kudhihirishwa ni jambo lililofanyika katika historia na kwa wazi.

Alipokuja duniani Kristo alifanyaje? Kwanza alibatili mauti, na pili alifunua uzima na kutokuharibika. Kuna mauti aina tatu (1) mauti ya kimwili ya kutengana mwili na roho. (2) mauti ya kiroho, utengano wa roho na Mungu na (3) mauti ya milele, utengano wa roho na mwili na Mungu kwa milele. Hizo aina tatu ni matokeo ya dhambi.

Alipotokea mara ya kanza Yesu aliibatili mauti, maana yake, alifanya mauti isiwe na nguvu, iwe bure, mfano wa nge kukosa uma lake (1 Kor.15:55). Mauti haina madhara kwa Wakristo.
Kwa hiyo si ajabu Paulo hakuionea haya Injili ya Wokovu (Rum.1:16). Si ajabu aliona ni heshima kubwa kuwa mhubiri wa Injili ya namna hiyo. Wala si ajabu Paulo alikuwa tayari kuteswa hata kuuawa kwa ajili yake. Makusudi ya Paulo ya kumwelezea Timotheo hayo yalikuwa kumfanya Timotheo asiionee haya hiyo Injili, wala asimwonee hayo mhubiri wake Paulo ambaye amefungwa minyororo kwa ajili yake, ili awe tayari kuzishiriki taabu sawa na “baba” yake katika Imani.

k.11-12 Paulo alishuhudia tena jinsi alivyoitwa kuwa mhubiri, na mtume, na mwalimu wa Injili. Timotheo hakuwa na haja ya kuambiwa hayo, ila ni kwamba kila alipowaza uzuri wa Injili Paulo alishikwa na shauku akikumbuka jinsi Mungu alivyomkubali na kumweka kuwa mtumishi wake. Hakuona shida yoyote juu ya mateso na dhiki zake, kinyume chake alizifurahia, kwa sababu alimjua na kumwamini Kristo kabisa na kuwa na hakika kwamba hayo yote hayakuwa bure (2 Kor.4: 17-18). Yote ni salama mikononi mwa Yesu na hakuona hofu juu ya siku ya hukumu ya kuipima kazi yake.

Ni wajibu wetu baada ya kumpokea Kristo kumtangaza kwa wengine. Ni wajibu wetu kuyavumilia mateso kwa ajili yake. (Gal.5:11; 6:12; 1 Thes.3:3; Mdo.14:22). Ni wajibu wetu kuilinda Injili. Kwa kumwandikia hayo yote Paulo alilenga kumtia Timotheo nguvu ili yeye naye asisikie haya juu ya Injili wala juu ya Paulo na mnyororo wake. Awe tayari kupambana na magumu yote kwa ajili ya Injili. Bila shaka daima Paulo alimkumbuka Bwana Yesu na jinsi alivyoaibishwa mno alipotundikwa mtini hali yu uchi, huku akiidharau aibu (Ebr.12:2-3).

k.13-14 Paulo hakusahau kwamba Timotheo amezungukwa na wale waalimu wa uongo, kwa hiyo neno lake kwa Timotheo ni kufuata kielelezo chake na kushika mafundisho ya kweli ambayo aliyaita “maneno ya uzima” na “ile amana nzuri”, njia mbili za kueleza Injili. Injili ni maneno ya afya na ni hazina. Ni mwongozo kwa Timotheo, budi aufuate. Tena yampasa ashike kwa imani na upendo ulio katika Yesu Kristo. Wengine huipigania Injili kwa ukali na kwa fitina na kwa kukosa upendo, wakisababisha uadui na uchungu. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu Timotheo apambane na waalimu wa uongo akishikilia kabisa mafundisho aliyoyapata kwa Paulo. Mafundisho hayo ni hazina, ni ya thamani

sana, lazima ilindwe. Timotheo awe macho kusudi mafundisho hayo yasipotoshwe.

k.15-18 Paulo alikuwa na sababu kubwa ya kumsihi Timotheo, maana alipokamatwa sehemu za Asia wengi walimwacha wakiongozwa na Figelo na Hermogene. Paulo alikuwa amefanya kazi Efeso kwa miaka miwili na zaidi, na wengi walimwamini Kristo (Mdo.19:10). Alipokamatwa yawezekana walidhani kuwa Ukristo utapoa, kwa sababu walihesabu Paulo ndiyo nguzo. Bila shaka habari hiyo ilimhuzunisha Paulo sana.

k.16 Lakini mmoja alisimama imara, jina lake Onesiforo, wala hakumwonea haya wala mnyororo wake. Wakati alipokuwa Rumi alimtafutatafuta kwa bidii, akampata. Inaonekana Paulo alifungwa katika chumba si katika gereza, kwa hiyo ilikuwa vigumu kumpata. Paulo aliburudishwa sana sana kwa kumwona. Bila shaka Onesiforo alimhudumia kwa mahitaji ya kimwili na kumpasha habari za makanisa na wakristo mbalimbali. Jambo kubwa alikuwa tayari kushirikiana na Paulo, hakumonea haya. Paulo aliwaombea watu wa nyumbani mwa Onesiforo ili Bwana awarehemu. Wengine hudhani kwamba kwa maneno hayo na maneno ya k.18 Onesiforo alikuwa amefariki dunia, ila si lazima tufikiri hivyo. Huenda familia yake ilikuwa imebaki pale Asia. Hata kabla ya kumhudumia Paulo huko Rumi Onesiforo alikuwa amemhudumia pale Efeso. Onesiforo alikuwa kielelezo chema kwa Timotheo kwa jinsi alivyoonyesha upendo wake kwa Paulo akiwa tayari kushirikiana naye bila kuona haya.

2:1-7 Paulo amsihi Timotheo tena

Mwisho wa sura ya kwanza Paulo alitaja habari ya wengi katika Asia kumwacha (1:15) ila wachache kama Onesiforo walidumu waaminifu kwake. Kwa hiyo Paulo alianza sura ya pili akimsihi Timotheo kwa maneno “basi wewe, mwanangu, uwe hodari”. Katika wengi kukengeuka yeye asimame imara. Nguvu ya kufanya hivyo ni neema atakayopata kwa Bwana Yesu. Amruhusu Mungu kumtia nguvu siku hadi siku anapokabili shida za pale Efeso.

k.2 Lakini kiutendaje afanye nini? Achukue hatua zipi? Paulo amekwisha kumwambia kushikilia sana Imani ya kweli na kuilinda Injili kama hazina ya thamani sana. Lakini pamoja na kuishikilia na kuilinda jambo moja jingine la maana sana ni kuikabidhi kwa wengine na kwa kizazi kifuatacho.Ni muhimu sana afanye hivyo. Karibuni hivi Paulo alitazamia kwamba atauawa, kwa hiyo, itakuwa juu ya Timotheo na wengine kama yeye kuilinda na kuikabidhi wengine. Tena Paulo alikuwa akimtaka Timotheo aje kwake Rumi mapema iwezekanavyo, basi pale Efeso apate wengine walio waaminifu ili waipokea hazina ya mafundisho ya uzima, watu ambao wataweza kuwafundisha wengine. Mafundisho hayo hayakuwa ya siri, ya watu wachache, bali ni kwa watu wote.

Timotheo awakabidhi watu gani? Kwanza, watu waaminifu, watu ambao hawakudanganywa wala kushawishiwa na waalimu wa uongo. Pia watu ambao hawakukengeuka waliposikia kwamba Paulo amekamatwa na kufungwa. Pili wawe watu “watakaofaa kuwafundisha na wengine” watu wenye kipawa cha ufundishaji, waliokuwa na ufahamu mzuri wa mafundisho ya kweli na kuishi kwa kuyafuata. Bila shaka baadhi ya wazee wa pale Efeso walifaa (1 Tim.3:2).

Hivyo twaona hatua zilizopo katika kupokezana kwa Imani ya kweli, Imani ya KiMitume. Kutoka Kristo mpaka Mitume, Paulo akihesabiwa kuwa mmoja wao; ndipo kutoka Mitume hasa Paulo mpaka Timotheo, Tito, na wengine kama hao; halafu kutoka Timotheo mpaka watu waaminifu, na kutoka hao waaminifu mpaka wale watakaofundishwa nao. Sasa amana hiyo, au mafundisho hayo ya uzima, yaani Injili hupatikana katika Agano Jipya. Wajibu wa Kanisa ni kufundisha kweli zilizomo katika Agano Jipya. Kwa hiyo, Timotheo awe hodari, achote sana katika neema ya Kristo ili asimame imara na kuchukua zile hatua za kuwakabidhi wengine Imani ya kweli. Ni dhahiri kwamba si wote waliokengeuka, wala si wote walionaswa na elimu ya uongo.

k.3-7 Ndipo Paulo alimpa Timotheo mifano mitatu ya wafanya kazi mbalimbali ili ajifunze kwao tabia za kumsaidia katika kazi yake. Mmoja ni askari, mwingine ni mshindani mbio na wa tatu ni mkulima.

Alitaja tena habari ya “kushiriki taabu” kama askari aendaye vitani, kwa sababu yeye pia ni “askari” askari wa kupiga vita ya Yesu Kristo na Injili yake. Paulo alipenda kutumia mfano wa vita (2 Kor.10:3-5; Efe.6:10-17) Flm.2). Askari ni chini ya amri ya Jemadari au mkuu wake, apaswa utii na kuwa mtiifu kwake. Askari hujitoa kabisa ili ampendeze bwana wake na kwa sababu hiyo madai ya mkuu wake huwekwa kabla ya madai ya familia au shughuli zingine. Yesu alisema “tafuta kwanza ufalme wake” (Mt.6:33). Mkristo aitwa kuachana na kitu chochote kinachomzuia asipige vita ya imani vizuri.

Askari hutazamia kwamba atapatwa na maumivu na jeraha katika vita na adui. Vivyo hivyo Mkristo hawezi kuepa mateso na dhiki anapopiga vita ya imani. Madai ya Kristo huzidi madai yote ya maisha yetu. Askari hutilia maanani utumishi wake, yu macho wakati wote ili asinaswe na shughuli zingine. Siyo maana kwamba Mkristo aache shughuli zote za dunia hii, la!. Atimize wajibu zake za nyumbani, na kazini n.k. Hakatazwi hizo (1 Tim.4:6;17) ila asifuate mengine ambayo si mabaya, ili si msaada katika maisha ya Kikristo.

k.5 Halafu Paulo alileta mfano wa mshindani mbio. Kwa huyo ajifunze nini? Mshindani mbio apaswa kufuata sheria za mchezo wake. Tena mshindani mbio hukazana kabisa kupata taji akifanya jitahada na mazoezi mengi kusudi afaulu. Michezo ya Olympiki ilifanyika kila miaka kumi katika Jimbo la Uyunani. Kila mchezaji alidaiwa kutoa ahadi kwamba atafanya mazoezi ya miezi 10 kabla ya

Michezo yenyewe kusudi Michezo iwe nzuri. Washindaji hawashindi kwa bahati tu, bali kwa kujitayarisha kwa muda mrefu kabla. Lazima ajitawala na kujizuia katika mengi. Tena ashindane kwa halali. “kwa halali” maana yake ni nini kwa Mkristo? Ina maana kwamba Mkristo apige vita ya Kikristo kwa kufuata kielelezo na mafundisho ya Yesu na kwa kuzishiriki mateso yake.

k.6 Paulo aliendelea kwa kutoa mfano wa mkulima. Mkulima hufanya kazi za kujichosha, na kwa bidii, bila kuona matunda yake mara, lazima angoje mpaka baadaye kwa mavuno. Vivyo hivyo mtumishi wa Kristo budi afanye kazi kwa bidii na kwa taaba pamoja na subira ya kungojea matokeo yake. Asiwe mvivu wala asikate tamaa, avumilie hadi malipo ya Bwana siku ya mwisho. Shughuli zake zitakuwa maombi, na huduma ya Neno la Mungu, na kuchunga watu wa Mungu na kuwatafutia wengine.

Hao wote watatu, askari, mshindani mbio, na mkulima hutazamia thawabu. Askari hutazamia ushindi wa vita, mpiga mbio hutazamia tuzo kwa kufaulu ule mbio na mkulima hutazamia kushiriki katika “mavuno”. Askari asiyejitia kabisa katika vita hawezi kushinda, wala mshindani mbio hatapata tuzo asiposhika sheria za michezo yake, na mavuno hayatakuwepo bila mkulima kujichosha katika kulima kwake. Kwa hiyo Timotheo ajitoe kabisa kushindana na adui za Injili, akishindana nao kwa uhalali, na kwa kukubali dhiki, na kufanya kwa bidii.

k.7 Paulo alimwambia Timotheo ayazingatie hayo na kutafakari sana hiyo mifano mitatu, na Yesu atamwelewesha zaidi. Twajifunza kwamba ni wajibu wetu kutafakari Neno la Mungu, haitoshi kusema “Bwana atanielewesha”, sisi tunayo sehemu yetu katika kuelewa. Kwa upande wa pili iwapo tutazingatia sana Maandiko mwishowe ni Bwana atakayetusaidia kuyaelewa. Yote mawili yatakiwa, kuwa na bidii katika kusoma na kutafakari Neno la Mungu na unyenyekevu wa kuomba ufunuo wa Mungu juu yake.

2:8-13 Msingi wa Ombi la Paulo

k.8-10 Kwa mifano mitatu Paulo alionyesha kwamba askari, mshindani mbio na mkulima wapata matokeo mazuri kwa sababu ya bidii na taabu zao za kazi. Katika k.8-10 amethibitishia neno hilo kwa kumtaja Bwana Yesu (k8) na yeye mwenyewe (k9) na mateso yake halafu katika k.11-13 alitaja waumini wote.

k.8: “Mkumbuke Yesu Kristo” aliyejitoa kabisa maisha yake yote, alitumika bila kujihurumia, na Kufa Kwake msalabani kulikuwa “upeo” wa kujitoa kwake. Timotheo atakapomkumbuka Bwana Yesu atatiwa nguvu kuvumilia yote yaliyo mbele yake hasa akijua kwamba Yesu yu hai baada ya Kufa na ya kuwa alipewa Jina lipitalo kila jina kwa sababu ya kunyenyekea kwake. Kwa nini Paulo alisema “wa uzao wa Daudi” (Rum.1:3-4) Ili Timotheo asimwaze Yesu kuwa tofauti na yeye, Yesu alikuwa mwanadamu sawa na sisi akijaribiwa kwa kweli, akisikia kwa kweli maumivu na huzuni n.k.(Eb.2:14-18; 5:7-9) Tena Yesu

Kristo ni timizo la kazi ya Mungu katika historia ya wanadamu, kwa hiyo ni wazi kwamba makusudi ya Mungu yataendelea kutimizwa kwa njia ya shughuli za Injili hata ikwa wapinzani watajitahidi kuyazuia.

k.9-10 Ndipo Paulo alijitaja. Timotheo alifahamu taabu na mateso ya Paulo, lakini Paulo alitaka Timotheo atambue mambo mawili. Kwanza Neno la Mungu halifungwi iwapo mhubiri wake amefungwa, wengine wataendelea kulihubiri, na hata pale gerezani Neno lahubiriwa kwa sababu watu watajua kwamba Paulo hakufungwa kwa kosa lolote lingine isipokuwa kwa kuhubiri Injili. Bila shaka wengi walizungumzia habari zake wakiulizana Injili ni nini hata mtu huwa tayari kufa kwa ajili yake (Flp.1:12-14).

Pili, ni kwa sababu alitaka watu waokolewe, wale waliokusudiwa na Mungu watapata kusikia Habari Njema na kumwamini Kristo. Paulo alijua kwa hakika kwamba mapenzi ya Mungu ni kwa watu kuokolewa (1 Tim.2:3-4). Kazi zake hazikuwa bure, zilihusu uzima wa milele na wokovu wa watu. “wateule” alitumia lugha ya Agano la Kale kuhusu watu wa Mungu. Wateule ni wale wote ambao watakuja kuamini kutokana na bidii na taabu za wahubiri. Paulo alitaka kushiriki raha ya mbinguni pamoja na wengine wengi. Mwisho wa yote ni utukufu wa milele. Tusifikiri kwamba mateso yetu yana uwezo wa kukomboa ndani yake sawa na mateso ya Kristo, la! lakini maana ya Paulo ilikuwa wateule waokolewe kwa njia ya Injili na yeye Paulo hakuweza kuhubiri Injili bila taabu na mateso.

k.11-13 Hapo twakuta tena “neno la kuaminiwa” (1 Tim.1:15; 3:1; 4:9; Tito 3:8). Tangu kifungu cha kwanza Paulo alikuwa akimsihi Timotheo kusimama imara, akitumia mfano wa askari, mpiga mbio na mkulima kuonyesha kwamba hao wote hawafaulu wasipofanya bidii na kukubali taabu. Ndipo alimwambia amkumbuke Yesu Kristo na jinsi alivyoshindana na upinzani mkubwa na kujitoa hadi kufa, ambaye sasa yu hai milele na milele katika utukufu wa Mungu. Halafu Paulo alitaja mateso yake, hata wakati uleule alipokuwa akimwandikia alitendewa kama mhalifu wa hali ya juu, na kufungwa na mnyororo gerezani.

Hata hivyo hakusita katika imani yake. Alijua kwamba Neno la Mungu halifungwi iwapo mtumishi wake amefungwa. Shabaha yake ilikuwa kuleta watu kwa Kristo, na kwa vyovyote Mungu, anayependa watu wote waokolewe ataendeleza mapenzi yake ya kuokoa watu, na kwa sababu hiyo mateso yake hayatakuwa bure.

Ndipo alileta “neno la kuaminiwa” mbele za Timotheo, pengine maneno hayo ni wimbo au shairi lililotumika katika ibada.

k.11 “kama tukifa..” Kifungu hiki chafanana na Rumi 6:8 ambapo Paulo alizungumzia neno la ubatizo. Ni mfano wa maisha ya Kikristo; tunapomkubali Kristo twakana nafsi zetu, hatujali usalama wetu, twatwika msalaba na

kumfuata Kristo. (1 Kor.15:31; 2 Kor.4:10) Bila msalaba hamna taji.(Rum.8:17; 2 Kor.4:17).

k.12 “Kama tukistahimili...tutamiliki..” Yaliyompata Kristo sisi tutapata tukifuata vizuri nyayo zake. Hapo duniani magumu na mateso, baadaye utukufu na kumiliki. (Rum.8:17).

k.12b “kama tukimkana...yeye naye atatukana..” Matokeo ni makubwa tukikubali magumu na mateso kwa ajili ya Kristo. Kristo atatupokea kwa furaha kubwa huko mbele na kutukiri kuwa Wake mbele za Baba yake. Vilevile matokeo ni makubwa tukimkana Kristo. Je! kuna jambo zito kuliko Kristo kutukana? Hata Yesu Mwenyewe alitoa onyo (Mt.10:33). Lazima waumini wajiandae tayari kupambana na jambo lolote ambalo litaweza kuwashawishi kuondoka katika Imani yao. Tufahamu kabisa kwamba twaitwa kuyastahimili magumu yote kwa ajili ya Kristo.

k.13 Iwapo wengine walimwacha Kristo hata hivyo Mungu hakati tamaa, Yeye hudumu maminifu na makusudi yake ya kuokoa atayaendeleza, kwa kuwa tabia ya Mungu ni kuokoa. Kwa sababu hiyo Timotheo na wenzake wazidi kustahimili ili wamiliki pamoja na Kristo katika uzima wa milele. Mungu atakuwa pamoja nao katika shughuli zao za kuwavuta wengine kwa Kristo. Ila kwa upande wa pili watu wafahamu kwamba Mungu aliye mwaminifu atatimiza neno la kuwakana wale wote wanaomkana.

k.14-19 Mashauri juu ya waalimu wa uongo

k.14 Jambo kubwa la kwanza ni kusimamia na kuendeleza mafundisho ya kweli. Timotheo awakumbushe waumini hayo yote aliyosema Paulo, nao wajue kwa hakika kwamba kustahimili ni njia ya Kristo itakayowafikisha kwenye uzima wa milele. Uzito wa jambo hilo unaonyeshwa katika maneno “ukiwaonya machoni pa Mungu” (1 Tim.5:21). Waepukane na mashindano ya maneno yasiyo na faida yoyote. Bila shaka wengine walitaka kushindana kwa sababu ya kiburi chao na kujiona kwao wakidhani watafaulu kunyamazisha wale waalimu wa uongo, lakini Paulo aliona njia hiyo ni ya hatari na upotevu.

k.15-16 Timotheo mwenyewe alitumie Neno la Mungu kwa halali, asiwe mjanja wala asiwe na hila. Aseme kweli wazi bila mapambo ya maneno mengi. Awe mnyofu kwa habari ya kweli Kwa kufanya hivyo atakuwa mtenda kazi mwenye kibali cha Bwana wake, pia atanyosha njia kwa wengine kuifuata kweli bila kuchanganyiwa, na yeye mwenyewe hatasikia haya. Njia ya kweli ikidhihirika wazi ndipo hitilafu yoyote katika mafundisho ya wengine itaonekana.

k.17-18 Lakini walikuwapo watenda kazi wabaya, ambao hawakunyoka katika kufundisha neno la kweli bali waligeuka upande, nao waliikosa ile kweli wakisema kwamba kiyama imekwisha kutokea. (1 Tim.1:6: 6:21). Shida ni

kwamba waalimu wa aina hii waliipindua imani ya wengine na Paulo alitambua kwamba bila Timotheo na waumini wa kweli kusimama imara na kuwapinga mafundisho ya uongo yatazidi kuenea. Paulo alitaja watu wawili Himenayo (1 Tim.1:20) na Fileto, pengine hao walikuwa viongozi. Hatari ni kwamba mafundisho ya uongo ni mfano wa donda-ndugu yanayoenea kwa haraka sana.

k.19 Timotheo ajue hakika kwamba iwapo walikuwa watu wasiofaa waliojitahidi kuzishambulia kweli za Mungu na imani za watu, hata hivyo Jengo ni imara kwa sababu Mungu anatenda kazi pale Efeso naye anajua walio wake hasa, hadanganyiwi na maneno ya wengine, na kipimo kwa watu kuuhakikishia uaminifu wao ni kuuacha uovu. Ni faraja kubwa kwa Timotheo kufahamu hayo, awe thabiti. Muhuri mmoja ni wa siri, hauonekani, na wa pili ni wa nje na wazi. Mungu huuona moyo, sisi twaona maisha. (Hes.16:5,26).

2:20-21 Mfano wa vyombo katika nyumba

Katika nyumba vimo vyombo ainaaina, vingine vizuri, vya heshima, na vingine havina. Huenda Paulo alikuwa akipambanua kati ya Himenayo na Fileto na Timotheo na wazee wa kweli. Hapo nyuma alitumia mfano wa “mtenda kazi” hapo alitumia mfano wa vyombo vilivyo na heshima na vyombo vilivyokosa heshima. Sharti moja ni mtu ajitakase kwa kujitenga na mafundisho ya uongo ndipo atakuwa chombo safi, kimfaacho Bwana, chombo kilicho tayari kwa kila kazi nzuri. Ni heshima ya hali ya juu kuwa chombo ambacho Bwana Yesu aweza kukitumia. Ni wajibu wetu kufanya juu chini ili maisha yetu yawe safi kwa ajili yake.

k.22-26 Wajibu wa Timotheo kuhusu waalimu wa uongo

Paulo alisema tena na Timotheo na kumshauri kwa nguvu kukimbia tamaa za ujanani. Vijana huwa na tamaa mbalimbali, wana haraka, wapenda mapya, watafuta makubwa, wapenda kudadisi na kujadiliana n.k. Timotheo akimbie tamaa hizo. Neno “kukimbia” ni neno la kuonyesha jinsi ilivyompasa aende kinyume cha hayo yote. Badala ya hali hizo, afuate haki, imani, upendo na amani, pamoja na waumini wenzake wenye moyo safi waliomwita Bwana awasaidie. Twakumbushwa habari za Yusufu, jinsi alivyokimbia dhambi, hakukubali kubaki na mke wa Potifa, (Mw.39:12). Wala tunapojaribiwa tusisitesite kama mke wa Lutu aliyekawia wakati wa Mungu kuleta hukumu juu ya Sodoma na Gomora (Mw.19:15,16).Twawajibika kukimbia hatari za kiroho na kukimbilia mema ya kiroho, yaani kufuata kwa bidii yale tunayoyajua ni sawa.

k.23-24 Timotheo akatae kabisa kusikiliza maswali na kuingia majadiliano kwa sababu mwisho wake ni ugomvi, na haimpasi mtumishi wa Bwana kuwa mgomvi. Awe mvumilivu na mpole katika kufundisha kwake, awe na adabu ili awavute watu polepole mpaka watakapoitambua kweli.

k.25 Awaonye wapinzani ila si kwa ukali. Twajifunza kwamba ni lazima watumishi wa Bwana wawe na msimamo, wawe imara, huku wakiwa wapole na wenye adabu. Bwana Yesu alijishuhudia upole wake (Mt.11:28). Katika Isaya na Nyimbo za Mtumishi picha ni ya Mtumishi Mpole, Mtumishi ateswaye bila kusema neno.

Ni Mungu tu mwenye uwezo wa kuwasaidia watu kutambua kweli na kuwapa watu nia ya kutubu na kuuacha upinzani wao na maisha yao mabaya na mafundisho ya uongo. Ni Shetani ambaye amewaloga na sumu ya uongo na kuwatega akiwatumia waalimu wa uongo katika kuwadanganya. Watu ni wa kuhurumiwa, watu walihitaji kuwekwa huru na kutoka chini ya utumwa wa Shetani. Kwa maneno hayo Paulo alionyesha tumaini la wengine kutubu na kumrudia Bwana.

Tusifikiri watumishi wa Bwana hawaruhusiwi kushindana kwa ajili ya Injili (Gal.2:11-14) Katika 1 Tim.6:12 Paulo alisema “piga vita vile vizuri vya imani (2 Tim.4:7), Paulo alikuwa akimshauri Timotheo kuepukana na majadiliano yote yasiyo ya maana juu ya mambo madogomadogo, ya bure.

3:1-9 Maovu yanayokuja

Paulo alianza sehemu hiyo kwa kumwambia Timotheo “ufahamu neno hili”. Je! Timotheo hakufahamu kwamba maovu yalikuwa yameenea sana. Ilikuwa wazi kwamba Injili ilipingwa sana, hata Paulo mhubiri wake alikuwa kifungoni kwa ajili yake. Wengi katika Asia walikuwa wamemwacha (1:15) na waalimu wa uongo walieneza mafundisho yao ya uongo. Kwa nini Paulo alisema “ufahamu neno hilo”. Ni kwa sababu alitaka kukaza kwamba kule kupingwa kwa Injili si jambo la muda ambalo litapita, bali ni kawaida. Timotheo asifikiri kwamba akitulia basi dhoruba itapita. La! siyo.

“siku za mwisho” tusifikiri hizo ni za baadaye kabla ya Kristo kurudi kwa mara ya pili. Katika Agano Jipya zamani za kale zilikwisha Yesu alipokuja kwa mara ya kwanza, ndipo dahari mpya ilianza na “siku za mwisho”. (Mdo.2:14-17; Ebr.1:1-2). Kwa hiyo yanayofuata ni maelezo ya wakati wote mpaka Kristo atakaporudi. Tazama jinsi Paulo alivyomwambia Timotheo ajiepushe na watu fulani k.5. Mbeleni mambo yatazidi kuwa mabaya k.13, lakini hata wakati wake yalikuwa mabaya.

Kutakuwa na vipindi vya hatari sana, vinavyosababishwa na watu. Kwa hiyo, Timotheo akifahamu neno hilo, na sisi pia tukilifahamu, basi tutaandaa tayari kupambana nayo.

k.2-5 Hapo Paulo ameorodhesha dhambi na tabia mbaya, maneno “kupenda” na “kutopenda” yatokea mara kwa mara.Kwanza kabisa watu watajipenda, ndiyo asili ya shida nyingi. Watapenda fedha, neno hilo lilitajwa (1 Tim.6:10ku)

watu watajiona na kujisifu, watakuwa watukanaji. Tena wataonyesha tabia zilizo kinyume cha kawaida ya wanadamu, maana hawatapenda wazazi wao wala ndugu zao. Watakosa shukrani, watu wasio na maisha safi. Hawatataka kuwasamehe wengine. Ni wapenda anasa badala ya kumpenda Mungu. Wataweka raha na anasa mahali pa Mungu. Ila hawatupi dini, ila hawairuhusu ibadili maisha yao, dini ni kama hirizi ya kuvaa nje bila kuiruhusu kuwabadili ndani.

k.5 Paulo alimwonya Timotheo wazi “ujiepushe nao” wala asiwape nafasi kupenya shirika za Kikristo na kuwaambikiza waumini.

k.6-7 Hao wabaya walithubutu kutafuta watu na kuwateka mateka na mafundisho yao. Walitumia njia za chinichini ili wapate nafasi kuingia katika nyumba za watu. Huenda walichagua saa ile ambayo walidhani bwana wa nyumba hatakuwepo, ndipo wakamshawishi mama wa nyumba. Bila shaka walilenga wale wanawake wavivu, wenye tamaa nyingi, wale wasiokuwa na msimamo, walio wepesi kuwasikiliza.

k.8-9 Paulo aliona mfano wake katika Farao kumpinga Musa. Yane na Yambre hawatajwi katika Biblia, majina yaonekana katika mapokeo ya Kiyahudi. Walikuwa wachawi au waganga wa Farao (Kut.7:11) nao walimpinga Musa. Kwa hiyo, tangu zamani watu wameipinga kweli; ila faraja kwa Timotheo na sisi ni kwamba hawataendelea sana, kwa sababu, muda si muda, ujinga wao utaonekana, nao watapotea. Uovu na uongo una mbegu za uharibifu ndani yake.

3:10-17 Kwa mara nyingine Paulo amsihi Timotheo

k.10 na k.14 twakuta maneno “bali wewe”. Paulo alirudi kusema na Timotheo, ni wazi kwamba Timotheo alitawala mawazo yake, akijua umuhimu wa Timotheo kusimama imara kati ya mabaya yaliyomzunguka.

Paulo amempa kielelezo chema katika mengi. Pamoja na kuona kielelezo chake Timotheo mwenyewe alikata shauri kukanyaga nyako zake. Neno kubwa la kwanza ameyafuata mafundisho yake, ndipo mwenendo wake katika maisha ya kila siku. Timotheo amehakikishiwa ukweli wa mafundisho yake katika kuyatekeleza kimaisha. Wala si hivyo tu, Timotheo amefahamu na kukubali makusudi yake ya kuieneza na kuipigania Injili. Ameona imani na uvumilivu wa Paulo na upendo na subira yake.

Halafu Paulo alimkumbusha mateso yake ya zamani yaliyompata katika safari za uinjilisti. Timotheo alitoka Listra, huenda alikuwepo siku ile Paulo alipopigwa mawe (Mdo.14:19-20, 16:1). Paulo hakutaja habari hizo kwa kujiinua na kuuonyesha uzuri wake, bali lengo lake lilikuwa kumtia moyo Timotheo.

k.12 Lakini Timotheo asiwaze kwamba yaliyompata Paulo ni la kipekee, la! Paulo alisema ni kawaida ya maisha ya Kikristo. Wote watakaoishi maisha ya utauwa wataudhiwa. Bwana Yesu alisema vivyo hivyo (Yoh.15:18-20; 16:33). Tangu mwanzo Wakristo walifundishwa neno hilo (Mdo.14:22) na zamani zile wengi walimpokea Kristo kati ya vipingamizi vingi.

k.13 Wale wabaya wataendelea katika mienendo yao mibaya na kuzidi kuwa waovu. Waliwadanganya wengine, huko wao wenyewe wamedanganyika.

k.14 “bali wewe” Timotheo awajibika kudumu katika ile kweli ambayo ana uhakika nayo. Wale waalimu wa uongo walipenda sana kutafititafiti mambo mapya lakini yampasa Timotheo awe radhi na yale anayoyajua ni sawa. Aliwafahamu waliomfundisha, yaani Paulo na wenzake, aliweza kutazama kwa ukaribu sana maisha yao. Pia alisaidiwa sana na malezi ya nyumbani kutoka kwa mama na bibi yake.

k.15-16 Tena, tangu utoto alielimishwa katika Maandiko Matakifu. Mama na bibi walimfundisha Agano la Kale. Kwa Maandiko alipata kujua habari za wokovu (Mdo.26:22ku. Rum.1:2). Bila shaka walimfundisha tumaini la kuja kwa Masihi. Shabaha ya Maandiko imewekwa wazi “kukuhekimisha hata upate wokovu”. Maandiko ni kama kidole cha kuelekeza mtu kwa Yesu Kristo.

Twaambiwa mambo mawili kuhusu Maandiko. Kwanza yamepuliziwa na Mungu, yametoka Kwake, ni Neno la Mungu. Uwezo wake ni katika asili yake katika Mungu. Pili, yafaa. Kama Myahudi, alifahamu na kuamini kwamba Maandiko ni pumzi ya Mungu, lakini Paulo alitaka kumkumbusha faida yake.

Yafaa kwa mambo gani? Kwanza, kwa mafundisho ili mtu ajue na kutambua ayaamini nini. Kwa upande wa pili Maandiko yafaa kuonyesha watu makosa yao. Tena, yafaa kuwaongoza watu ili wajifunze iwapasayo, kusudi wafanye yaliyo haki na sawa.

Maandiko yafaa kwa kuwaelimisha watu yaliyo kweli na kuyakemea makosa. Wajibu mkubwa wa Timotheo pale Efeso ni kuwaelekeza watu kuishi katika hali ya kumpendeza Mungu na kutenda yaliyo na kibali machoni mwake.

k.17 Pamoja na hayo kwa Maandiko Mungu humsaidia mtu kukua kiroho na kutimiza mapenzi yake katika kufanya kila tendo jema (Ef.2:8-10). Maandiko ni chombo cha kumwezesha mtu kutekeleza kazi yake, mtu wa Mungu ni mtu wa Neno la Mungu. Bila shaka neno hilo lilimhusu Timotheo, ili awe mtiifu kwa Mungu, kwa Paulo, na kwa Maandiko.

4:1-5 Agizo la mwisho la Paulo kwa Timotheo

Hapo twafikia maneno ya mwisho tuliyo nayo ya Paulo yaliyoandikwa muda mfupi kabla ya kuuawa kwake. Paulo alikuwa mzee, alikuwa ametumika miaka mingi, na sasa yumo gerezani pale Rumi akiingojea hukumu ya kesi yake. Jambo kubwa mbele yake kabla ya kufa ni kumtayarisha Timotheo na watu kama Tito, ila watumike katika Injili kama yeye.

Katika 1 Tim.5:21 Paulo alitoa agizo kubwa kwa Timotheo ndipo sasa alitoa agizo zito sana. Uzito unaonekana katika maneno “nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Yesu Kristo atakayewahukumu walio hai na waliokufa...” Kristo ni mhukumu wa watu wote, ambaye atakaporudi ataitekeleza hiyo hukumu. Atakaporudi tena Ufalme wa Mungu utaingizwa kwa nguvu na falme na tawala zingine zote zitakwisha. Timotheo awe na uhakika wa makubwa hayo, kuyawaza hayo yatamtia moyo wa kudumu kuwa mwaminifu. Uzito uliongezwa kwa kujua kwamba ni mausia ya mwisho kutoka kwa Paulo, baba yake kiimani, hali akikaribia kufa.

k.2 Agizo lenyewe lilikuwa nini? Lilikuwa “lihubiri neno, karipia, kemea, onyo kwa uvumilivu wote na mafundisho” Yampasa Timotheo akate shauri kabisa kabisa kuihubiri Injili na kuendelea kuihubiri, haidhuru mazingara na hali zilizopo ni nzuri au mbaya. Yeye mwenyewe asifuate hali ya hewa bali awe tayari kuhubiri wakati wote.

Anapohubiri alingane na hali na mahitaji ya watu. Kwa maisha yao wengine watahitaji kukaripiwa, wengine kukemewa, na wengine kuonywa, kusudi mafundisho yake yaguse maisha yao ya kila siku. Kwa kufanya hivyo watu watasaidiwa. Iwapo atapenda sana watu waokolewe asiwasukume kinyume cha nia yao, budi awe mvumilivu. Tena afanye hivyo kwa kuwafundisha ili waelewe kwa nini mengine hayakubalika. Kukemea bila kuwafundisha ni kubakiza shina la kosa ambalo huenda litachipuka tena baadaye.

k.3-4 Hata wakati ule Injili ilipingwa na Paulo aliona ya kuwa siku za usoni itazidi kupingwa. Watu watakataa kuyasikiliza mafundisho yenye uzima, watawatafutia waalimu watakaowafurahisha na mafundisho ya hadithi hadithi, mafundisho yasiyo na lengo wala maana. Tumesikia mengi juu ya waalimu wa uongo lakini hapo Paulo amewalaumu watu kwa sababu walitaka mafundisho ya uongo. Walikuwa na “masikio ya utafiti” hawakutaka kujua kweli Watu ambao tayari wamekata shauri ni nini wanayotaka kuyasikia. Hawawi tayari kusikiliza mafundisho kwanza, ndipo kuamua yapi ni ya kweli, na ya kuwafaa, maana wamekwisha kujiepushe na kweli na kugeukia uongo.

k.5 “bali wewe” (4:10, 14) Timotheo awe tofauti na wale wala asifuate kawaida ya siku zake. Awe na kiasi katika mambo yote, asiyumbeyumbe (1 The.5:6), awe macho, aendelee tu. Kwa sababu haridhiani nao kwa vyovyote

watamfanyia mabaya, na kwa sababu hiyo budi awe tayari kuvumilia. Afanye kazi yake ya kuihubiri Injili kwa sababu ni kazi ya maana na wajibu wake mkubwa. Injili ni ya kuenezwa si ya kuhifadhiwa tu.

Timotheo aitimize huduma yake kwa sababu amekwisha kuiweka mikono yake kwenye plau, asiangalie nyuma bali akazane kutimiza huduma aliyopewa. Twajifunza kwamba haitupasi kulegea wakati mgumu, wala si vizuri tuwe kimya eti watu hawataki kuhubiriwa Injili.

k.6-8 Kwa Paulo, mambo yamefikia upeo. Kwa sababu kuuawa kwake kumekaribia, “mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika” Paulo amemaliza huduma yake na mwenendo wake. Alitumia neno “namiminwa”, anatoa maisha yake kwa Mungu mpaka kufa kama dhabihu, maisha yake yanamwagwa kama dhabihu kwenye madhahabu (Flp.2:17). Ni karibu kabisa hata aliandika kama kumeanza tayari. “kufariki kwangu” neno linalotumika ni lile la meli kuondoka bandarini kuanza safari, au la askari kung'oa hema, au mnyama kufunguliwa kwa kazi.(Flp.1:21). Kwa Timotheo ni mwisho wa kushirikiana na Paulo, bali kwa Paulo ni kuingia ulimwengu mpya (Flp.1:23), ili aanze maisha mapya mbali na vizuizi vya hapo duniani.

k.7 Paulo alitazama nyuma kwa huduma yake ya kama miaka thelathini, halafu akaijumlisha kwa kifupi sana akitaja mambo matatu. Jambo moja “nimevipiga vita vilivyo vizuri” la pili “mwendo nimeumaliza” na la tatu; “Imani nimeilinda”. Kama askari mwema wa Kristo amepiga vita vyake vizuri; kama mshindani wa mbio ameumaliza mwendo wake; na kama Mlinzi Mwaminifu ameilinda Imani, amedumu mwaminifu kwa Injili, na kuilinda kama hazina ya thamani sana. Hayo yote yalimgharimia kazi za taabu, kujitoa kabisa, na kujihatarisha nafsi yake. Tangu kuitwa hadi kufikia hatua ya uzee amekuwa mwaminifu.

Inayombakia ni tuzo - taji ya haki iliyomo mikononi mwa Bwana Yesu, naye atamvika Siku ile ya mwisho, Yesu atakapofunuliwa. Kaisari Nero aweza kukosa katika uamuzi wa kesi yake, ila Yesu kamwe hawezi kukosa, ni Mhukumu wa haki. Taji ni haki (Flp.3:9) Alihesabiwa haki kwa imani, na amezidi kuwa na tabia ya haki ya ndani kutokana na kazi ya Mungu ndani yake thibitisho la maisha yake kuwa yamekubalika mbele za Mungu. Wala si yeye peke yake atakayepewa - ni kwa wote wampendao Bwana Yesu, wanaotamani na kutazamia Kurudi Kwake, Timotheo akiwa miongoni mwao.

k.9-18 Maagizo na maneno ya kibinafsi ya Paulo
Hapo twasoma habari ya mipango ya Paulo kabla ya kuondoka kwake.

k.9 na k.21 Ombi lake la kwanza ni kwa Timotheo kuja kwake upesi. Paulo hakutumaini kwamba atafunguliwa, kwa hiyo, kwa sababu ya uhusiano wa ukaribu sana na Timotheo alipenda kuonana na “mwana wake”. Katika barua

amempa maagizo na mashauri jinsi ya kuendelea baadaye, hata hivyo, alikuwa na mambo kusema naye uso kwa uso.

k.10 Dema alikuwa amekaa na Paulo lakini alishindwa kuvumilia magumu na iwapo alikuwa mmoja wa wajoli wake kwa muda mrefu akamwacha na kurudi Thesalonike. (Flm.24; Kol.4:14). Kama aliacha kumwamini Kristo hatujui, maana Paulo alisema “aliniacha akiupenda ulimwengu wa sasa”. Pengine hakupenda kushiriki taabu za Paulo. Bila shaka Paulo aliumizwa sana kwa kuachwa na Dema, iwapo Luka alikuwa pamoja naye k.11.

Paulo alimpasha habari za wengine. Kreske ambaye hakutajwa mahali pengine katika Agano Jipya alikwenda Galatia. Tito ambaye hapa nyuma aliachwa Krete alikuwa amekwenda Dalmatia, na Paulo alimtuma Tikiko mpaka Efeso badala ya Timotheo. (Ef.6:21,23, Kol.4:7.8; Tito 3:12) Paulo alimwita Tikiko “ndugu mpendwa” “mjoli wangu”. Yawezekana ni yeye aliyepewa barua hiyo kumpelekea Timotheo, ndipo yeye abaki pale Efeso na Timotheo apate nafasi ya kumfikia Paulo huko Rumi.

k.11 Ila mmoja amebaki pale Rumi kwa Paulo, ni Luka, “tabibi mpendwa” (Kol.4:10).

Paulo alitaka Timotheo ameletee vitu vitatu. Kwanza, amlete Marko pamoja naye. Zamani Paulo na Marko walifarakana kwa sababu katika Safari kubwa ya kwanza Marko aliwaacha kabla ya kumaliza safari (Mdo.12:25; 13:13; 15:38, 39) na Paulo hakuwa tayari kumchukua kwa Safari ya pili. Hatuna habari jinsi walivyopatanishwa lakini twajua walitengeneza mambo yao (Kol.4:10; Flm.24; 1Pet.5:13) Paulo aliona ya kuwa atamfaa pale Rumi.

Paulo alimwomba Timotheo alilete joho lake aliloliacha kwa Karpo huko Troa. Kwa neno hilo twajifunza kwamba Paulo alikuwa Troa kabla au wakati wa kukamatwa. Bila shaka alitaka kukinga baridi ya chumba chake wakati wa baridi uliokaribia k.21.

Pamoja na joho alitaka vitabu fulani, hasa vile vya ngozi. Ni vitabu gani? Wengine wametoa wazo ni Hati ya sheria na hati ya Uraia wake wa Kirumi. Wengine hufikiri ni Maandiko ya Agano la Kale, au pengine ni Kitabu chenye habari za Matendo na Misemo ya Bwana Yesu. Hatujui, ila twajua Paulo alivitaka vile vitabu. Ajabu ni kwamba iwapo Paulo alisafiri sana na kufanya kazi usiku na mchana, hata hivyo, alijiwekea nafasi ya kusoma na kuandika vitabu.

k.14-15 Alimwonya Timotheo juu ya Iskanda, mfua shaba. Watu wengi walikuwa na jina hilo, kwa hivyo si lazima awe yule aliyetajwa katika 1 Tim.1:20 au Mdo.19:33.



Vitabu vya Karne ya kwanza

Paulo hakutoboa ni ubaya gani aliotendewa na Iskanda, wengine wanafikiri ni yeye aliyewapasha viongozi juu yake na kusababisha kukamatwa kwake. Pengine jambo hilo lilitokea pale Troa na ndiyo sababu Timotheo alionywa juu yake, maana Timotheo atapitia Troa kwa kuchukua joho na vitabu, njiani kwenda kwa Paulo. Huenda ni sababu ya Paulo kuviacha vile vitu. Hasa picha ni ya Iskanda kumpinga Paulo na ujumbe wake.

k.16-17 Paulo alipoletwa mahakamani kwa mara ya kwanza hakuna mtu aliyethubutu kumtetea, akabaki peke yake, wote wengine wakiogopa kujiunga naye. Paulo aliomba wasihesabiwe kosa hilo, akifuata kielelezo cha Bwana Yesu. Lakini katika upweke huo na katika hatari hiyo Bwana Yesu alikuwa pamoja naye na kumtia nguvu. Pengine alijaliwa maono. Bila shaka alipewa nafasi ya kuieleza Injili aliyohubiri. Mwishowe alisema “nikaokolewa katika kinywa cha simba”. Neno hilo ni tofauti na tazamio lake la k.6-8; na k.18. “Bwana ataniokoa na kila neno baya”. Pengine Paulo alikuwa na maana ya kiroho si ya kimwili. Zaidi ya kumwokoa Bwana atamhifadhi hata kumfikisha

kwenye ufalme wake wa mbinguni. Paulo amekaza mawazo yake kwa mambo ya mbinguni kuliko kufunguliwa.

k.19-23 Salaam za mwisho

Paulo alituma salaam kwa Priska na Akila rafiki zake wa siku nyingi (Mdo.18:18, 26; Rum.16:3; Mdo.18:2; 1 Kor.16:19). Pia alituma salaam kwa nyumbani mwa Onesiforo (1:16,17) ni huyo aliyemtafuta kwa bidii pale Rumi. Mwingine wa kusalimiwa ni Erasto wa Korintho (Rum.16:23) au labda ni Erasto aliyetajwa katika Mdo.19:22 aliyetumwa Makedonia pamoja na Timotheo. Trofimo alikwenda na Paulo mpaka Mileto na alikuwa Yerusalemu pamoja na Paulo (Mdo.20:4 Mdo.21:29).

k.21 Halafu Paulo alirudia kumwomba Timotheo aje kwake kabla ya wakati wa baridi. Huenda Paulo alitaka asafiri kabla ya hali ya hewa kumzuia.

Ndipo Paulo alitaja kwa majina wakristo wanne walioko Rumi ambao walituma salaam zao kwa Timotheo. Ni mara ya kwanza hao kutajwa, bila shaka ni waumini wa pale Rumi, ambao wamemtembelea pale gerezani. Paulo aliongeza “na ndugu wote pia”.

k.22 Kisha Paulo aliagana na Timotheo kwa maneno “Bwana na awe pamoja na roho yako” na katika sehemu ya pili aliandika “Neema iwe pamoja nanyi” neno kwa waumini wote walio pamoja na Timotheo pale Efeso.